

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA MBILI

Kikao cha Ishirini na Tano - Tarehe 16 Julai, 2003

(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA SAYANSI, TEKNOLOJIA NA ELIMU YA JUU:

Hotuba ya Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu kwa Mwaka wa Fedha 2003/2004.

MHE. MARGARETH A. MKANGA (k.n.y. MHE. OMAR S. KWAANGW' - MWENYEKITI WA KAMATI YA HUDUMA ZA JAMII):

Taarifa ya Kamati ya Huduma za Jamii kuhusu utekelezaji wa Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu katika mwaka uliopita, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka 2003/2004.

MASWALI NA MAJIBU

Na. 239

Majimbo ya Uchaguzi

MHE. JAMES P. MUSALIKA (k.n.y. MHE. DR. WILLIAM F. SHIJA) aliuliza:-

Kwa kuwa baadhi ya Majimbo ya Uchaguzi ni makubwa sana kijiografia na kwa wingi wa watu; je, Serikali itashauriana na Tume ya Uchaguzi ili kuongeza Majimbo ya Uchaguzi katika baadhi ya maeneo nchini katika Uchaguzi wa mwaka 2005?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. MUHAMMED SEIF KHATIB) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Dr. William Shija, Mbunge wa Sengerema, naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, lilipokuwa linajibiwa swali la Mheshimiwa Ireneus Ngwatura, Mbunge wa Jimbo la Mbinga Magharibi na pia swali la Mheshimiwa Sophia Simba, Mbunge wa Viti Maalum, CCM

katika Mikutano ya Saba na Kumi na Moja sawia ya Bungeni, nilieleza kwamba, kwa mujibu wa Ibara ya 75(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania 1977, Jamhuri ya Muungano inaweza kugawanywa katika Majimbo ya Uchaguzi kwa idadi na namna itakavyoamuliwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi baada ya kupata kibali cha Mheshimiwa Rais. Ibara ya 75(4) ya Katiba inatoa maelezo zaidi kuwa Tume ya Uchaguzi inaweza kugawa Majimbo ya Uchaguzi ya Wabunge mara kwa mara angalau kila baada ya miaka 10.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya machache ya utangulizi, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. William Shija, kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa Tume ya Uchaguzi kisheria ilichunguza na kuigawa Jamhuri ya Muungano katika Majimbo ya Uchaguzi kwa mara ya mwisho mwaka 1995, sasa inaweza kuchunguza na kugawa Majimbo ya Uchaguzi mwaka 2005, endapo itakuwepo haja ya kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoliarifu Bunge hili, lilipojibiwa swali la nyongeza la Mheshimiwa Sophia Simba, kwamba muda ukifika, Majimbo yatatazamwa upya kwa nchi nzima kutegemea na hali itakavyojitokeza. Serikali itatekeleza azma hiyo, kwa kuhakikisha unakuwepo ushirikiano wakati Tume ya Uchaguzi itakapotokea kugawa Majimbo ya Uchaguzi, kwa kutumia vigezo vifuatavyo ambavyo hutazamwa kwa pamoja:-

- (a) Idadi ya watu;
- (b) Hali ya Kijiografia ya eneo na uchumi wa eneo linalokusudiwa kugawanywa;
- (c) Mipaka ya kiutawala kwa vile Jimbo la Uchaguzi linatakiwa liwe ndani ya Mipaka ya Wilaya;
- (d) Mgawanyo wa mipaka ya Kata ya kila Wilaya ambayo hutangazwa na Waziri anayehusika na Serikali za Mitaa; na
- (e) Upatikanaji wa njia za Mawasiliano.

Kwa hiyo, vigezo vya ukubwa wa baadhi ya Majimbo ya Uchaguzi kijiografia na wingi wa watu, sio vigezo pekee vyenye kufanya Majimbo ya Uchaguzi yagawanywe.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge waamini na kukubali kuwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, itatekeleza majukumu yake na itaifanyia kazi suala hili kabla ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2005.

MHE. JAMES P. MUSALIKA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa yapo Majimbo makubwa sana na yenye watu wengi sana hapa nchini na Majimbo mengine ni madogo madogo na yana watu wachache sana.

Je, Serikali haioni kwamba haiwatendei haki wale Waheshimiwa Wabunge wenye Majimbo makubwa sana kwa kuwapa nyenzo sawa na wale wenye Majimbo madogo na kwamba sasa Serikali irekebisha kasoro hiyo na ikishairekebisha itakuwa tayari kutoa fidia kwa Waheshimiwa Wabunge wenye Majimbo makubwa ambao kwa muda mrefu wamesota? (*Makofi*)

(b) Kwa kuwa kadri Waheshimiwa Wabunge wanavyokuwa wengi kwenye maeneo makubwa ndivyo wanavyosaidiana kuisihi Serikali na kuiomba kusaidia maendeleo kama vile barabara za maeneo hayo hususan barabara ya Busisi katika Jimbo la Sengerema mpaka Nyakongolo katika Jimbo la Nyang'hwale. Je, Serikali sasa itakuwa tayari kugawa Jimbo la Sengerema, Jimbo la Nyang'hwale, Jimbo la Busanda na Geita, ili Waheshimiwa Wabunge wasaidiane kuisihi Serikali kuleta maendeleo huko? (*Makofi*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. MUHAMMED SEIF KHATIB): Mheshimiwa Spika, nimeeleza katika majibu yangu ya msingi kwamba vigezo vitano ambavyo vinatumiwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi katika kugawa Majimbo ya Uchaguzi na vigezo hivyo vimo ndani ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kwa hiyo, nafikiri kwamba Tume ya Taifa ya Uchaguzi imefanya haki kugawanya Majimbo ambapo Waheshimiwa Wabunge wote ambao wamo ndani ya Bunge hili ni Waheshimiwa Wabunge halali kwa mujibu wa vigezo hivyo. Majimbo yanagawanywa pia kwa kufuata idadi ya watu. Wakati tunayagawa Majimbo haya ilifikiriwa kwamba angalau idadi ya watu 100,000 kwa Majimbo ya Tanzania Bara na watu 10,000 kwa Jimbo la Tanzania Visiwani. Lakini nasema kwamba vigezo vya watu pekee yake havitoshi.

Mheshimiwa Spika, la pili ni kwamba wakati ukifika maoni ya Mheshimiwa James Musalika na Waheshimiwa Wabunge wengine pia yatazingatiwa kuona kwamba kama inawezekana kugawa zaidi Majimbo hayo kwa mujibu wa vigezo vilivyowekwa na sheria.

MHE. HASNAIN M. MURJI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niulize swali la nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, kwa kuwa mwaka 1995 kuna Majimbo yalifutwa kama Jimbo la Mitema. Je, Serikali sasa inasemaje kuhusu kurudisha Jimbo hilo na Tume ya Taifa ya Uchaguzi iliahidi kwamba mwaka 2005 watarudisha Jimbo hilo?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. MUHAMMED SEIF KHATIB): Mheshimiwa Spika, sidhani kwa nini Waheshimiwa Wabunge wana haraka sana kukimbia kabla ya wakati wake. Pili, wakati ukifika Tume ya Taifa ya Uchaguzi itaangalia Majimbo yote na kuyagawa upya kama haja itakuwepo. Subirini tusiwe na haraka sana. (*Makofi*)

Na. 240

Idadi ya Wabunge wa Viti Maalum Bungeni

MHE. KHADIJA SALEH NGOZI aliuliza:-

Kwa kuwa Wabunge wa Viti Maalum ni moja ya aina ya Wabunge wanaounda Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chini ya Ibara ya 66(1)(b) ya Katiba ya Nchi, kwamba idadi hiyo iongezeke kuanzia asilimia 20 ya Wabunge waliotajwa katika aya (a), (c) na (d); na kwa kuwa Kamati ya Kuratibu maoni kuhusu Katiba (*White Paper*) katika Hoja ya Nane (c) ambayo ilihusu “Kama utaratibu wa Viti Maalum vya Wanawake uendelezwe na Idadi ya viti hivyo iongezwe,” ilipendekezwa kuwa idadi ya Viti vya Wabunge Wanawake iongezwe hadi kufikia asilimia 30 ya Viti vya Wabunge wote.

Je, Serikali iliukubali ushauri huo wa Kamati na kama iliukubali lengo la utekelezaji wake wa asilimia 30 litafikiwa lini?

WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Khadija Saleh Ngozi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Nakubaliana na Mheshimiwa Hadija Saleh Ngozi, kuwa kwa Mujibu wa Ibara ya 66(1)(b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Wabunge wa Viti Maalum ni aina mojawapo ya Wabunge wanaounda Bunge la Jamhuri ya Muungano. Lengo la kuwepo Viti hivi na ni hatua ya makusudi ya kuleta uwiano wa kijinsia katika uwakilishi Bungeni. Ni kweli pia kwamba Kamati ya Kuratibu Maoni ya Wananchi kuhusu Katiba (*White Paper*) ilipendekeza kuwa idadi ya Viti Maalum vya Wabunge Wanawake viongezwe kutoka asilimia 15 iliyokuwepo hadi kufikia asilimia 30 ya Viti vya Wabunge wote.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilikubali ushauri huo wa Kamati na kuandaa Muswada wa Marekebisho ya Katiba yaliyopitishwa na Bunge na kuongeza idadi kutoka asilimia 15 hadi kufikia asilimia 20. Ingawa Serikali ina nia ya kuongeza idadi ya Viti Maalum toka asilimia 20 ya hivi sasa hadi asilimia 30, ipo misingi mingine ya kuzingatia ikiwepo ufinyu wa nafasi katika jengo hili. Hivyo, idadi ya Wabunge wa Viti Maalum itaweza kufikia asilimia 30 katika muda muafaka baada ya kuzingatia vigezo vyote likiwepo suala la ukumbi.

MHE. KHADIJA SALEH NGOZI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa yapo mapendekezo mengi kwenye taarifa hiyo ya Jaji Robert Kisanga; je, ingingekuwa vyema kwa Serikali kuwajulisha wananchi kupitia kwa Waheshimiwa Wabunge wao ni mapendekezo gani yamekubaliwa, yapi ambayo yamekataliwa na yapi yanaendelea kufanyiwa kazi?

(b) Kwa kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imetekeleza asilimia hiyo kwa wanawake wengi kuingia katika Baraza la Wawakilishi. Je, kwa upande wa Tanzania Bara suala hili litatekelezwa lini huku ukizingatia kuwa Serikali mbili utendaji wake unakwenda sambamba? (*Makofi*)

WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA: Mheshimiwa Spika, kwanza nichukue nafasi hii kukupa pole kwa kufiwa na kaka yako.

Mheshimiwa Spika, suala la kuongeza kama nilivyolizungumza katika jibu langu la msingi idadi ya wawakilishi wa Viti Maalum kufikia asilimia 30 liko katika ripoti ya Jaji Robert Kisanga na ripoti hiyo iliwasilishwa ndani ya Bunge hili ikazungumzwa na kukawa kuna maafikiano. Kwa hiyo, suala hili linafahamika kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, pili, kuongeza idadi kufikia asilimia 30 katika Bunge hili ukilinganisha na idadi hiyo katika Baraza la Wawakilishi ni kweli zipo tafouti hizo, lakini tunakwenda kwa wakati. Nadhani ikifika wakati muafaka asilimia 30 pia itafikiwa katika Bunge hili. (*Makofi*)

MHE. BALOZI GETRUDE I. MONGELLA: Mheshimiwa Spika, ninaomba kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa Tanzania imeridhia Mikataba mbalimbali ya Umoja wa Mataifa ikiwemo *Convention of Elimination of Discrimination Against Women*; na kwa kuwa Mheshimiwa Rais wa Tanzania ni mmoja wa Marais walioweka Mkataba wa *SADC* wa kuhakikisha ya kwamba asilimia 30 ya uwakilishi wa wanawake katika nyanja zote na katika jamii zinafikiwa kabla ya mwaka 2010. Hoja ya Mheshimiwa Waziri ya kutokuwa na nafasi ndani ya Bunge ni hoja halali? (*Makofi*)

WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA: Mheshimiwa Spika, nimesema kwa kweli nia ipo ya kuongeza idadi ama asilimia hiyo kufikia asilimia 30 na suala hili tumekwishaafikiana. Lakini tatizo ni ufinyu wa jengo lenyewe. (*Makofi*)

WABUNGE FULANI: Aaa.....!

WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA: Lakini ningependa niseme tu kwamba Mheshimiwa Rais yuko mstari wa mbele kabisa katika kuwatetea akinamama katika masuala mbalimbali siyo ndani ya Bunge hili, lakini pia katika uteuzi wa viongozi wetu mbalimbali na ni mara machache ukakuta kwamba mkeo akakusifia kwamba unafanya kazi nzuri kama mama Mkapa alivyomsifia Mheshimiwa Rais, kwamba yuko mstari wa mbele kabisa kutetea haki za akinamama. Kwa hiyo, naomba tuvute subira. (*Makofi/Kicheko*)

Na. 241

Huduma ya Simu

MHE. JACOB D. SHIBILITI (k.n.y. MHE. ESTHER K. NYAWAZWA) aliuliza:-

Kwa kuwa Tarafa ya Nyamilama, iliyopo katika Wilaya ya Kwimba ipo mbali sana na Makao Makuu ya Wilaya.

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuweka Simu ya Upepo (*Radio Call*) ili iwasaidie wananchi na watendaji kurahisisha mawasiliano na Makao Makuu ya Wilaya yao ya Kwimba?

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Esther Nyawazwa, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kuweka mawasiliano ya uhakika ili iwasaidie wananchi na watendaji kurahisisha mawasiliano kati ya Wilaya ya Kwimba pamoja na Wilaya nyingine zote nchini.

Kampuni ya Simu Tanzania imetayarisha mpango wa uboreshaji wa mawasiliano ya simu vijijini. Chini ya mpango huu vijiji vya Mwankule, Luhala na Nyamilama vinatarajia kupata simu mbili za vibandani kwa kila kijiji. Mpango huu utanza kutekelezwa baada ya wenye hisa katika Kampuni kukubaliana kuhusu nafasi ya Kampuni katika utekelezaji wa sera ya mawasiliano.

MHE. JACOB D. SHIBILITI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa Wilaya Kwimba mpaka sasa hivi haina mawasiliano kabisa, mawasiliano yote ni ya matatizo hususan katika maeneo ya Mwamakonye, Mwakilyabiti, Mwankule na Nyamilama yenyewe ni lini hasa watasaidia tatizo hili kulitatua pamoja na simu za mkononi kupatikana katika eneo hilo? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, nakubaliana kwamba mawasiliano ya Wilaya ya Kwimba kidogo siyo mazuri sana kwa sababu bado Kwimba wanatumia mitambo ya zamani ya simu za kukoroga.

Mheshimiwa Spika, ni nia ya Kampuni ya Simu kuiondoa mitambo ya zamani ya simu za kukoroga na kuweka simu za kisasa. Hivi sasa shughuli zinazofanyika ni kuona *transmission link* kutoka Mwanza kwenda Geita na kwenda Bukoba inaboreshwa ili huduma za mawasiliano ya simu ziwe ni za uhakika. Lakini napenda nimhakikishie pia hata Mwanza sasa hivi yapo mambo ambayo yanafanyika ili kuondoa simu za kukoroga na kuweka simu za kisasa.

Na. 242

Umeme Mji Mdogo wa Laela

MHE. CHRISANT M. MZINDAKAYA aliuliza:-

Kwa kuwa Mji Mdogo wa Laela ni wa tatu kwa ukubwa na wingi wa wakazi baada ya Sumbawanga na Mpanda; na kwa kuwa Makao Makuu ya Mkoa yaliyoko Sumbawanga yatakuwa na umeme wa uhakika kutoka Zambia:

Je, isingekuwa jambo jema kwa mitambo ya umeme ya Dizeli iliyoko Sumbawanga ikahamishiwa Laela?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Chrisant Mzindakaya, Mbunge wa Kwela, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana kabisa na Mheshimiwa Chrisant Mzindakaya, kwamba ingekuwa jambo jema kama mitambo ya dizeli iliyoko Sumbawanga ingehamishiwa Mji mdogo wa Laela kwa wakati huu ambapo Makao Makuu ya Mkoa pale Sumbawanga yamepatiwa umeme wa uhakika kutoka Zambia.

Hata hivyo, kulingana na sera ya Serikali kuhusu usambazaji umeme vijijini ambayo pamoja na kupeleka umeme kwenye Makao Makuu ya Mkoa inasisitiza pia kupeleka umeme kwenye Makao Makuu ya Wilaya na katika Mkoa wa Rukwa, Wilaya moja ya Nkasi bado haijapata umeme na kwa sasa hivi jitahada zetu zinaelekezwa huko ili Wilaya hii iweze kupata umeme. Baada ya mradi huu kukamilika, Serikali itaangalia uwezekano wa kupeleka umeme maeneo mengine kulingana na upatikanaji wa fedha kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge ameulizia juu ya umeme wa Laela. Serikali imekuwa ikiwasiliana na nchi mbalimbali na kupanga pia mipango ya humu ndani ya kuhakikisha kwamba tunapata fedha kwa ajili ya utekelezaji miradi hii ya umeme.

Mheshimiwa Spika, hali ya mitambo ya diseli iliyokuwa ikizalisha umeme mjini Sumbawanga kwa kweli siyo ya kuridhisha na tusingependa kumpa mzigo Mheshimiwa Mbunge na watu wake kupeleka mitambo ambayo imepitwa na wakati na badala ya kusaidia ikawa mitambo hii ni kero kubwa. Kwa hiyo, ni bora kutafuta mitambo mingine mipya na kufuatana na hali ya fedha ambayo nimezungumzia hapo awali.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema awali jitihada zetu kwanza zinaelekezwa katika kuupatia umeme Makao Makuu ya Wilaya ya Nkasi yaani Mji wa Namanyere na hapo tutakapopata uwezo mwingine tutahakikisha kwamba Mji mdogo wa Laela unapatiwa umeme na ili kuupatia umeme Mji huu inabidi kujenga njia ya umeme ya msongo wa kilovolti 33 kutoka Sumbawanga hadi Laela umbali wa kilometa 90 na gharama zake zinakisiwa kuwa shilingi bilioni 1.3.

MHE. CHRISANT M. MZINDAKAYA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba nia ni kupeleka umeme kwanza katika Makao Makuu ya Wilaya zote nchini. Sasa atueleze lini Mji wa Namanyere Makao Makuu ya Wilaya ya Nkasi utapata umeme?

(b) Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwanza ni Makao Makuu ya Wilaya. Sasa nataka kumuuliza swali je, hakuna umeme wowote katika Miji Midogo ambayo siyo Makao Makuu ya Wilaya hapa nchini? *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, kwanza ni lini Mji wa Namanyere utapata umeme? Nilishawahi kusema katika Bunge hili Tukufu katika majibu ya maswali yaliyopita kwamba Serikali iliweka ahadi katika utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi kwamba Miji hii ingepata umeme ifikapo mwaka 2005 kulingana na upatikanaji wa fedha. Kuhusu Mji wa Namanyere programu yake ni baina ya mwaka 2003 hadi 2005 kulingana na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Spika, napenda nichukue nafasi hii niliambie Bunge lako Tukufu kwamba kwa kweli hivi sasa tunaishughulikia Miji yote ile ya Makao Makuu ya Wilaya ambayo bado haijapata umeme katika kutimiza azma hii, na nisingependa nitoe ufafanuzi zaidi kwa sababu ndiyo tupo katika mpango huo wa kutafuta uwezo wa kufikisha umeme kwenye maeneo yale ambayo bado hayajafikishiwa umeme.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili, je, kuna Miji midogo au vitongoji na kadhalika ambavyo vina umeme. Napenda niseme hapa Bungeni kwamba ni kweli kabisa pamoja na kwamba tumesema sera ni kufikisha umeme kwenye Makao Makuu ya Wilaya kwanza. Lakini pia ni sera hiyo hiyo kwamba tunapofikisha umeme kwenye Makao Makuu ya Wilaya kuna vijiji au vituo vingine ambavyo viko njiani vinaweza vikapatiwa umeme.

Kwa hiyo, ni kwamba ipo Miji Midogo ambayo inapatiwa umeme wakati ambapo Makao Makuu ya Wilaya inapatiwa umeme au hata kabla ya Makao Makuu ya Wilaya haijapatiwa umeme, inategemea na hali ilivyo katika eneo lile ambalo usambazaji umeme unashughulikiwa.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, katika sera hii ya nishati ya kusambaza umeme vijijini. Tunatilia maanani maeneo ya uzalishaji ambayo yana viwanda. Kwa mfano, kwenye uchambuzi wa pamba kwa mfano na viwanda vingine. Nitoe mfano hapa sasa hivi tunashughulikia kupeleka umeme katika Wilaya ya Biharamulo, lakini tunaupitisha pia umeme Chato na Chato kule kuna *ginneries* ambapo tunapitisha umeme. Kwa hiyo, sababu hiyo na sababu nyingine ndizo zinafanya kwamba maeneo haya mengine yanapata umeme na wakati huo huo Makao Makuu ya Wilaya zingine zinapata umeme au hazijapata umeme inategemea hali jinsi ilivyo.

Na. 243

Athari za Mvua zilizonyesha Kata ya Ulowa Jimbo la Kahama

MHE. STEPHEN M. KAZI (k.n.y. MHE. RAPHAEL N. MLOLWA) aliluliza:-

Kwa kuwa tarehe 18 Februari, 2003 mvua kubwa ya mawe iliyonyesha kwenye Kata ya Ulowa, Jimboni Kahama ilisababisha hasara ya jumla ya ekari 242.5 za Tumbaku ya wakulima wapatao 122 wa Vyama vya Msingi 6 vya Ngilimba - ekari 108, Mkombozi - ekari 28.5, Kangame - ekari 59.5, Kasela - ekari 20, Kipalapala - ekari 18.5 na Bugela - ekari 8; na kwa kuwa kutokana na athari hizo, ni dhahiri kwamba wakulima hao wamepoteza jumla ya kilo 100,000 za Tumbaku; na kwa kuwa wakulima hao hawatakuwa na uwezo tena wa kulipia madeni yao ya pembejeo ya msimu kwa Makampuni ya *Tanzania Leaf Tobacco Company* na *Dimon* kwa kuwa janga hilo lilikuwa nje ya uwezo wao:

Je, Serikali itawasaidiaje wakulima hao wa Tumbaku wa Ulowa katika janga hilo?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Raphael Mlolwa, Mbunge wa Kahama, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tathmini iliyofanywa na wataalam wa kilimo imeonyesha kwamba ni kweli kwamba Februari 2003, mvua za mawe zilinyesha kwenye Kata ya Ulowa, Jimboni Kahama na kusababisha hasara kwa wakulima wa tumbaku. Baada ya wataalam wa kilimo kubaini tatizo hilo, walitoa ushauri kwa wakulima juu ya namna ya kuhudumia tumbaku iliyoathirika kwa mvua hizo ili iweze kuendelea kustawi na kuota tumbaku bora na nyingi.

Vile vile, wakulima walifundishwa jinsi ya kukausha majani ya tumbaku yaliyoathirika kutokana na mvua hizo ili yafikie madaraja ya juu ya ubora. Hatua hizo zimekuwa na matokeo mazuri. Tayari urejeshaji wa madeni umefikia asilimia 100 kutokana na tumbaku iliyozwa na wakulima hao kati ya tarehe 1 Aprili na tarehe 8 Julai, 2003.

Mheshimiwa Spika, taarifa za Vyama vya Msingi vya Kangene, Mkombozi, Ngilimba, Kipalapala Bugela na Kasela, ambavyo vinahudumia maeneo yaliyoathirika na mvua za mawe, zinaonyesha kuwa vimeuza kilo 554,284 za tumbaku zenye thamani ya shilingi milioni 432.7. Vyama hivyo, tayari vimelipa shilingi milioni 220.2 ambalo ni deni la Vyama hivyo.

Mheshimiwa Spika, aidha, wakulima wana tumbaku inayokadiriwa kufikia kilo 230,716 ambayo inatarajiwa kuwaingiza kiasi cha shilingi milioni 161.5 itakapouzwa. Kutokana na hali iliyopo, ni dhahiri kwamba Wakulima hawahitaji msaada wowote maalum zaidi ya ule uliotolewa na wataalam.

MHE. STEPHEN M. KAZI: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri yaliyotolewa na Naibu Waziri, lakini ukweli amekiri kwamba athari imekuwepo.

Mheshimiwa Spika, lakini nikirudi nyuma nchi yetu ina uzoefu wa kushughulikia matatizo ya majanga kwenye maeneo mbalimbali. Hayo yaliyowapata watu wa Kahama yako nje ya uwezo wao na ni

majanga. Sasa swali kwa nini Serikali kutokana na tabia ya kushughulikia majanga kama tulivyopata huko nyuma ya treni, mafuriko, mabasi isichukue hatua pia kuwasaidia pia hawa watu wa Kahama ambao wameathirika na Wizara ikachangamka kuona kwamba hawa watu wanavuna mara moja kwa mwaka na wamepoteza mazao yao? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA: Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu kwenye swali la msingi. Palifanyika tathmini hawa wataalamu wa kilimo na kwa hivyo walitoa msaada kulingana na athari ile. Kwa hiyo, walifanya kilichotakiwa kufanyika majanga yanapotokea.

Pili, tumeangalia hata jinsi walivyokuwa wanalipa imeonekana dhahiri kuwa hapana maafa kwa sababu watu wamepata kipato kikubwa. Kwanza, walipata daraja zuri la tumbaku halafu wakapata fedha za kutosha na zaidi ya hao wamerejesha mikopo yote kama nilivyoeleza. Hivyo ni dhahiri kuwa janga lilishughulikiwa lilivyotakiwa.

Na. 244

Mkakati wa Kuboresha Kilimo cha Umwagiliaji

MHE. JENISTA J. MHAGAMA aliuliza:-

Kwa kuwa Wizara ya Kilimo na Chakula imejiweka mkakati mahsusi wa kuboresha Kilimo cha Umwagiliaji nchini; na kwa kuwa wananchi walio wengi Mkoani Ruvuma tayari wameshajanzishia kilimo hicho na hasa kwenye mabonde ya mito mikubwa ya Ruvuma na Mngaka:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kushirikiana na wananchi hao wa Ruvuma katika Mpango huo wa kilimo chenye tija?

(b) Je, ni kiasi gani cha fedha kimetengwa kwa ajili ya kuboresha kilimo cha umwagiliaji katika Mkoa wa Ruvuma?

(c) Je, kuna mipango gani mingine shirikishi ya matumizi bora ya mabonde hayo isiyoleta uharibifu wa mazingira bali kilimo endelevu chenye tija?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo na Chakula, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali imeainisha maeneo yanayofaa kwa kilimo cha umwagiliaji maji mashambani na kuyaorodhesha katika mpango kamambe wa Taifa wa Umwagiliaji Maji Mashambani. Aidha, wataalam wa Ofisi za Kanda za Umwagiliaji Maji Mashambani wanashirikiana na wataalam wa Halmashauri za Wilaya katika uandaji wa miradi ambayo itatafutiwa fedha kwa ajili ya utekelezaji. Utaratibu huu tayari umewezesha maandiko ya miradi mbalimbali ikiwemo miradi ya Nakahuga, Namatuhi, Kitanda na Mpitimbi ambayo imeombewa fedha za utekelezaji.

(b) Kwa mwaka wa fedha wa 2003/2004, Skimu ya Liyuni imetengewa shilingi milioni 50. Aidha, miradi ya Nakahuga, Namatuhi, Kitanda na Mpitimbi imeombewa fedha kutoka *Food Aid Counterpart Fund*. Miradi hiyo kwa pamoja itagharimu zaidi ya shilingi milioni 600.

(c) Miradi yote ya Umwagiliaji Maji Mashambani hufanyiwa tathmini ya athari kwa mazingira (*Environmental Impact Assessment*). Tathmini hiyo hufanywa kwa kushirikiana na wadau ili washiriki katika kulinda mazingira miradi inapoanza kutekelezwa.

MHE. JENISTA J. MHAGAMA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa katika Bajeti ya mwaka huu ya Wizara ya Kilimo na Chakula, Serikali kwa kushirikiana na Wizara hiyo imeonyesha wazi kwamba suala hili la kuboresha Kilimo cha Umwagiliaji ambacho ni kilimo chenye tija imepewa kipaumbele kikubwa sana katika nchi yetu ya Tanzania na hata katika Mkoa wa Ruvuma.

Mheshimiwa Spika, swali je, Mheshimiwa Naibu Waziri akishirikiana na Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula wako tayari kufuatana nami kwenda katika Mkoa wa Ruvuma ili kupokea shukrani za pekee kwa niaba ya Serikali kwa kuona umuhimu huo wa Kilimo cha Umwagiliaji?

SPIKA: Kupokea shukrani sio swali linalohitaji majibu. Ameshapokea shukrani. (*Makofi*)

MHE. RAYNALD A. MROPE: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza.

Kwa kuwa Mto Ruvuma unaishia Mkoa wa upande wa Mtwara na kwa kuwa kuna bonde kubwa sana katika upande huu wa Mashariki. Je, Wizara ya Kilimo na Chakula ina *master plan* gani ya kuendeleza bonde hili la Ruvuma katika Mkoa wa Mtwara na bonde la Lukuledi na Matandu hasa hasa ikieleweka kwamba mabonde haya kwa muda mrefu hayajatumika na yanaweza kuzalisha chakula kingi sana kwa nchi hii? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA: Mheshimiwa Spika, Wizara imetambua hilo na kuanzia mwaka jana tuliwaomba Waheshimiwa Wabunge watupelekee mapendekezo yao Wizarani kusudi tunapotengeneza ule mradi kamambe tuweze kuyaaanisha yote. Naamini Mkoa wa Ruvuma, Mtwara na Lindi wamefanya hivyo. Hata hivyo tayari kwa *speech* ya mwaka huu fedha zimetengwa kwa ajili ya Kitele na Mradi mwingine ulio njiani na hilo. Nitaendelea kufanya hivyo kama akitaka ufafanuzi zaidi namkaribisha Mheshimiwa Mbunge Wizarani tushughulikie haya masuala.

MHE. DR. THADEUS M. LUOGA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa Wilaya ya Mbiga ni sehemu ya Mkoa wa Ruvuma na ina mabonde mengi tu katika Kata ya Mtipwili, Lulingo, Lundo, Kitui, Kigonsera, Kitubanjiosi. Je, katika mpango huo mabonde hayo yamewekewa mikakati gani? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA: Mheshimiwa Spika, ni kweli Wilaya ya Mbinga ni sehemu ya Mkoa wa Ruvuma na kwa kutambua hivyo mtaalamu wetu wa Kanda kutoka Mtwara alipokuja kuainisha miradi ya Wilaya Songea nilimwelekeza binafsi aende Wilaya ya Mbinga na Tunduru kusudi akaainishe maeneo hayo. Tayari kuna maeneo yanayovuka hekta 4,500 kutoka Wilaya ya Mbinga yatahusu utekelezaji wa miradi. Ninachoomba tu Mheshimiwa Mbunge, kabla hajaenda Mbinga apitie Wizarani niweze kumwonyesha maeneo hayo kusudi ahamasishe wananchi wawe tayari kushiriki kikamilifu.

Na. 245

Matatizo Makubwa ya Maji Safi na Salama Kwenye Vijiji 25 Kyela

MHE. JOHN L. MWAKIPESILE aliuliza:-

Kwa kuwa Vijiji 25 katika Kata za Ikama, Mwaya, Kajunjumile, Ipinda na Ipande bado vina matatizo makubwa ya kutopata maji safi na salama jambo ambalo linawafanya waishi maisha duni na ya umaskini:-

(a) Je, ule mpango wa Serikali wa kukarabati Mradi wa Maji wa *Kanga Group* ambao kama ungekamilika ungeondoa kero hiyo ya wananchi utaanza lini?

(b) Je, Serikali inaweza kufanya utafiti ili kuona uwezekano wa kutumia maji ya Ziwa Nyasa kama chanzo cha maji safi na salama kwa wananchi wa Kyela?

(c) Je, chanzo cha maji cha *Makwale Group* ambacho kiko Wilayani Kyela, kwenye miteremko ya Milima ya *Livingstone* hakiwezi kupanuliwa ili Kata zote za Tarafa ya Ntebela ziweze kupata maji kwenye chanzo hicho muhimu na cha kuaminika?

WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa John Mwakipesile, Mbunge wa Kyela, naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Vijiji 25 vyenye shida ya maji kwenye Kata 5 zilizotajwa na Mheshimiwa Mbunge vilikusudiwa kupata maji kwenye mradi wa *Kanga Group* kama ungekamilika jinsi ulivyobuniwa hapo awali. Mradi huo ulifanyiwa usanifu mwaka 1973 na kuanza kutekelezwa kati ya mwaka 1975/1979 hadi 1985/1986 ujenzi wake ulipositishwa baada ya mhisani kujitoka. Sasa hivi usanifu wa awali umepitwa na wakati hivyo kunahitajika mapitio mapya kuhusu uwezo wa vyanzo, bomba kuu, matanki na mfumo wa usambazaji wa maji katika mradi mzima.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, lenye sehemu (a), (b), na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mpango wa Serikali wa kukarabati mradi wa maji wa *Kanga Group* utaanza mara baada ya kukamilisha uchunguzi na usanifu upya wa mradi huo ili kubaini mkakati sahihi wa ukarabati wake.

(b) Uchunguzi wa awali umekwisha baina kuwa chanzo cha Ziwa Nyasa ni mojawapo wa vyanzo vya kuweza kuongeza maji kwa wananchi wa Mji wa Kyela. Kwa sasa Serikali inatafuta fedha ili utafiti wa usanifu wa kina ufanyike kwa ajili ya kukitumia chanzo hicho cha maji.

(c) Kwa pamoja vyanzo vitatu (Mwalisi, Lusongo na Matema) vya mradi wa maji wa *Makwale Group* vinaweza kutosheleza mahitaji ya maji kwa Kata zote za Tarafa ya Ntebela. Tatizo lililopo kwa sasa ni kuanza kuathirika kwa vyanzo hivyo kutokana na uharibifu wa mazingira unaofanyika katika miteremko ya Milima ya *Livingstone*. Upanuzi wa chanzo hicho cha *Makwale Group* utafanyika baada ya Serikali kupata fedha kwa ajili ya utafiti na hatimaye upanuzi wenyewe.

Kwa Bajeti ya mwaka huu tutatenga fedha za kutafiti na kusanifu mradi wa *Kanga Group*.
(*Makofi*)

MHE. HALIMENSHI K. R. MAYONGA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali moja la nyongeza.

Tatizo la maji katika nchi nzima bado linaonekana ni kubwa kwa kiwango kikubwa. Hivi Serikali imeweka mikakati ipi ya makusudi inayoweza kuonyesha kwamba tunaweza kuondokana na tatizo hili la maji maeneo mengi tu hasa ya ufugaji hawana maji kwa kipindi kirefu na maeneo mengine huko Kigoma, Rukwa, Lindi hakuna maji ni tatizo lililokuwa kubwa. Sasa je, hili mkakati ni upi wa haraka wa kuweza kuondokana na tatizo hilo, hapo sasa?

SPIKA: Ni swali jipya, lakini kama Waziri una maelezo unaweza kuyatoa.

WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO: Mheshimiwa Spika, kwanza hali ya maji nchini, Serikali imejitahidi sana. kwa sababu upatikanaji wa maji mijini ni asilimia 73 na vijijini ni asilimia 53. Hata hivyo tunafanya kila jitihada kuhakikisha kwamba tunatimiza malengo ya Kimataifa ya kuhakikisha kwamba ifikapo 2015 asilimia kubwa ya wananchi wawe wamepata maji. Kwa sera mpya ya maji tunawashirikisha zaidi wananchi kutumia nguvu zao na wafadhili wanapendezwa pale wanapoona jitihada zetu wenyewe zipo na kwa hiyo wanatuunga mkono.

MHE. EDSON M. HALINGA aliuliza:-

Kwa kuwa maeneo ya uzalishaji wa Kahawa yana uhaba mkubwa wa maji kwani visima vifupi vya Kata za Igamba, Msia, Itaka, Nabinzo na Isansa vinakuwa havina maji wakati wa kuvuna na kusafisha Kahawa jambo linalofanya zao hili kukosa ubora wake, ambao unategemewa katika kuinua kipato cha mkulima na Taifa kwa ujumla:-

(a) Je, ni lini tatizo la maji katika maeneo hayo litashughulikiwa ili kuboresha zao la Kahawa?

(b) Kwa kuwa Kata ya Ndalambo nayo ina shida kubwa ya maji hasa nyakati za kiangazi; Je, Serikali inachukua hatua gani kuhakikisha kwamba maji yanapatikana ili wananchi watazamwe sawa na wananchi wa maeneo mengine katika nchi hii?

WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Edson Halinga, Mbunge wa Mbozi Mashariki, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Kata za Igamba, Msia, Itaka, Nabinzo na Halungu zinaunda Tarafa ya Igamba yenye idadi ya watu 165,061 kulingana na Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2002. Kati ya idadi hiyo watu wanaopata huduma ya maji ni 24,758 ikiwa ni sawa na asilimia 15 ya watu wote na hivyo hali ya upatikanaji wa maji maeneo hayo si ya kuridhisha. Wananchi wanalazimika kutumia visima vya asili ambavyo maji yake si salama na wala hayatoshi kwa matumizi ya nyumbani ama kusafishia Kahawa.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kuliona tatizo la Kata za Igamba, Msia, Itaka, Nabinzo na Isansa, ilishirikiana na wananchi wa Kata hizo na wafadhili wa kuweza kuchimba visima 106, ambapo wafadhili wa *STABEX* walichimba visima 18 kati ya hivyo. Serikali kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi itaendelea kuchangia ujenzi wa miradi ya maji ya gharama nafuu ili kupunguza tatizo la maji kwa matumizi ya majumbani na kusafishia Kahawa katika Kata hizo.

(b) Kata ya Ndalambo ina vijiji sita ambavyo ni Ndalambo, Ipumila, Kakavi, Nyenjele na Nakawale na Ikana. Ni kweli Kata hii pia ina matatizo ya maji kwa sababu ya kutokuwa na vyanzo vya maji vya kuaminika. Jumla ya visima 50 vinahitajika angalau kupunguza tatizo la maji katika Kata ya Ndalambo. Serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi ili kuchimba visima vya maji na ukarabati wa Mradi wa Maji wa Ndalambo na Kakosi ili kupunguza tatizo hilo la maji.

MHE. EDSON M. HALINGA: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri na ninashukuru sana kwa kuwa matatizo anayaelewa vizuri. Je, Serikali itatusaidia vipi kuona kwamba tatizo hili maana magonjwa mengi ya kuenea kwa kukosa maji yanazidi sana katika maeneo haya hasa Ndalambo na sehemu za Itata na Isansa?

Pili, kuna mradi uliokwishaanzishwa na wafadhili wa *Mission KKKT Konde*, Matema ambao kwa niaba ya Wizara Mhandisi wa Mkoa alikubaliana nao na wananchi waliambiwa na wamekwisha gharamia upimaji na kuweka akiba ya fedha za Mfuko wa Maji. Je, atatusaidia vipi katika kuendeleza suala hili maana wananchi wanadhani fedha zao zimetapeliwa kwa kuwa mradi umesimama haujatoa jibu lolote mpaka sasa?

WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO: Mheshimiwa Spika, kwanza mimi nakubaliana nayo kwamba kwa kweli kuna tatizo kubwa sana la maji Mbozi. Lakini kama alivyosema tunafanya kila jitihada kuhakikisha kwamba matatizo hayo tunayatua. Wakati Mheshimiwa Waziri wa Fedha akitoa Bajeti hapa alieleza kwamba nchi yetu imepata heshima ya kukubalika Kimataifa kwa sababu tunalipa mikopo na miradi yetu inatekelezwa kwa wananchi. Kwa hiyo, tunazungumza na wafadhili ili kuangalia uwezekano wa kusaidia tatizo la maji Mbozi.

Mheshimiwa Spika, kwa suala la pili, kwanza niwapongeze sana *KKKT* kwa hatua ambazo wamechukua kushughulikia maji huko Mbozi. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba tutajiunga nao kutatua matatizo ya maji katika Wilaya ya Mbozi. *(Makofi)*

MHE. FATMA SAID ALI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana na mimi napenda kumwuliza Mheshimiwa Waziri swali dogo la nyongeza. Kabla sijamwuliza Mheshimiwa Waziri Edward Lowassa, nilikuwa napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Kamishna wetu mpya Rose Badi Kulijira, ambaye amechaguliwa juzi kwenye *African Union* atashughulikia *Rural Development* na *Agriculture*.

Sasa swali langu la nyongeza je, Mheshimiwa Waziri kwa kuwa maji ni ukombozi kwa wanawake na tumepata Kamishna huyo mpya wa Tanzania kwa Afrika nzima anayeshughulikia Kilimo na Maendeleo Vijijini. Je, atakuwa tayari kushirikiana naye huyu Kamishna ili tuweze wanawake kugomboka katika maji tuendeleze kilimo katika nchi yetu? *(Makofi)*

SPIKA: Ni swali jipya, lakini Waziri kama una majibu endelea kuyatoa.

WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO: Mheshimiwa Spika, kwanza na mimi najiunga naye kumpongeza Rose Badi Kulijira, kwa kuteuliwa kushika nafasi hiyo kwa niaba ya Watanania.

Kama nilivyosema tutashirikiana na kila mtu ambaye yuko tayari kushirikiana na sisi kusaidia matatizo ya maji katika nchi yetu pamoja na huyo Kulijira. *(Makofi)*

Na. 247

Ajali za Barabarani

MHE. DAMAS P. NAKEI aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali bado inaendelea kushuhudia ajali nyingi zikitokea na kusababisha kupotea kwa maisha ya watu na wengine wengi zaidi kubakia vilema kwa kudumu; na kwa kuwa Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali za kukabiliana na hali hiyo ikiwa ni pamoja na kuamuru matumizi ya *Speed Governors*:

(a) Je, Serikali inaridhika vipi na hatua ilizochukua wakati bado tunaona ajali mbaya zikiendelea kutokea na kuongezeka na nyingi zikiwa zinatokana na uzembe na ukaidi wa madreva waendao kwa mwendo wa kasi?

(b) Je, kwa nini Serikali isichukue hatua zaidi kwa kuwashirikisha wananchi na abiria wanaosafiri kwa vyombo hivyo na kuwatakiwa watoe taarifa kwa Askari wa Usalama Barabarani wanapooa madreva wanaendesha magari kwa mwendo wa kasi pamoja na makosa mengine wanayoyafanya wakiwa safarini?

(c) Je, Serikali haioni kwamba sasa umefika wakati wa kupiga marufuku ubebaji wa abiria kwenye matrika *Pick ups* na kwenye malori hasa siku za minada?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Damas Nakei, Mbunge wa Babati Magharibi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali hairidhiki na hali ya kuendelea kutokea kwa ajali mbaya zinazosababisha upotevu wa maisha na mali.

Kutokana na madhara yatokanayo na ajali hizo, Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali kupambana na matukio ya ajali barabarani hasa matumizi ya Sheria ya Usalama Barabarani Na. 30 ya mwaka 1973 ambayo ilibidi irekebishwe na Sheria na. 6 ya mwaka 1996 ili kupambana vilivyo na tatizo hili. Sheria hii inayataka magari yote ya abiria kufunga vidhibiti mwendo. Wapo baadhi ya madreva wenye tabia ya kulegeza au kunyofoa vidhibiti mwendo ili waendeshe magari kwa kasi. Huu ni uvunjaji

wa sheria na mara kwa mara askari wa usalama barabarani huendesha misako ya kuwakamata madreva hao.

Mheshimiwa Spika, wote wanaokamatwa kwa kulegeza vidhibiti mwendo hufikishwa Mahakamani na hupewa adhabu kulingana na sheria. Serikali itaendelea kuwakamata wale wote wanaokiuka sheria hii.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikiwahamasisha na kuwaelimisha wananchi kwa njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuwepo kwa vipindi vya redio juu ya umuhimu wa kutoa taarifa Polisi wanapooona madreva wanaohatarisha maisha ya abiria kwa kwenda mwendo wa kasi. Lakini hadi sasa hatujapata ushirikiano wa kutosha kuhusu suala hili. Wakati mwingine baadhi ya abiria wanapenda gari iendayo kasi, hivyo huwachochea madreva waende kwa kasi kubwa.

Mheshimiwa Spika, katika hali hii ninawaomba Waheshimiwa Wabunge tushirikiane katika kazi ya uelimishaji wa wananchi ili wasaidiwe Polisi kwa kutoa taarifa dhidi ya madreva wanaohatarisha maisha ya abiria.

(c) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa sehemu mbalimbali hasa minadani mara nyingi matrekta, malori na *pick-ups* hutumika kubeba abiria. Usafirishaji wa abiria, katika vyombo hivyo husababisha ajali nyingi na kubwa. Serikali kwa muda mrefu inalitambua tatizo hili na ndiyo maana malori, matrekta na *pick-ups* hazipewi leseni za kubeba abiria na pia wanaopata ajali katika vyombo hivyo sheria haiwapi malipo ya fidia kutoka katika Mashirika ya Bima.

Mheshimiwa Spika, pamoja na sheria inayokataza ubebaji wa abiria kwenye malori. Miaka machache iliyopita baadhi ya wananchi na hata Wabunge waliomba uwezekano wa Serikali kuwasaidia wananchi wanaokaa pembezoni na ambao hawana usafiri wa Mabasi waruhusiwe kutumia *pick ups* na malori. Kutokana na kukosekana kwa Mabasi, watu wengi hasa vijijini hivi sasa wanatumia malori na matrekta kusafiria. Huu ni uvunjaji wa sheria, lakini kwa kutambua tatizo lao, Serikali imekuwa haiwakamati na kuwapeleka Mahakamani. Ushauri wa Mheshimiwa Mbunge kwamba sasa Serikali ianze kuwakamata wale wote wanaosafiri katika malori na *pick ups* ni sawa kabisa kisheria na tutauzingatia. Hata hivyo, ili wananchi vijijini wasiumie kwa kukosa usafiri, tunaomba Waheshimiwa Wabunge tuendeleo kuhamasisha wenye Mabasi wayapeleke hadi vijijini.

MHE. SEMINDU K. PAWA: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa swali linataja *Speed Governor*. Hivi tuna kiwanda cha *Speed Governor* nchini kwa hivyo taarifa nilizonazo kwamba wanaweza wakashirikiana na *Customs importation* ya *Speed Governor* katika muda wa miaka miwili ni chache kuliko mabasi ambayo yanaendeshwa nchini. Unaweza ukafuatilia hilo? (Makofi)

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, hatuna taarifa kwamba hapa nchini kuna upungufu wa *Speed Governors*. Tatizo si upungufu wa *Speed Governors*, tatizo ni watu kulegeza, wananunua wanaweka katika mabasi na wanalegeza. Hili ndilo tatizo kubwa na ndilo tunalopambana nalo na tutaendelea kupambana na wale wote wanaolegeza *Speed Governors*.

Na. 248

Wizi wa Mali na Mauaji Yanayotokana na Uvamizi wa Wanajeshi wa Burundi

MHE. KILONTSI M. MPOROGOMYI (k.n.y. MHE. BEATUS R. MAGAYANE) aliuliza:-

Kwa kuwa mara nyingi Serikali imekuwa inakubali kuwa wananchi waishio Mpakani na Burundi hasa katika Wilaya ya Kasulu na Kibondo wamekuwa wakipata hasara ya kuibiwa mali zao na hata kusababisha mauaji yanayotokana na wanajeshi wa Burundi kuyavamia maeneo yao kwa kisingizio cha kufuatilia waasi; na kwa kuwa Serikali imesema kuwa inaandaa taratibu za fidia kwa kufuata sheria za Kimataifa hasa pale nchi ya Burundi itakapokuwa na Serikali kamili na siyo hii ya Mpito:-

(a) Je, ni matukio mangapi ambayo Serikali tayari imeandaa na yenye vielelezo vya kutosha kuyatolea taarifa kwa Umoja wa Mataifa kwa lengo la kudai fidia kutoka kwa Serikali ya Burundi?

(b) Kwa kuwa Serikali yetu inawajali sana wananchi wake; Je, isingekuwa busara kuwalipa kifuta machozi waathirika wa matukio hayo wakati wakisubiri malipo kamili toka Serikali ya Burundi?

(c) Je, Serikali kwa kushirikiana na Jumuiya za Kimataifa kwa nini isiunde Tume Huru ya kuchunguza na kuihakikishia Burundi kuwa hakuna waasi wanaotokea Tanzania kwenda kuipiga Burundi, ili pindi Burundi itakapoingia Tanzania kwa kisingizio hicho basi iwe ni uthibitisho wa uchokozi na hivyo ishughulikiwe ipasavyo?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Beatus Magayane, Mbunge wa Buyungu, napenda kutoa maelezo yafuatayo ya utangulizi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mapigano ya wenyewe kwa wenyewe nchini Burundi, Watanzania waishio Mpakani na Burundi wamepata athari mbalimbali kama wizi, kujeruhiwa na hata kupoteza maisha. Uvamizi huu umekuwa unafanywa na pande mbili zinazohusika na mapigano hayo, yaani askari wa Jeshi la Burundi na askari waasi.

Kutokana na athari wanazozipata raia wetu, Wizara yangu imetafuta ushauri wa kisheria kutoka kwa wataalam wa sheria za Kimataifa na Diplomasia wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa lengo la kuandaa madai ya fidia kutoka Serikali ya Burundi. Ushauri uliotolewa na wataalamu hao unaonyesha kwamba fidia kama hiyo hutolewa pale tu ambapo nchi zinapokuwa vitani; baada ya vita, nchi iliyoanzisha vita hutakiwa kulipa fidia kwa athari na hasara iliyotokana na vita hiyo (*War Reparations*).

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Beatus Magayane, Mbunge wa Buyungu, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba yamekuwepo matukio kadhaa kwenye mpaka kati yetu na Burundi ambayo yamesababisha wizi wa mali na mauaji yanayotokana na uvamizi wa wanajeshi wa Burundi na askari waasi wa Burundi. Orodha ya matukio hayo ipo lakini haitapelekwa Umoja wa Mataifa au kwenye Mahakama Kuu ya Kimataifa kwa lengo la kudai fidia. Serikali yetu haitarajii kudai fidia Serikali ya Burundi kwani Sheria za Kimataifa zinaelekeza kuwa fidia ya aina hiyo inaweza kudaiwa pale ambapo nchi zinapokuwa vitani, na sio vinginevyo.

(b) Mheshimiwa Spika, ni kweli pia kwamba Serikali yetu inawajali sana wananchi wake, lakini Serikali kwa hivi sasa haina uwezo wa kuwalipa waathirika wa mapigano ya vikundi vya mbalimbali nchini Burundi. Aidha, Serikali yetu haisubiri kupata malipo yoyote ya fidia kutoka Serikali ya Burundi kwa sababu ile ile iliyotolewa awali.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali ya Tanzania inajua, Jumuiya ya Kimataifa inajua na Burundi yenyewe inajua, kwamba Tanzania haiwahifadhi waasi wa Burundi kwa ajili ya kuendeleza vita vya wenyewe kwa wenyewe nchini Burundi. Aidha, uhusiano wetu na Burundi ni mzuri na utaboreshwa zaidi kutokana na hatua ya Tanzania kufungua Ofisi ya Ubalozzi nchini Burundi hivi karibuni.

Katika mazingira haya, Mheshimiwa Mbunge atakubaliana nami kuwa hakuna haja ya kuundwa kwa Tume Huru ya Kimataifa kuchunguza madai kuwa Tanzania inahifadhi waasi wa Burundi.

Mheshimiwa Spika, napenda kumalizia kwamba, japokuwa kisheria hatuna hoja ya kudai fidia Serikali ya Burundi, bado tuna nia ya kufanya mazungumzo ya kindugu na Serikali ya Burundi hapo hali ya mapigano itakapotulia ili kuona uwezekano wa kuwalipa kifuta machozi waathirika wa mapigano yao kwenye mpaka wetu.

MHE. KILONTSI M. MPOROGOMYI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa jibu la sasa hivi la Mheshimiwa Waziri, je, watu wetu waendele kuuawa tu?

Lakini swali la pili halikuuliza tatizo la mahusiano yetu na Burundi. Lakini je, Mheshimiwa Waziri anakubali kwamba kukosekana kwa usalama Mpakani mwa Tanzania na Burundi kwa sababu ya matukio mengi ambayo yamekuwepo kunawafanya wananchi wawe na wasi wasi kwamba usalama wa maisha yao sasa uko hatarini kwa majibu aliyetoa. Ahsante Mheshimiwa Spika. *(Makofi)*

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, tatizo letu ni kwamba hatuna uhuru au uwezo wa kuchagua jirani na tumejikuta tuna majirani tulionao, wengine tuko nao vizuri na wengine ndio tuko katika hali hiyo ambayo tuko nayo hivi sasa hivi.

Alivyojibu Mheshimiwa Naibu Waziri ni sahihi kabisa kwamba kwa mujibu wa Mikataba ya Kimataifa ni mpaka nchi ziwe ndani ya vita na ndio maana tulikuwa na matatizo hayo hayo katika mpaka wetu na Mozambique wakati wenzetu wakipigania Uhuru. Waliathirika raia wetu wengi Mpakani kule, lakini wenzetu walipopata Uhuru tulifarijika na Uhuru wao na usalama ambao tunaendelea kupata katika mpaka ule. Kwa hiyo, ni matumaini yetu vile vile kwamba na Burundi watamaliza matatizo yao na ndio maana Serikali yetu iko mstari wa mbele kuhakikisha kwamba chanzo cha matatizo ya Burundi kinapatiwa majibu na chanzo ni kuhakikisha kwamba wenyewe wanaelewana na wanaendesha shughuli zao kwa usalama.

Kwa hiyo, sio kweli kwamba tutarajie tu au ni mategemeo yetu au ndio tunavyoomba kwamba wananchi wetu waendeleo kuteseka tu, lakini jitihada tunazozifanya za kuhakikisha usalama wa kudumu Burundi ndizo ambazo zitatuotea majibu ya kudumu. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana, Waheshimiwa Wabunge muda wa maswali umekwisha na maswali pia yamemalizika. Kuna tangazo moja kutoka kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Wabunge wote, Mheshimiwa Waziri Mkuu anaomba niwatangazie kwamba tutakapitisha shughuli za Bunge hapo saa 7.00 mchana, Waheshimiwa Wabunge wote wabaki humu ndani kwa jambo fupi la dakika kumi au kumi na tano hivi, anataka kutueleza. Kamati ya Wabunge wote wa CCM baada ya kusitisha shughuli...*(Kicheko/Makofi)*

Samahani, Kamati ya Wabunge wote wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Kicheko/Makofi)*

Mwisho wa matangazo. Katibu endelea na *Order Paper*.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2003/2004 Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu

WAZIRI WA SAYANSI, TEKNOLOJIA NA ELIMU YA JUU: Mheshimiwa Spika, awali ya yote kabla sijasoma hotuba yangu nawaomba Waheshimiwa Wabunge mkaangalie katika *pigeon holes* zenu, nimeweka kitabu cha takwimu. Ahsante.

Mheshimiwa Spika, kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati inayohusu Wizara yangu, naomba kutoa hoja kwamba Bunge sasa likubali na kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu na Taasisi zake kwa mwaka wa fedha 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, aidha, niruhusu pia niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu katika kuwapongeza Wabunge 19 wapya ambao nimewaandikia waliochaguliwa na kuapishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukurani za dhati kwa wale wote waliotuwezesha kutekeleza majukumu ya Wizara yetu kwa kipindi kilichopita na ambao wametuwezesha kupanga mipango ya mwaka 2003/2004 na kuboresha hoja zetu ambazo tunaziwasilisha katika hotuba hii.

Aidha, natoa shukurani kwa wananchi wote wa Tanzania. Pia shukurani zimwendee Naibu Waziri wangu, Mheshimiwa Zabein Muhaji Mhita, Katibu Mkuu, Bibi Ruth H. Mollel, watumishi wa Wizara yangu pamoja na Taasisi na Mashirika mbalimbali ya ndani na nje kwa misaada na ushauri wao, bila kumsahau Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi, Mbunge wa Kyerwa (*TLP*) na Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani katika Wizara yangu kwa ushirikiano wake na mchango wake katika kuiboresha hoja hii.

Aidha, shukurani zangu ziwaendee Waheshimiwa Wabunge wa Kamati ya Huduma za Jamii chini ya Mwenyekiti wao Mheshimiwa Omar Kwaangw', Mbunge wa Babati Mashariki (CCM) kwa uchambuzi na ushauri wao. (*Makofi*)

Mwisho, napenda kuwashukuru wananchi wa Jimbo langu la Maswa, kwa uvumilivu, uelewa, ushauri na kwa kura zao ambazo zimeniwezesha kuwa Bungeni kwa mfululizo wa vipindi vitano. Ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba yangu mwaka wa fedha 2002/2003 nililiarifu Bunge lako Tukufu kuwa Wizara yangu ilikuwa imekamilisha maandalizi ya Mpango Kamambe (*Master Plan*) utakaongoza ukuaji wa Sekta za Sayansi na Teknolojia, Elimu ya Juu na Ufundi. Aidha, nililiarifu Bunge lako Tukufu pia kuwa utafiti kuhusu gharama ya kumwelimisha mwanafunzi katika elimu ya juu na ufundi ilikuwa imekamilika. Nafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa mipango hii sasa imezinduliwa rasmi na kuanza kutumika.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inaendelea na zoezi la uhuishaji wa Vyuo. Katika mwaka wa fedha 2002/2003, Wizara yangu imekamilisha ukusanyaji wa taarifa muhimu zinazohusu raslimali ya Vyuo vilivyopo vya Sekta mbalimbali. Aidha, zoezi hili limefanikisha kukusanya taarifa muhimu zinazohusu hali ya Vyuo husika, umuhimu na ufanisi wa namna elimu inavyotolewa. Pia zoezi hili limefanya uchambuzi unaohusu mahusiano kati ya elimu, kwa upande mmoja na soko la ajira na ukuaji wa uchumi kwa ujumla. Kwa upande mwingine, kukamilika kwa zoezi hili kutaimarisha matumizi ya raslimali zilizo kwa kupanua Elimu ya Juu na Ufundi na kutoa matokeo yanayokidhi haja ya soko la ajira.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2002/2003 Wizara yangu ilitekeleza yafuatayo:-
Kwanza, kukamilisha maandalizi ya rasimu ya Muswada wa Sheria ya Elimu ya Juu, pili, kukamilisha maandalizi ya rasimu ya Waraka wa Kuridhia Itifaki ya uanzishwaji wa Baraza la Vyuo Vikuu vya Afrika Mashariki, tatu, kukamilisha maandalizi ya Sheria ya kuanzishwa rasmi kwa chombo cha utoaji na urejeshwaji wa mikopo ya kuchangia gharama za kusomeshea wanafunzi Vyuo vya Elimu ya Juu nchini na mwisho, kuimarisha Mfuko wa Elimu kwa kufanya uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko huo.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2002/2003 Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kimetekeleza yafuatayo:-

Kwanza, kimepunguza ada ili kuwezesha wanafunzi wengi kujiunga na Chuo kwa kujigharamia. Aidha, hivi sasa gharama hizi zitakuwa kati ya Shilingi laki sita hadi milioni moja kwa mwaka kwa kozi za shahada ya kwanza, pili, kimetafuta wadhamini mbalimbali wa ndani na nje ambao wanaweza kusaidia kugharamia masomo ya wanafunzi kama vile Sida – SAREC, NORAD na *Carnegie Foundation* na tatu, kuendelea na mpango wake wa mageuzi unaoitwa *Institution Transformation*.

Mheshimiwa Spika, kuhusu udahili wa wanafunzi, hivi karibuni kumekuwepo mtazamo potofu kwamba Serikali inashindwa kugharamia wanafunzi wenye sifa za kujiunga na Elimu ya Juu. Kupitia Bunge lako Tukufu naomba nitoe ufafanuzi ufuatao:-

Mheshimiwa Spika, kuna tofauti ya kimsingi kati ya udahili na udhamini, Vyuo vina mamlaka ya kudahili idadi yoyote ya wanafunzi kadri ya uwezo wao. Serikali inadhamini sehemu tu ya wanafunzi waliodahiliwa kulingana na Bajeti na sehemu iliyobakia ya wanafunzi waliodahiliwa inapaswa kudhaminiwa na wadau wengine.

Mheshimiwa Spika, mwaka wa fedha 2002/2003, Chuo Kikuu kishiriki cha Ardhi na Usanifu Majengo kimetekeleza yafuatayo:-

Kwanza, kimeongeza idadi ya wanafunzi toka 786 hadi 863 kati yao wanaume ni 739 na wanawake 124, sawa na asilimia 14 ya wanafunzi wote, pili, kimeanzisha masomo ya Stashahada ya Uzamili kukiwa na wanafunzi tisa wa Stashahada na kumi wa Shahada ya Uzamili katika fani ya Mipango Miji na Uendeshaji na tatu, kimefikisha idadi ya walimu wa Shahada ya falsafa 27 toka watatu wale Kilianza nao mwaka 1996.

Mheshimiwa Spika, Chuo Kikuu Kishiriki cha Sayansi za Afya Muhimbili kimetekeleza yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, kimefanya ukarabati na upanuzi wa jengo la Kitivo cha Tiba ya Meno. Kutokana na upanuzi huo yafuatayo yamekamilika:-

Mheshimiwa Spika, kitivo hicho kimekamilisha vyumba vya matibabu 13, vyumba vya kufanyia maonyesho (*Demonstration Rooms*) vitatu, madarasa 13 na ofisi kumi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2002/2003, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kimetekeleza yafuatayo:-

Kwanza, kimeongeza idadi ya wanafunzi toka 10,897 mwaka 2002 hadi wanafunzi 13,357 mwaka 2003, asilimia 19 ya wanafunzi hao ni wanawake, pili, kimeanzisha Kitivo cha Biashara na Kurugenzi ya Utafiti na Masomo ya Uzamili na tatu, kimeongeza machapisho ya kufundishia na kujifunzia toka machapisho 112 mwaka 2002 hadi machapisho 118 mwaka 2003.

Mheshimiwa Spika, Chuo Kikuu Mzumbe kilizinduliwa rasmi na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, mnamo tarehe 13 Desemba, 2002 na kimetekeleza yafuatayo:-

Kimeanzisha kozi za Shahada za Uzamili na Udaktari wa falsafa mbili zenye washiriki 165, kimeendelea na upanuzi wa Maktaba ili iweze kutumiwa na wanachuo 500 kwa wakati mmoja, kimeweka mtandao wa kompyuta wa *Local Area Network* na hivyo kuanzisha matumizi ya kompyuta katika kuweka kumbukumbu za Chuo katika nyanja za Uhasibu, Utawala na Kumbukumbu za wanachuo, kimewawezesha Walimu wapya tisa kupata nafasi ya kusomea Udaktari wa Falsafa na kimeongeza usajili wa wanachuo wa kike kutoka asilimia 33 ya sasa hadi kufikia asilimia 40.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2002/2003 Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kimetekeleza yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, kimeongeza idadi ya wanafunzi wa Shahada ya kwanza kutoka 2,051 mwaka 2001/2002 hadi 2,246 mwaka 2002/2003. Kati ya hao wanafunzi wa kike ni 674, pili, kimeendelea na utafiti katika maeneo yafuatayo:-

(i) Uzalishaji wa mboga na matunda unaotekelezwa na Idara ya Mimea Vipando. Jumla ya Wakulima 1,597 wamenufaika na mradi huo katika Vijiji vinne Morogoro Vijijini.

(ii) Kilimo cha Mseto (*Agro-forestry*). Mradi huu unahusu upandaji miti bora na inayofaa kwa matumizi ya malisho, kuni kurutubisha na kuhifadhi ardhi. Jumla ya wakulima 175 wanashiriki na kunufaika na mradi huu.

(iii) Ufugaji wa mbuzi chotara katika kuzalisha maziwa na nyama. Mradi huu unafadhiliwa na Shirika la *DANIDA*. Jumla ya wafugaji 200 wanashiriki na kunufaika na mradi huu katika Mikoa ya Mtwara, Kigoma na Dodoma.

(iv) Utafiti wa kilimo kwa wakulima wadogo wadogo Tanzania (*Tanzania Agricultural Research Project – TARP II*). Mradi huu unafadhiliwa na Serikali ya Norway kupitia Shirika la *NORAD* na kusimamiwa na Wizara ya Kilimo na Chakula kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo.

Lengo kuu la mradi huu ni kuimarisha uhakika wa chakula na pato la kaya la wakulima wadogo wadogo na hasa wanawake.

Mheshimiwa Spika, pia, kutoa mafunzo kwa wakulima, walimu wa Vyuo vya Kilimo, wafanyakazi wanaotoa ushauri wa kilimo, misitu na ufugaji bora, Maafisa Mipango, Mameneja, Watafiti na wengineo na kimeanzisha huduma ya *Television* ambayo Taasisi ya Elimu ya Kujiendeleza huitumia kuelimisha wakulima, matokeo ya utafiti kwa wananchi. Kwa kuanzia, huduma hii inanufaisha maeneo ya Manispaa ya Morogoro na Vitongoji vyake.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2002/2003 Baraza la Ithibati la Elimu ya Juu lilitekeleza yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, kutoa Hati za Mamlaka ya kuanzisha Vyuo vitatu vitarajiwa kutoa Hati ya Usajili wa muda kwa Vyuo vitano, kusitisha kwa muda usajili kamili wa Chuo kimoja, kutayarisha mwongozo wa viwango vya majengo, vifaa na miundombinu vinavyopaswa kutumika katika Vyuo vya Elimu ya Juu, kukamilisha mwongozo wa kusaidia Vyuo ili kuhakiki ubora wa elimu itolewayo na kuratibu ubora wa programu za masomo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2002/2003 Mamlaka ya Elimu Tanzania imepata Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Elimu Tanzania kuanzia tarehe Mosi Machi, 2003 na imetekeleza yafuatayo:-

Kwanza, kukamilisha taratibu, miongozo, vigezo vya matumizi ya fedha za Mfuko wa Elimu, kuwasiliana na Uongozi wa Mfuko wa Elimu ya Juu Zanzibar kuhusu utaratibu na makubaliano ya matumizi na uchangiaji wa fedha za Mfuko kwa ajili ya Elimu ya Juu Tanzania Visiwani, kutoa ruzuku ya shilingi 1,500,00,000/= kwa Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu ili zitumike kugharamia wanafunzi 603 waliokosa udhamini katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam katika mwaka wa masomo 2002/2003 na imeanzisha uhamasishaji wa kutoa elimu kwa wadau na wananchi juu ya mamlaka na Mfuko wa Elimu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2002/2003 Wizara imefanya yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika Wizara imekarabati majengo, mitambo na vifaa mbalimbali katika vyuo vya Ufundi Arusha na Mbeya, imegharamia Mafunzo ya Uzalishaji wa Walimu 12 kwa ngazi za Udaktari wa Falsafa, Shahada ya Uzamili na Diploma ya Uzamili na Stashahada ya Juu ya Uhandisi ikilinganishwa na walimu 15 kwa mwaka 2001/2002 ambapo Udaktari wa Falsafa walikuwa watatu, Shahada ya Uzamili sita, Diploma ya Uzamili nne na Stashahada ya Juu ya Uhandisi mbili, imewawezesha wasichana kumi kati ya 16 kujiunga na Mafunzo ya Elimu ya Ufundi baada ya kuhudhuria kozi maalum ya wiki kumi kuinua uwezo wao kitaaluma ambayo yalifanyika Vyuo vya Ufundi Mbeya na Arusha na imeanzisha mafunzo ya miaka mitatu ya kozi ya Stashahada ya Juu ya Uhandisi (ADE) katika Chuo cha Ufundi Mbeya, kuanzia mwezi Oktoba, 2002 kwa kudahili wanafunzi 35 katika fani ya Ujenzi na Mitambo.

Pia kununua mashine na mitambo yenye thamani ya shilingi milioni 150 kwa ajili ya Chuo cha Ufundi Mbeya ili kuimarisha ufundishaji wa Stashahada ya juu ya Uhandisi. Aidha, imenunua vitabu vya kiada na rejea vyenye thamani ya Shilingi milioni 81.5, kuandaa mpango kabambe (*Master Plan*) wa kubadili Chuo cha Ufundi Mbeya kuwa Taasisi ya Sayansi na Teknolojia, kuajiri walimu 12 wa Uhandisi na Sayansi wenye kiwango cha Elimu ya Shahada ya Kwanza, wanane na wanne Shahada ya Uzamili kwa ajili ya kuimarisha Elimu ya Ufundi katika Vyuo vya Ufundi Mbeya na Arusha na kugharamia mafunzo maalum ya Ualimu kwa walimu Wahandisi 20 walijajiriwa hivi karibuni katika Vyuo vya Ufundi vya Arusha na Mbeya na Makao Makuu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2002/2003 Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam imetekeleza yafuatayo:-

Kuanzisha kitengo cha jinsia ili kushughulikia uhamasishaji wa wasichana kujiunga na Elimu ya Ufundi, kugharamia mafunzo ya Uzamili kwa Walimu 26 ndani na nje ya nchi; Udaktari wa Falasafa 13,

Shahada ya Uzamili nane na Diploma ya Uzamili watano. Aidha, walimu watatu wamepata mafunzo ya Shahada ya Kwanza na wawili Stashahada ya Juu ya Uhandisi. Mmoja kati ya walimu hao ni mwanamke ambaye anasoma *Ph.D*, kuendelea kuratibu mpango wa kujenga utamaduni wa ukarabati (*Culture of Maintenance and Maintenance Network*), kuanzisha Kituo cha Mafunzo ya Mawasiliano ya Redio (*Amateur Radio Station*) kinachujulikana kama *DIT Radio Amateur Station* kwa ajili ya mawasiliano ya kitaaluma, kukarabati mabweni, maabara, meko ya umeme na mtandao wa maji kwa kutumia jumla ya shilingi milioni 170 zilizotokana na shughuli za uzalishaji mali za Taasisi na kuanzisha utaratibu wa mafunzo ya *computer network* chini ya *Cisco Academy* kwa ushirikiano wa Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (*UNDP*) na Tume ya Mawasiliano ya Tanzania (*TCC*).

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2002/2003, Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi limetekeleza yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Baraza limekamilisha miongozo, kanuni na taratibu za utayarishaji, ukuzaji na uidhinishaji wa mitaala ya elimu na mafunzo ya Ufundi inayozingatia umahiri yaani *competence based curriculum* kwa maeneo matano ya elimu na mafunzo ya Ufundi, limesajili Vyuo 60 na kati ya hivyo 41 vimepewa usajili kamili na 19 vimepewa usajili wa muda. Aidha, Vyuo vitano vimefungiwa kudahili wanafunzi na kuanzisha programu mpya za mafunzo mpaka hapo Baraza litakaporidhika na uwezo wa Vyuo hivyo kuendesha mafunzo hayo, limetoa ithibati ya muda yaani *Provisional Accreditation* kwa Vyuo viwili ambavyo ni *Dar es Salaam Institute of Technology (DIT)* na *Dar es Salaam Maritime Institute (DMI)*. Aidha, Baraza limepokea maombi ya Vyuo vinne kwa ajili ya kupata ithibati na kuajiri watumishi 18 ili kuimarisha utendaji kazi wa Baraza katika maeneo ya Afya na Sayansi za Tiba, Biashara na Menejimenti, Kilimo, Maliasili na Mazingira, Uhandisi na Sayansi nyingine, Ustawi wa Jamii na Mipango na kuanzisha tovuti ya Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi www.nacte-tz.org.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2002/2003, Wizara yangu imetekeleza yafuatayo:-

Kwanza, imeandaa mapendekezo ya nyaraka mbalimbali za Baraza la Mawaziri na kuziwasilisha katika ngazi husika kwa lengo la kukuza na kusimamia matumizi salama na ya amani ya nishati ya nyuklia. Nyaraka hizo ni pamoja na Tanzania kuridhia Mkataba unaohusu misaada ya kushughulikia ajali ya nyuklia au dharura ya ki-rediolojia, Tanzania kuridhia Mkataba unaokusudia kutumia nishati ya nyuklia kwa shughuli za amani na sio katika utengenezaji wa silaha za nyuklia (*Safeguards Agreement*), Tanzania kuruhusu ujenzi wa Kituo cha Kimatiafa cha Kupima na Kufuatilia Viwango vya Mionzi Ayonisha katika Mazingira chini ya Tume ya Kimataifa ya Udhhibiti wa Majaribio ya Silaha za Nyuklia, Tanzania kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa kuzuia majaribio ya silaha za nyuklia (*Comprehensive Test Ban Treaty*) na Tanzania kuridhia Mkataba unaohusu azma ya kutokuendeleza utengenezaji na matumizi ya silaha za nyuklia (*Non-Proliferation of Nuclear Weapon Treaty – NPT*).

Pia, kutoa tuzo ya Mheshimiwa Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu kwa wasichana watano walioongoza katika nafasi tatu za mwanzo katika masomo ya sayansi ya msingi (Hisabati, Kemia, Fizikia na Baiolojia) katika mitihani ya kumaliza Kidato cha Sita mwezi Mei, mwaka 2002 na wasichana saba waliofanya vizuri katika mitihani ya kumaliza Kidato cha nne mwezi Novemba mwaka 2002 kwa lengo la kuwahamasisha wasichana wengi waweze kujiunga na masomo ya sayansi. Tuzo hiyo pia imetolewa kwa Shule na walimu wa masomo husika.

Mheshimiwa Spika, pia kuwasilisha Muswada wa Sheria wa kufutwa kwa Sheria Na.5 ya mwaka 1983 ya kinga ya mionzi na kutunga sheria mpya ya Tume ya Nguvu za Atomiki nchini, kuandaa rasimu ya Sera ya Baiteknolojia yenye lengo la kukuza na kusimamia matumizi ya teknolojia ya Baiteknolojia, kushiriki katika kuandaa itifaki kitakayounda Baraza la Sayansi na Teknolojia la Afrika Mashariki (*The East African Science and Technology Council (EASTEKO)*) kwa lengo la kusimamia maendeleo ya Sayansi na Teknolojia kwa nchi zilizo Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, kuendelea kuwahamasisha wananchi kupitia Redio Tanzania juu ya matumizi ya sayansi na teknolojia katika kujiletea maendeleo yao. Vipindi vingi vililenga matumizi ya teknolojia na gesi ya samadi na majiko banifu.

Aidha, Waheshimiwa Wabunge na wananchi walielimishwa juu ya matumizi salama na ya amani ya nguvu za atomiki katika kuleta maendeleo ya haraka ikiwa ni pamoja na uzalishaji umeme wa gharama

nafuu na kuhusu tahadhari za kuchukua ili kujikinga na madhara yatokanayo na vyanzo vya mionzi. Pia kuandaa rasimu ya mwongozo wa kuwapa motisha wananchi wenye vipaji maalum vya ubunifu na uvumbuzi kwa lengo la kuendeleza vipaji hivyo, kugharamia ujenzi wa tembe bora za maonyesho katika Vijiji vinne (Chitanda, Mkongo, Muungano/Zomba na Nambecha), Mkoani Ruvuma kwa lengo la kusambaza teknolojia muafaka kwa wananchi kwa kushirikiana na Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda nchini (*TIRDO*). Teknolojia hiyo itasaidia kwa kiasi kikubwa kuongeza ubora wa tumbaku inayokaushwa, kupunguza madhara kiafya kwa wakulima hao na kupunguza ukataji miti, kuandaa rasimu ya mwongozo wa uanzishwaji wa Vituo vya Sayansi na Teknolojia kwa lengo la kurahisisha usambazaji wa metokeo ya utafiti na teknolojia mbalimbali hapa nchini na kukamilisha hadidu za rejea za kuandaa sera ya utafiti zitakazowezesha asasi za utafiti na maendeleo kufanya utafiti unaolingana na mahitaji ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2002/2003, Tume ya Sayansi na Teknolojia ilitekeleza kusambaza matokeo ya utafiti kwa wananchi hapa nchini kwa kushirikiana na Taasisi mbalimbali za utafiti. Matokeo hayo ni kama Teknolojia ya meko Sanifu yanayotumia makaa ya mawe ili kulinda mazingira na Kilimo cha uyoga.

Pia Wizara iliendelea na upanuzi wa mradi wa kutumia *ICT* kwa Utawala Bora katika Halmashauri ya Wilaya ya Kinondoni, Halmashauri ya Manispaa ya Zanzibar, Kijiji cha Lugoba (Bagamoyo) ambacho kimeunganishwa katika *internet* kwa kutumia *V-SAT*. Wizara imeshatoa umeme, nishati ya upepo na teknolojia ya *Biogas*, kugharamia mafunzo ya teknolojia ya mawasiliano ya habari kwa washiriki 180. Washiriki hao walitoka katika Wilaya ya Kinondoni, Halmashauri ya Manispaa ya Zanzibar, Mji wa Kasulu (Mkoa wa Kigoma) na maeneo mbalimbali ya Jiji la Dar es Salaam), kutoa utaalamu wa kuanzisha mtandao wa ndani (*Local Area Network – LAN*) katika Idara ya Mambo ya Kale na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo iliyoko Mikocheni (*Mikocheni Agricultural Research Institute*), kuanzisha Vituo vya teknolojia ya habari na mawasiliano katika Mji wa Kasulu Mkoani Kigoma ili kuiwezesha jamii kupata taarifa mbalimbali za ulimwengu, kufanya utafiti kwa ajili ya kupima kasi ya upepo katika sehemu zifuatazo:- Mkumbura (Tanga), Karatu (Arusha), Litembe (Mtwara) na Gomvu (Dar es Salaam) kwa lengo la kuzalisha umeme wa kupeleka katika gridi ya Taifa kwa kushirikiana na Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Denmark (*DANIDA*), *TANESCO*, Idara ya Hali ya Hewa, Wizara ya Nishati na Madini na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kujenga uwezo wa Mafundi Michundo wa kutengeneza mitambo ya *Biogas* katika Mkoa wa Arusha kwa kushirikiana na *SIDO* na *CARMATEC*.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2002/2003, Tume ya Taifa ya Mionzi ilitekeleza yafuatayo:-

Kutoa huduma ya upimaji wa miozi kwa wafanyakazi 970 kati ya 1,200 wanaotumia mionzi katika Vituo 121 kati ya Vituo 200 vilivyopo nchini, kukagua Vituo 171 vya *X-ray* ambapo Vituo 121 vimepewa leseni ya kutumia mionzi, Vituo 30 vimefungiwa kutoa huduma hiyo kwa sababu ya kutokidhi viwango salama vya mionzi vinavyokubaliwa Kimataifa. Vituo 20 vimeagizwa kurekebisha kasoro zilizojitokeza. Mashine 22 za *X-ray* zimefanyika marekebisho, kuhakiki vifaa vya kupimia mionzi 31 kati ya hivyo vifaa vinne vilitoka nchi ya Kenya, vifaa 18 kutoka Uganda na vifaa tisa vilikuwa vya Tume yenyewe na kukagua sampuli 2,800 za vyakula, mbolea na bidhaa nyingine ili kuepuka madhara ya mionzi ayonisha kwa wananchi kutokana na bidhaa mbalimbali zinazoingizwa na kusafirishwa nje ya nchi.

Pia kuratibu na kusimamia utekelezaji wa miradi minane inayotumia teknolojia ya mionzi hapa nchini. Miradi hiyo yenye thamani ya Dola za Kimarekani 550,000 hugharamiwa na Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomiki, *International Atomic Energy Agency (IAEA)* kwa njia ya vifaa, mafunzo na ushauri wa kitaalamu na kuendelea na ukamilishaji wa jengo la kuhifadha mabaki ya mionzi ayonisha huko Arusha ili kuepusha athari zitokanazo na mabaki ya mionzi kwa viumbe hai hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Taifa ya *UNESCO* imetekeleza yafuatayo:-

Kuratibu utekelezaji wa maamuzi ya Kikao cha 31 cha Mkutano Mkuu wa *UNESCO* kwa kushirikiana na vyombo vya Serikali na Taasisi nyingine, kuratibu utekelezaji wa miradi iliyofadhiliwa na *UNESCO* kama ifuatavyo:-

Kwanza, mradi wa kuimarisha utawala bora kwa kutumia teknolojia ya kisasa ya mawasiliano katika Manispaa ya Zanzibar, mradi huu umekamilika, mradi wa Maktaba Wilaya ya Bagamoyo, hii imekuwa Maktaba ya kwanza katika Mkoa wa Pwani, mradi wa Hifadhi ya Magofu ya Kilwa Kisiwani na Songo Mnara kama sehemu ya mradi wa Hifadhi ya Utamaduni wa Dunia na mradi wa Ujenzi wa Uzio katika Shule ya Sekondari Kigoma.

Mheshimiwa Spika, pia kuimarisha mpango wa *Club za UNESCO* na Mtandao wa Shule zilizoshirikishwa katika Mipango ya *UNESCO* kwa lengo la kudumisha amani, kuwashirikisha wataalamu wetu katika nafasi za mafunzo, mikutano na warsha zinazoandaliwa na *UNESCO* Kitaifa na Kimataifa, kuratibu kwa kushirikiana na Ofisi ya Bunge kuandaa na kuhudumia Kikao cha Waheshimiwa Wabunge wenye taaluma ya Elimu Barani Afrika kilichofanyika nchini tarehe 28 Novemba hadi tarehe 2 Desemba, 2002 na kufunguliwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu na kufungwa na Mheshimiwa Waziri Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na kuratibu kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu (Bara) na Wizara ya Elimu na Michezo (Zanzibar) Mkutano wa nane wa Mawaziri wa Elimu Barani Afrika ambao ulifanyika tarehe 2 – 6 Desemba, 2002 (*MINEDAF VIII*).

Pia kuratibu ugeni wa Mkurugenzi Mkuu wa *UNESCO* hapa nchini wa tarehe 1 hadi 4 Desemba, 2002. Hati ya Makubaliano ya Ushirikiano kati ya Serikali na *UNESCO* ilitiwa saina. Wakati wa ziara yake, Mkurugenzi Mkuu wa *UNESCO* alitunukiwa Shahada ya heshima ya Udaktari ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania na pia alizindua Chuo Kikuu cha Zanzibar (*The State University of Zanzibar*).

Mheshimiwa Spika, Mkutano wa *MINEDAF VIII* ulifunguliwa na Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa na kupitisha tamko la Dar es Salaam (*The Dar es Salaam Statement of Commitment*) linalodhamiria elimu kujenga Afrika mpya. Tanzania imechaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Mkutano huo kwa miaka minne ijayo (2003/2006). Wizara yangu imepewa jukumu hilo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Utawala na Utumishi, Wizara yangu imetekeleza yafuatayo:-

Kwanza, kupandisha vyeo vya watumishi 82 wa kada mbalimbali, kuwapatia mafunzo ya muda mrefu watumishi 13 na muda mfupi watumishi watatu ndani na nje ya nchi, kuendesha Semina za maadili katika utumishi wa umma kwa watumishi wote wa Wizara Makao Makuu pamoja na mafunzo ya jinsia kwa walimu wa Vyuo vya Ufundi na kuendesha semina na warsha kuhusu madhara na tahadhari au kinga dhidi ya ugonjwa hatari wa Ukimwi kwa watumishi wa Wizara na Vyuo Vikuu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004 Wizara yangu inatarajia kutekeleza yafuatayo:-

Kutayarisha programu za utekezaji wa mpango kabambe wa Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia 2003 – 2008 kwa kuzingatia lengo la kuviwezesha Vyuo na Asasi za Elimu ya Juu kudahili wanafunzi wengi zaidi. Aidha, mfumo bora zaidi wa Serikali wa kugharamia Elimu ya Juu utakaozingatia ufanisi, ubunifu na ujasirimali utabuniwa na kukamilisha utafiti wa mradi wa uhuishaji wa Vyuo vya Elimu ya Juu kwa lengo la kupanga matumizi bora ya rasilimali hizi.

Pia kuwasilisha Muswada wa Sheria ya Elimu ya juu Bungeni, kuboresha mitaala na mbinu za kufundishia kwa lengo la kuboresha Elimu ya Juu, kutekeleza ushauri wa wadau katika kuboresha utoaji wa Elimu ya Juu, kushirikisha wadau katika kutathmini utekezaji wa mikakati wa kuviwezesha Vyuo Vikuu kujigharamia, kuhuishia Sera ya Elimu ya Juu (1999) na kuwasilisha Bungeni Muswada wa Uanzishwaji wa Chombo cha Utoaji na Urejeshwaji Mikopo kwa Wanafunzi wa Vyuo vya Elimu ya Juu Nchini na Nje ya Nchi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2003/2004, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kinatarajia kutekeleza yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, kutekeleza programu ya Chuo Kikuu chenye yaani *Institutional Transmission Program ya University of Dar es Salaam*, kukarabati majengo na vifaa, kuongeza nafasi za wanafunzi wa shahada za juu, kuongeza madarasa, Maabara na Ofisi katika Kitivo cha Sayansi ili kupunguza msongamano uliopo sasa, kuanza awamu ya pili ya ujenzi katika jengo la Kitivo cha biashara na Uongozi na kuanza awamu ya pili ya ujenzi wa barabara za Chuo katika Kampasi ya Mlimani

pamoja na Chuo Kikuu Kishiriki cha Ardhi na Usanifu Majengo na Chuo Kikuu Kishiriki cha Tiba na Sayansi Muhimbili.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2003/2004, Chuo Kikuu Kishiriki cha Ardhi na Usanifu Mejengo kinatarajia kufanikisha yafuatayo:-

Kwanza, kuanzisha masomo ya Shahada za Uzamili katika fani za Ardhi na Uhandisi Mazingira, kujenga msingi imara katika kufundisha na kusimamia mafunzo ya Udaktari wa Falsafa kwa kushirikiana na Vyuo vingine, kutathmini masomo yanayofundishwa na jinsi yanavyofundishwa ili kufanya mabadiliko pale panapostahili, kutathmini utendaji wa kazi baada ya kuanza kutumika muundo mpya wa uongozi na kuimarisha uhusiano na Taasisi mbalimbali za Kitaifa na Kimataifa zinazohusiana na taaluma za Makazi na Mazingira.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2003/2004, Chuo kinatarajia kutekeleza yafuatayo:-

Kuimarisha mfumo wa mawasiliano ya mtandao katika majengo yake yote kufuatia Chuo kuwa na mtandao wa tovuti na kukarabati hosteli za barabara ya *Chole Road, Oysterbay*.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2003/2004, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kinatarajia kutekeleza yafuatayo:-

Kuendelea kuongeza idadi ya wanafunzi hadi kufikia wanafunzi 14,437 na kuboresha uwiano wa kijinsia kati ya wanawake na wanaume kufikia asilimia 20 ifikapo mwaka 2004/2005. (*Makofi*)

Pia kuongeza idadi ya wanafunzi wasioona na kuimarisha huduma kulingana na mahitaji yao, kuendelea kuhamasisha uandishi wa vitabu vya masomo kwa kutumia wataalamu wetu wa hapa nchini, kuanzisha karakana ya kompyuta ili wanafunzi waweze kujifunza kupitia mtandao wa kompyuta, kuendelea kuimarisha mawasiliano kati ya Makao Makuu na Ofisi za Vituo Mikoani na kuendelea na ukamilishaji wa ukarabati wa majengo ya Makao Makuu ya Chuo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, Chuo Kikuu Mzumbe kinatarajia kuanza kufundisha baadhi ya program za Chuo katika Jiji la Dar es Salaam katika jengo lililonunuliwa na Chuo, kuanza programu ya Shahada ya Udaktari wa Falsafa, kuongeza ushirikiano na Vyuo Vikuu vingine vya nje na ndani ya nchi, kufanya tathmini ya ubora wa elimu inavyotolewa na Chuo (*Academic Audit*) na kupanua, kuboresha na kuimarisha huduma za Maktaba kulingana na hadhi yake ya Chuo Kikuu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2003/2004, Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kinatarajia kutoa kipaumbele kwa miradi inayojumuisha utafiti na mafunzo ya mbinu bora za kilimo kwa wakulima, kufanya warsha/kongamano za sayansi ambazo wanataaluma na wadau kutoka ndani na nje ya nchi watakaribishwa na kujadili matokeo mbalimbali ya utafiti, kuandaa na kuendesha kozi fupi, warsha mikutano, semina na pia kutoa huduma za ushauri wa kilimo, utunzaji na usimamizi wa mali ya asili, misitu na ufugaji, kukarabati majengo na mitambo, kuboresha mazingira ya sehemu wanamoishi wanafunzi, kujenga Maabara ya Zoolojia, kupanua jengo la Maktaba iliyopo Kampasi ya Solomon Mahlangu ili kuongeza uwezo wake wa kukaa kutoka wanafunzi 300 hadi 1,000 na kujenga jengo la Kitengo cha Biashara (*Business Service Centre*).

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, Baraza litatekeleza yafuatayo:-

Baraza limeendelea kushauri, kuratibu na kuhakikisha uanzishwaji wa Vyuo bora vya Elimu ya Juu na kukagua Vyuo, kuvisajili na kuvipa ithubati, kutoa ushauri kwa Serikali na vyombo vinavyomiliki Vyuo kuhusu uendelezaji, upanuzi, uboreshaji na uwekezaji katika Elimu ya Juu, kushirikiana na vyombo vingine vinavyoratibu ubora wa elimu na mafunzo, kutayarisha mafumo ya tuzo zitakazotambuliwa Kitaifa yaani *National Qualifications Framework*, kuendelea kutoa machapisho na kuelimisha umma kuhusu majukumu na taratibu za Baraza na Elimu ya Juu kwa jumla na kuhamasisha wafanyakazi wa Baraza kuhusu kinga dhidi ya Ukimwi na katika vita ya kupambana na rushwa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka huu wa fedha 2003/2004 Mamlaka ya Elimu Tanzania inatarajia kukamilisha taratibu za ajira ya wafanyakazi watakaohudumia Mamlaka, kukamilisha taratibu, miongozo, vigezo vya matumizi ya fedha za Mfuko wa Elimu kwa ajili ya ngazi zote nne za elimu, kukamilisha utayarishaji wa masharti na kanuni za uchangiaji kwa ajili ya Mfuko wa Elimu kama itakavyoainishwa katika Mpango Kabambe wa Mamlaka na mwisho, kushirikiana na Mamlaka ya Mapato Tanzania kuandaa utaratibu utakaowawezesha wachangiaji wa Mfuko wa Elimu wanufaika na msamaha wa kodi ya mapato/ushuru wa forodha/ongezeko la thamani kama Sheria Na.8 ya mwaka 2001 inavyosema.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu katika mwaka wa fedha 2003/2004, inakusudia kugharamia mafunzo ya watumishi 22 wa Vyuo vya Ufundi Arusha na Mbeya katika ngazi ya Udaktari wa Falsafa wawili, Shahada ya Uzamili 12, Diploma ya Uzamili wanne na Stashahada ya Juu ya Uhandisi wanne, kukarabati majengo, mitambo na vifaa mbalimbali kwa Vyuo vya Ufundi vya Arusha na Mbeya, kutoa mfunzo maalum kwa wasichana katika mpango maalum wa kujiunga na Elimu ya Ufundi katika Vyuo vya Ufundi vya Arusha na Mbeya, kutoa mafunzo maalum ya Ualimu kwa Walimu Wahandisi watakoajiriwa katika Vyuo vya Ufundi vya Arusha na Mbeya, kununua na kufunga mashine na mitambo katika Chuo cha Ufundi Mbeya kwa lengo la kuboresha mafunzo yatolewayo na kuhisha Sera ya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya mwaka 1996 ili iendane na mabadiliko ya sasa ya ushindani kiteknolojia na utandawazi.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka huu wa 2003/2004, Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam inakusudia kununua kompyuta 100 kwa msaada toka Sweden (*Sida*) chini ya mradi wa *IT Fundis Project* na kuziweka kwenye Maabara ya Kompyuta ili zitumike kufundisha wanafunzi na wafanyakazi wa Chuo hicho, kuendelea kuwapeleka wafanyakazi kwenye mafunzo ya muda mfupi, muda mrefu na mafunzo ya uzamili na kuendelea kuwahudumia walioko masomoni na kukamilisha maandalizi ya mtaala wa uanzishwaji wa mafunzo ya ufundi sanifu wa migodi na madini.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2003/2004 Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi linakusudia kukagua na kusajili Vyuo 30 vyenye uwezo wa kutoa mafunzo ya Elimu ya Ufundi, kukuza na kuidhinisha mitaala ya progamu kumi (10) za mafunzo yenye kuzingatia umahiri yaani *Competence Based Curricula* na kutoa ithibati kwa Vyuo 20 vyenye uwezo wa kutoa mafunzo ya Elimu ya Ufundi na ambavyo tayari vimepata usajili.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, Wizara yangu inatarajia kukamilisha Sera ya Utafiti wa Sayansi na Teknolojia nchini, kuhisha Sheria Na.7 ya mwaka 1986 iliyounda Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia, kukamilisha Sera ya Baiteknojia, kuwatambua, kuwaendeleza na kuwagharamia wabunifu, kuwahamasisha wanafunzi wa kike kujiunga na masomo ya sayansi katika ngazi zote za elimu kwa kushirikiana na wadau wengine, kuendelea na maandalizi ya uanzishwaji wa Vituo vya Sayansi nchini pamoja na usambazaji wa teknolojia muafaka, kukamilisha dhana ya uanzishwaji wa *Centre of Excellence on Industrial Technology and Marine Sciences* na kuridhia mikataba na itifaki ya matumizi ya nishati ya nyuklia kwa shughuli za amani na usalama.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia inatarajia kukamilisha uanzishaji wa Maktaba ya Taifa ya Utafiti, kuboresha teknolojia za mawasiliano na habari nchini kwa kuendelea na upanuzi wa mtandao wa mawasiliano kwa njia ya kompyuta kati ya Taasisi, asasi na mtandao wa watafiti wa ndani na nje ya nchi na kutoa mafunzo kwa wadau mbalimbali, kufuatilia utekelezaji wa miradi ya matumizi ya nishati mbadala kama vile makaa ya mawe, mionzi ya jua, upepo wa gesi ya samadi majumbani ili kupunguza madhara ya ukataji miti, kufanya utafiti wa matumizi ya teknolojia za upepo kutoa umeme na matumizi ya makaa ya mawe majumbani kwa kutumia vumbi linalopatikana huko Kiwira na kuandaa kongamano la wanasayansi na watafiti pamoja na Maonyesho ya Sayansi ya Vijana.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2003/2004, Tume ya Taifa ya Mionzi itatekeleza kwanza, kusimamia utekelezaji wa sheria ndogo ya kudhibiti viwango vya mionzi kwenye chakula kwa kupima sampuni za vyakula vyote viingiavyo kutoka nje ya nchi, kuanzisha upimaji wa vyanzo vya mionzi katika migodi sita hapa nchini. Migodi hiyo ni pamoja na *Kahama Gold Mines* (Shinyanga), *Geita gold Mines* (Mwanza), *Afrika Mashariki Gold Mines* (Musoma), *Nzega Gold Mines* (Shinyanga), *Mererani*

Tanzanite Mines (Arusha) na *Kiwira Coal Mines* (Mbeya), kukusanya mabaki ya vyanzo vya mionzi kote nchini na kuyahifadhi katika Maabara iliyoko Arusha, kukamilisha mpango wa kushughulikia dharura za mionzi Kitaifa yaani *Radiological Emergency Plan Preparedness* na usalama wa vyanzo vya mionzi (*security of radioactive sources*) na kuimarisha na kutoa miongozo ya uendeshaji wa majukumu ya Tume ya Nishati ya Atomiki (*The Tanzania Atomic Energy Commission - TAECCO*).

Mheshimiwa Spika, katika mwaka huu wa fedha 2003/2004, Tume ya *UNESCO* inatarajia kuendelea kuratibu utekelezaji wa maamuzi ya kikao cha 31 cha Mkutano Mkuu wa *UNESCO* kwa kushirikiana na vyombo mbalimbali vya Serikali na Taasisi nyingine, kuandaa kwa kushirikiana na vyombo mbalimbali *program* na Bajeti ya *UNESCO* kwa mwaka 2004 – 2005 ambayo itawasilishwa kwenye Kikao cha 32 cha Mkutano Mkuu wa *UNESCO* utakaofanyika Paris, Ufaransa mwezi Septemba – Oktoba 2003. Wizara yangu itaongoza Ujumbe wa Serikali katika Mkutano huo, kuratibu utekelezaji wa miradi itakayoidhinishwa chini ya Hati ya Makubaliano kati ya *UNESCO* na Serikali ya Tanzania na miradi mingine inayoendelea na ile itakayoidhinishwa na Shirika hilo kupitia *program* zake mbalimbali na kuratibu ufuatiliaji wa mpendekezo ya Mkutano wa Nane wa Mawaziri wa Elimu Barani Afrika.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Utawala na Utumishi inatarajia kudhamini watumishi 40 mafunzo ya muda mrefu na watumishi 120 mafunzo ya muda mfupi, kuwapandisha vyeo watumishi 66 wa kada mbalimbali ambao wametimiza masharti ya ajira zao, kuendelea kuendesha semina za maadili Wizarani kwa lengo la kuboresha utoaji huduma kwa wananchi, kuendelea kuendesha Semina na Warsha kwa wafanyakazi kuhusu athari za ugonjwa hatari wa Ukimwi na kuwaelimisha watumishi wa Wizara kuhusu mpango wa maboresho ya Utumishi wa Umma (*PSRP*).

Mheshimiwa Spika, kama nilivyolieleza Bunge lako Tukufu katika mwaka wa fedha 2002/2003 kuwa Dira ya Wizara yangu ni kujenga jamii iliyolimika yenye uwiano wa kijinsia na inayoweza kujiletea maendeleo kwa kutumia sayansi na teknolojia. Katika kufikia azma hiyo, Wizara yangu imedhamiria kuweka mkazo katika maeneo yafuatayo:-

Kuimarisha Tume ya Sayansi na Teknolojia kwa minajili ya kuhamasisha matumizi ya sayansi na teknolojia katika maendeleo ya Taifa, kuimarisha utafiti na kusambaza matokeo ya tafiti mbalimbali hapa nchini, kuhamasisha wanafunzi wengi zaidi wa kike kujiunga na Elimu ya Juu na Ufundi, kutoa mwongozo kwa wabunifu/wagunduzi wanasayansi katika ngazi zote hapa nchini, kuhakikisha teknolojia mpya zinazolingizwa nchini na kusambazwa kwa wananchi hazileti madhara, kuanzisha chombo cha kutoa na kurejesha mikopo ya kugharamia elimu na kuimarisha Chuo cha Ufundi Mbeya katika hatua za kukigeuza kuwa Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ili hatimaye kiwe Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia. Pia kuendelea kuboresha mitaala na mbinu za kufundishia kwa lengo la kuboresha Elimu ya Juu na Ufundi ili kukidhi haja ya soko la ajira, kuendelea kuweka uwiano mzuri kati ya idadi ya wanafunzi wa kike na kiume katika Vyuo vya Elimu ya Juu na Vyuo vya Ufundi nakuratibu na kuhakikisha uanzishwaji wa Vyuo bora vya Elimu ya Juu na vya Ufundi, kuvikagua, kuvisajili na kuvipa ithibati. Pia kuendelea kuhamasisha wananchi kuhusu dhana ya uchangiaji na uwekezaji katika Elimu ya Juu, kuboresha mazingira ya kazi ikiwa ni pamoja na kuimarisha mafunzo kwa watumishi na wanataaluma, kuendelea kuhamasisha wanafunzi na wafanyakazi kutambua na kujihami dhidi ya madhara ya ugonjwa hatari wa Ukimwi na kuimarisha Tume ya Taifa *UNESCO*.

Mheshimiwa Spika, pia, kuendelea juhudi za kupambana na rushwa katika Wizara na Taasisi zake, kuweka mipango na mbinu thabiti ya kuongeza udahili na udhamini wa wanafunzi katika Vyuo Vikuu na Asasi za Elimu ya Juu, kushirikiana na Sekta binafsi katika kuanzisha Mfuko wa Mafunzo ya ubingwa katika fani za Utawala, Biashara Fedha, Ufundi na Sheria na kukamilisha mpango wa kuanzisha Vituo vya ubora wa juu (*Centre of Excellence*) katika elimu ya juu, Ufundi, Utafiti na Teknolojia.

Mwisho, napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa Wahisani na Wadau mbalimbali kwa mchango wao mkubwa wanaoutoa katika Wizara yangu. Ni dhahiri kuwa msaada walioutoa katika kuboresha Sayansi na Teknolojia, Elimu ya Juu na ya Ufundi umekuwa na manufaa makubwa. Nchi hizo ni pamoja na Sweden, Uholanzi, Japan, Ubelgiji, Korea, China na Umoja wa Nchi za Ulaya. Aidha, Mashirika ni pamoja na Benki ya Dunia, *Commonwealth Science Council*, *International Atomic Energy Agency*, *Third World Academy of Sciences*, *International Foundation for Sciences*, *UNESCO* na Shirika la

Maendeleo la Sweden (*SIDA/SAREC*), *Carnegie Foundation* na *NORAD*. Naomba kuwashukuru hao na waendeleo na ushirikiano huu tulionao.

Mheshimiwa Spika, ili kuiwezesha Wizara yangu na Taasisi zake kutekeleza mipango iliyojiwekea katika mwaka wa fedha 2003/2004, sasa naliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 86,140,463,400.00. Kati ya fedha hizo shilingi 69,536,245,300.00 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 16,604,218,100.00 ni kwa matumizi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

MHE. MARGARETH A. MKANGA (k.n.y. MHE. OMAR S. KWAANGW' – MWENYEKITI WA KAMATI YA HUDUMA ZA JAMII): Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii, awali ya yote nashukuru kwa kunipa nafasi ya kutimiza masharti yaliyomo kwenye Kanuni ya 81(1) ya mwaka 2003 ya kutoa maoni ya Kamati ya Huduma za Jamii uliyoipa ya kuchambua Taarifa ya utekelezaji na malengo yaliyowekwa na Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu kwa mwaka 2002/2003 na kupitia malengo na makadirio ya mwaka wa fedha 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Huduma za Jamii ilikutana tarehe 6 Juni, 2003 Dar es Salaam na kupata muda wa kutosha kuchambua na kujadili dira na majukumu ya Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, utekelezaji wa maagizo na mapendekezo ya Kamati iliyoichambua Bajeti ya mwaka ya Wizara ya mwaka 2002/2003, malengo yaliyopangwa kutekelezwa mwaka wa fedha wa 2003/2004 na maombi ya fedha kwa mwaka 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, baada ya Kamati kujadili na kuchambua vipengele nilivyotaja hapo juu Mheshimiwa Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu na Naibu Waziri wake wakisaidiana na Timu ya Wataalam wakiongozwa na Katibu Mkuu wa Wizara na walijibu hoja na maswali ya Wanakamati kwa ukamilifu na hivyo Kamati kukubali hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu iletwe mbele ya Bunge lako Tukufu. Kwa maelezo hayo Kamati yangu inaunga mkono hoja hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, maoni na mapendekezo ya Kamati, pamoja na kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, Kamati ina maoni na ushauri ufuatavyo kwa Serikali kupitia Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, kuhusu dira na majukumu ya Wizara, Kamati ya Huduma za Jamii, inakubali mwelekeo wa dira ya Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, inayolenga kuwa ifikapo mwaka 2025 Serikali iwe imefanikiwa kujenga jamii iliyoelimika, yenye uwiano wa kijinsia (*Gender Balance*) na inayoweza kujiletea maendeleo kirahisi kwa kutumia sayansi na teknolojia.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Huduma za Jamii, inaunga mkono dira ya Wizara hii inayohimiza wananchi na Taifa kwa ujumla kujiletea maendeleo kwa kutumia Sayansi na Teknolojia katika nyanja mbalimbali za uchumi, kurahisisha uzalishaji na uboreshaji unaoweza kuzalisha. Aidha, kwa kuzingatia wito wa Jumuiya ya Kimataifa kuwa karne ya 21 ni ya kuhimiza maendeleo na matumizi ya sayansi na teknolojia, katika kujenga uwezo na ustawi wa Taifa kiuchumi na kijamii. Kamati inapendekeza kuwa ili kuleta maendeleo yanayotamkwa na dira hii ni vema Serikali ikatekeleza kwa vitendo nadharia hii.

Mheshimiwa Spika, katika azma ya Serikali kutekeleza Sera ya kuinua maendeleo ya uzalishaji kwa kutumia sayansi na teknolojia, Kamati inayo mapendekezo na ushauri kuwa mfuko wa Maendeleo wa Sayansi na Teknolojia, Serikali ijenge misingi ya kuliwezesha Taifa kutumia na kuendeleza Sayansi na Teknolojia katika shughuli zote za uzalishaji na hatimaye kuongeza kasi na ubora wa uzalishaji katika Sekta zote za uchumi.

Pia Serikali ione umuhimu wa kutenga fedha katika bajeti yake, kuanzia mwaka ujao wa fedha angalau asilimia moja ya pato la Taifa kwa ajili ya kuendeleza utafiti. Katika nyanja ya Sayansi na Teknolojia unaofanyika katika Asasi mbalimbali na Serikali ianzishe utaratibu wa kutambua na kuwaenzi wavumbuzi wa vifaa mbalimbali.

Aidha, Kamati inashauri kuwa mafanikio yanayopatikana katika utafiti yaendelezwe na yasambazwe kwa wazalishaji hasa walioko vijijini ambao ndiyo wazalishaji wakuu ili yarahishe shughuli za uzalishaji na kuleta ufanisi. Pamoja na kusambaza mafanikio hayo, Kamati inashauri Wizara ioanishe *rationalize* utafiti na huduma za ugani zinazotolewa kwa wakulima ili waelewe umuhimu wa kutumia mbegu bora kila msimu zinazoandaliwa kitaalam ili kutoa mazao mengi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na ushauri huo hapo juu, Kamati inasisitiza umuhimu wa kuendeleza utafiti na mafanikio yaliyokwishapatikana ikizingatiwa kuwa nchi nyingi zilizofanikiwa kiuchumi kuendelea kutenga fedha katika bajeti zao kwa ajili ya kuendeleza utafiti ili kukidhi mabadiliko katika mahitaji ya jamii yanayoendana na wakati. Vile vile ikizingitiwa kuwa maendeleo ya Sayansi na Teknolojia ni kigezo muhimu katika kukuza maendeleo ya kiuchumi pamoja na majukumu mengine yanayoikabili Serikali kifedha ni vema ikatekeleza azma yake ya kuendeleza na kukuza matumizi ya Sayansi na Teknolojia kwa kutenga fedha kwa ajili ya kuendeleza utafiti.

Mheshimiwa Spika, kuhusu usajili wa Vyuo wa Elimu ya Juu, Kamati yangu ilijadili taratibu na vigezo vinavyotakiwa kufikiwa kwa ajili ya Vyuo vya Elimu ya Juu vinavyoanzishwa kuweza kupata usajili wa kudumu kupitia Baraza la Ithibati la Elimu ya Juu.

Mheshimiwa Spika, Kamati inakubaliana na uamzi wa Baraza la Ithibati wa Elimu ya Juu kwa kushitisha shughuli za Chuo cha Teknolojia ya Tiba (*IMTU*) na *Bukoba University* baada ya Vyuo hivyo kushindwa kutekeleza kwa ukamilifu, taratibu, kanuni na vigezo vya kuendesha vyuo vikuu. Kamati ina maoni kuwa ni muhimu sana kwa Vyuo Vikuu vyote kuzingatia vigezo vyote vya Baraza la Ithibati ikiwa ni pamoja na kuwepo Wahadhiri wenye sifa, wanaotosheleza, mitaala inayokidhi taaluma inayotolewa, vifaa na mazingira bora na sahihi ya kufundishia na kujifunzia.

Kuanzishwa kwa Vyuo Vikuu Vishiriki (*Campus Colleges*), Kamati imepokea mapendekezo ya Wizara ya umuhimu wa kuanzisha Vyuo Vikuu Vishiriki ndani ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, ikijulikana kama *Campus Colleges* kwa lengo la kufanikisha na kurahisisha utekelezaji wa majukumu ya Chuo. Aidha, Kamati ilielezwa kuwa badala ya kuwa na Vitivo vya Uhandisi, Ujenzi na Mazingira jengwa, uhandisi mnene, mifumo ya kompyuta na Uhandisi mitambo na Kemikali. Inapendekezwa kuanzishwa chuo cha *Campus* cha Uhandisi na Teknolojia na kuwa maandilizi yalikuwa yamekamilika.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri kuwa Vyuo Vikuu Vishiriki vianzishwe vikiwa ni jawabu la kutatua matatizo ya kiutendaji na kuleta ufanisi katika utoaji wa elimu ya juu. Aidha, Kamati inashauri kuwa ili kuepukana na matatizo ya utekelezaji yaliyojitokeza katika kuanzishwa vyuo *IMTU* na *Bukoba University*, uanzishaji wa vyuo hivyo uzingatie taratibu na vigezo vya Baraza la Ithibati na Elimu ya Juu na Sheria. Aidha, Kamati inashauri Sheria zitakazotungwa vijitosheleze na vikidhi mahitaji ya vyuo hivyo kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kituo cha *Computer, Dar es Salaam University Computing Center*, Kamati inapongeza juhudi zinazofanywa na Kituo hicho kwa kutoa mafunzo katika taaluma mbalimbali za kompyuta katika viwango vinavyokubalika na pia kufungua vituo vya kufundishia taaluma hii muhimu Mikoani. Hatua hii itawezesha watu wengi kupata taaluma hii muhimu inayohitajika katika ulimwengu wa sasa. Vile vile Kamati inapongeza uongozi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa kuungana na vyuo vingine nje ya Baraza la Afrika kwa kutumia teknolojia ya mawasiliano na kuweza kupokea na kuendeleza mafunzo kwa njia ya mtandao wa kompyuta.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu inaona kuwa katika siku za hivi karibuni Vyuo vya kufundisha taaluma ya kompyuta vimeota kama uyoga mitaani, bila udhibiti wa ubora wa kutoa taaluma hii muhimu, hasa suala la mitaala na walimu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri kuwa Serikali iweke utaratibu utaoweka vigezo vya kufikiwa kabla ya kuanzisha vyuo vya kompyuta ikiwa ni pamoja na kuainisha mitaala, sifa za wakufunzi na tuzo zinazotolewa ili taaluma hii itolewe na wenye taaluma sahihi na katika mazingira yanayofaa. Hivyo, Kamati inashauri Serikali kuchukua hatua madhubuti za kuwezesha wananchi kupata taaluma sahihi na kwa viwango vinavyokubalika kwa kila ngazi iwe ya cheti, stashahada na shahada.

Mheshimiwa Spika, udahili wa wanafunzi, Kamati inaipongeza Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu kwa ajili ilivyoshirikiana na uongozi wa vyuo vikuu hapa nchini katika kutekeleza programu na mipango kamambe ya kuendeleza na kupanua asasi na vyuo. Mfano, *UDSM 2000, SUA 2000* na kadhalika ambayo ilianzishwa kwa madhumuni ya kuboresha mazingira ya kujifunzia na kuongeza idadi ya wanafunzi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kununua hosteli mbili za Kijitonyama na Ubungo zenye uwezo wa kutoa malazi kwa watu 566 na kutoa fedha za ujenzi wa hosteli ya wanafunzi kwa shahada ya uzamili. Vile vile Kamati inaupongeza uongozi wa Mfuko wa Hifadhi ya Taifa (*NSSF*), kwa kukamilisha ujenzi wa hosteli za wanafunzi Mabibo zenye uwezo wa kutoa nafasi ya malazi kwa wanafunzi 4,200. Hatua hii inaonyesha dhahiri utekelezaji wa dhati katika kupanua elimu ya juu.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua juhudi za Serikali za kudhamini wanafunzi kila mwaka kutokana na uwezo wake. Hata hivyo, Kamati inashauri kuwa kutokana na wingi wa wanafunzi wenye sifa za kujiunga na elimu ya juu kuongezeka, Serikali iweke mipango kabambe itakayowezesha kupanua miundombinu ya vyuo vya elimu ya juu kukabiliana na ongezeko hilo. Aidha, Serikali imewaelimisha wananchi utaratibu unaotumika kudhamini wanafunzi wanaosoma katika vyuo vya elimu ya juu hivi sasa na mipango ya baadaye.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali imefanikiwa kutekeleza mpango wa kuboresha elimu ya msingi MEM na kwa sasa inajiandaa kuanza utekelezaji wa mpango wa elimu ya sekondari, ni vema pia ikaanza kujiandaa kupokea na kuendeleza matokeo ya mipango hiyo katika ngazi ya elimu ya juu kwani wanafunzi wengi wenye sifa za kujiunga na vyuo vya elimu ya juu watakosa nafasi kutokana na uhaba wa nafasi katika vyuo na pia ukosefu wa fedha za kugharamia elimu hiyo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri kuwa sasa ni muda muafaka vyuo vikuu kutumia wataalam wake kubuni vyanzo vingine vya fedha za kusaidia Bajeti ya Serikali katika kufanikisha utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya vyuo ikiwa ni pamoja na kulipa gharama za kuongeza wanafunzi wengi zaidi kwa taaluma mbalimbali kupata wataalam wengi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri kuwa Serikali isaidiane na uongozi wa vyuo vya elimu ya juu kuhamasisha na kuweka utaratibu utakaokubalika kwa mashirika ya kampuni kubwa zenye viwanda. Huduma za uzalishaji na migodi, kwa mfano, *TBL, CELTEL, VODACOM, TTCL, Mwadui Diamond* na kadhalika ambazo baadhi yake vimeweza kudhamini michezo na kadhalika. Pia vimetoa asilimia ndogo ya mapato yao kwa ajili ya kusaidia Serikali kugharamia masomo katika vyuo vya elimu ya juu kwa vile nao huhitaji wahitimu wazuri kwa ajira mbalimbali kwenye makampuni yao.

Mheshimiwa Spika, chombo cha kutoa na kurejesha mikopo. Kamati imepokea maelezo kuhusu hatua ya Serikali ya kuanzisha chombo cha kuratibu utoaji na urejeshwaji wa mikopo ya kugharamia elimu ya juu kuanzia mwaka huu wa fedha. Kamati inashauri kuwa chombo hiki kiwezeshwe kutoa mikopo kwa wanafunzi wote waliopo katika vyuo vya elimu ya juu nchini.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri kuwa chombo hiki pia kipewe uwezo wa kufanikisha azma ya Serikali ya kuboresha uwiano wa kijinsia kwa kutoa mikopo zaidi kwa wasichana wenye sifa za kujiunga na elimu ya juu. Pia chombo hiki kiwe na mawasiliano ya karibu na mifuko mingine inayosaidia kugharamia elimu ya juu kwa wasichana kama *Free Entry Female Programme, Scholarship, Human Resource Development Trust Fund, Women Education Fund, Student Assistance Fund* na Taasisi ya Sayansi za Bahari Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatoa pongezi kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa kutoa hati ya kumiliki eneo la Buyu lililotengwa kwa ajili ya kupanua Taasisi ya Sayansi ya Bahari ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Matazamio ya Kamati ni kuwa kwa mwaka huu wa fedha ujenzi wa Chuo hicho utaanza.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Elimu ya Ufundi, Kamati ilitafakari maendeleo ya elimu ya ufundi nchini na umuhimu wake katika karne hii kwa kuleta maendeleo na mabadiliko katika njia za uzalishaji. Pamoja na jitihada za Serikali, Kamati inaona kuwa baada ya elimu hii ipo katika kiwango ambacho inabidi kiboreshwe. Hata hivyo, Kamati inaunga mkono Serikali hatua za kuimarisha elimu ya ufundi hasa kwa kuunda Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi lenye jukumu la kuweka na kusimamia ubora wa viwango vya elimu ya ufundi na kuidhinisha tuzo zinazotolewa vyo vya ufundi.

Mheshimiwa Spika, matazamio ya Kamati ni kuwa Baraza la Elimu ya Ufundi litaendelea kusimamia ubora wa elimu ya ufundi nchini ili tuzo zinazotolewa zilingane na elimu na ujuzi.

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Ufundi Dar es Salaam. Kamati inashauri Serikali kufanya juhudi za makusudi kuboresha Taasisi ya Ufundi Dar es Salaam ili iweze kufikia azma yake ya kuwa Taasisi yenye ubora wa hali ya juu *Center of Excellency*, yenye uwezo wa kutoa elimu ya ufundi inayokidhi mahitaji na soko la ajira ya ushindani. Juhudi hizo ziwe ni pamoja na kufanyia ukarabati majengo ya chuo ambao baadhi yake yamechakaa sana. Kwani ni ya muda mrefu na mengi ni ya tangu mwaka 1957.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri kuwa Serikali iboreshe mazingira na vifaa vya kufundishia. Wawekwe wakufunzi wenye sifa na mitaala inayokidhi matakwa ya vigezo vya tuzo za Baraza la Ufundi la Taifa yanayoendana na mahitaji ya wataalam katika soko la ajira.

Mheshimiwa Spika, Kamati vile vile inashauri kuwa uongozi wa Chuo ubuni vyanzo vingine vya fedha nje ya Bajeti ya Serikali ili kufanikisha ukarabati wa miundombinu ya chuo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na ushauri uliotolewa hapo juu Kamati inashauri kuwa ikamilishe taratibu za kisheria za kuiwezesha Taasisi ya Ufundi Dar es Salaam ili iwe na uwezo wa kujitegemea, walimu wenye sifa. Kuandaa mitaala na uwezo wa kutunga mitihani yake na kutoa tuzo na hivyo kuondokana na malalamiko ya walimu, wanafunzi na wahitimu wa Taasisi hiyo hasa wanapopata nafasi za kuchukua masomo ya juu zaidi.

Mheshimiwa Spika, tangu mwaka 1997 ilipotungwa Sheria Na. 6 ya kuanzisha Taasisi ya Ufundi Dar es Salaam Serikali haijakamilisha taratibu za kukipa uwezo wa kujitegemea na ndiyo sababu wanafunzi na wafanyakazi wa *DIT* kulalamika mbele ya Kamati ilipotembelea Taasisi hiyo hivi karibuni.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Ufundi Mbeya. Kamati inashauri kwamba kwa kuwa Serikali imeshatenga hekta 418 za ardhi, kwa ajili ya upanuzi wa Chuo cha Ufundi Mbeya, ni vema Serikali ikaongeze kasi ya kupanua na kuimarisha chuo hicho ili hatima yake kiwe Chuo kikuu cha Sayansi na Teknolojia. (*Makofi*)

Muda wa kustaafu wana taaluma wa Vyuo Vikuu, Kamati inaipongeza Serikali kwa kukubali kimsingi kuongeza muda wa kustaafu kwa lazima kwa wana taaluma (*Professors*) katika vyuo vya elimu ya juu hadi miaka 65. Hatua hii itawezesha Taifa kunufaika na taaluma zao hasa kipindi hiki ambapo Serikali inatekeleza azma yake ya kuongeza idadi ya wanafunzi katika vyuo vya elimu ya juu. Kamati inashauri Serikali kuboresha Sheria zinazohusika ili wahusika waendeleo na kazi kwa kuzingatia sheria na ifuatilie kwa karibu uwezo wa wana taaluma hao kufundisha na kufanya utafiti katika umri huo mkubwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri kuwa Serikali ione umuhimu wa kuwatumia vizuri wana taaluma wazalendo katika shughuli za ushauri wa kitaalam *Consultant* mara nafasi zinapotokea badala ya kuwaagiza wataalam hao kutoka nje ya nchi kwa gharama kubwa, ambalo inawezekana baadhi ya wanaoletwa wakawa hawajabobea kitaalam kama wana taaluma wetu. Hatua hii ni pamoja na kutoa ushauri wa kitaalam katika miradi au mipango ya kitaifa.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri kwamba kwa kuwa wana taaluma wengi hutumia muda mwingi katika utafiti wa kitaalam na kufundisha na kwa vile ujuzi wao unahitajika hata kwa nchi za nje, hali ambayo hupelekea baadhi yao kwenda kufanya kazi nje ya nchi wakati bado tunawahitaji. Ni vema

Serikali ifikirie njia bora ya kuwapatia marupurupu, *a good attractive package* ili wasiendeele kuhangaika kutafuta maslahi bora zaidi. *(Makofi)*

Mwisho nachukua nafasi hii kumpongeza Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, Mheshimiwa Dr. Pius Ng'wandu, Naibu wake Mheshimiwa Zabein Muhaji Mhita, kwa ushirikiano wao na Kamati yangu wakati wa kujadili na kuchambua utekelezaji wa Wizara yao kwa mwaka 2002/2003 na malengo ya Bajeti ya mwaka 2003/2004. Aidha, nawapongeza Wataalam wote wa Wizara hii wakiongozwa na Katibu Mkuu, Ndugu Ruth Mollel, kwa ushirikiano walioutoa katika kujibu hoja na maswali wakati wa kuchambua bajeti ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wa Kamati ya Huduma za Jamii kwa umakini na ushirikiano wao mkubwa wakati wa kujadili Fungu 68 sasa naomba niwatambue kwa majina, nao ni Mheshimiwa Omar Kwaangw', Mwenyekiti, Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir, Mheshimiwa Mohamed Abdully Ally, Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji, Mheshimiwa Kheri Khatib Ameir, Mheshimiwa Parmukh Singh Hoogan, Mheshimiwa Janet Kahama, Mheshimiwa Stephen Kahumbi, Mheshimiwa Halimenshi Mayonga, Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, Mheshimiwa Oscar Mloka, Mheshimiwa Alhaji Ahamadi Mpeme, Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi, Mheshimiwa Hamisi Nguli, Mheshimiwa Said Nkumba, Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba na mwisho mimi mwenyewe Mheshimiwa Margareth Mkanga. *(Makofi)*

Mwisho, nampongeza Katibu wa Bunge na Katibu wa Kamati hii kwa kuratibu shughuli za Kamati hadi maoni ya Kamati kutoka.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI – MSEMaji MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA SAYANSI, TEKNOLOJIA NA ELIMU YA JUU: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, napenda kutanguliza shukrani kwako wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ili niweze kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani Bungeni kuhusu hotuba ya Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu kwa Bajeti ya mwaka 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, nafurahi vile vile kuchukua nafasi hii kuwapongeza sana Wabunge wote waliochaguliwa katika uchaguzi mdogo wa mwezi Mei, mwaka 2003 kwa ushindi wao. Nawapongeza kwa maana ya kipekee Wabunge wa *CUF* kwa kuwaonyesha Watanzania na dunia nzima kuwa uchaguzi ukiwa wa uhuru na haki kila chama kinaweza kupata ushindi halali kinaostahili. *(Makofi)*

Vile vile nampongeza sana Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, Mbunge kwa kuchaguliwa kuwa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawapongeza viongozi wote wa Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu wakiongozwa na Mheshimiwa Dr. Pius Ng'wandu, kwa kazi yao nzuri wanayoifanya katika Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama ilivyo jina la Wizara hii Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, basi na mimi wakati wa kutoa maoni nitazingatia sana dhana na dhima ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu kama injini muhimu katika kuharakisha maendeleo ya kiuchumi na kijamii katika karne ya 21. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, elimu ya juu, bila ya kupoteza muda wa kurudia hadithi ya hali halisi ya nafasi ya Tanzania katika nchi zote duniani kuhusu idadi ya Vyuo Vikuu ilivyo navyo, idadi ya wanafunzi katika Vyuo Vikuu hivyo la muhimu hapa kuikumbusha Serikali kuwa inatakiwa kuandaa programu ya mipango kamambe ya kuongeza idadi ya Vyuo Vikuu hapa Tanzania kwa awamu ya miaka mitano mitano, kuongeza idadi ya wanafunzi katika vyuo hivyo kwa kuweka idadi kamili ya wanafunzi wanaopaswa kudahiliwa mwaka wa kwanza kila mwaka kwa kila Chuo Kikuu, kuandaa mpango wa ujenzi wa miundombinu inayohitajika katika Vyuo Vikuu na makadirio ya gharama zake halisi na kuandaa mpango kamambe wa jinsi ya kupata walimu wa kutosheleza kufundisha kwenye vyuo vikuu hivyo.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inatoa maoni haya kwa sababu tumegundua kuwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kilipanga kuwa kitaongeza idadi ya wanafunzi wanaoingia mwaka wa kwanza kwa shahada ya kwanza kuwa 3,500 kwa mwaka wa 2002 na kwamba ifikapo mwaka 2008 wanaoingia mwaka wa kwanza wawe 13,000. Lakini kwa kuwa Serikali haikuhusika kwa sababu inazozijua yenyewe, inachukua hatua ambazo ni dhahiri hazitatosheleza kufikiwa kwa kiwango hicho. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, mfano, ni pale ambapo Serikali ilidhamini wanafunzi 3,500 mwaka 2002/2003 na hivi sasa mwaka 2003/2004 imedhamini wanafunzi 2,500. Uamuzi huu unaing'oa mizizi ya ndoto ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kutimiza malengo yake. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, wakati takwimu zinaonyesha kuwa wanafunzi wanaopashwa kudahiliwa kuingia mwaka wa kwanza Chuo Kikuu ni 6,000 ni wanafunzi 2,500 tu walidahiliwa na kuwaacha wengine 3,500 wakitamani elimu ya Chuo Kikuu na hii ndiyo Serikali ya Tanzania iliyopania kwa maneno yaliyomo kwenye Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2002/2025 kuwa na jamii iliyoolimika na inayotumia sayansi na teknolojia. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani ingefurahi na Watanzania wote wangepurahi pia kama Serikali ingetoa majibu ya ni kwa nini Tanzania inatoa wahitimu 10,000 karibu wastani wa 10,000 kila mwaka wakati Uganda inatoa wahitimu 40,000, Kenya wahitimu 50,000. (Makofi)

Je, Tanzania kwa kuwa iko katika *East African Community* ndiyo nchi yenye idadi ya watu wengi na itatumia mbinu gani ili angalau kuwa katika kiwango kimoja cha idadi ya wahitimu na Kenya ndani ya miaka mitano ijayo? (Makofi)

Je, Serikali haioni kuwa kwa kutoa wahitimu 10,000 ambapo baada ya miaka 20 iliyobaki itakuwa imetoa wahitimu kwa kuzidisha vile 220,000 au kama itajitutumua lakini 440,000 ifikapo mwaka 2025 na je, Serikali haioni kwa kuwa kwa mwendo huu wa kinyonga, Tanzania itakuwa nchi yenye watu wenye elimu ya chuo kikuu wasiozidi 700,000 kati ya watu wasiopungua milioni 60 watakuwa wanaishi katika Tanzania ifikapo mwaka 2025? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inapenda kutoa maoni yafuatayo na kwa kweli Watanzania wangekiingiza chama chochote cha upinzani chenye Wabunge Bungeni madarakani tungefanya yafuatayo:- (Makofi)

Kwanza, ifikapo mwaka 2005 kila Mkoa ungelikuwa na Chuo Kikuu kinachoendeshwa kwa gharama za Serikali. Pia, ifikapo mwaka 2007 wanafunzi wanaosoma shahada ya uzamili na udaktari wa falsafa ingeongezeka kutoka 700 ya sasa hadi 7,000. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, pia tungeongeza mshahara wa walimu wa chuo kikuu kutoka *take home* ya shilingi laki moja kwenda shilingi milioni moja na *point* tano. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, wenzetu walioko Serikalini watauliza, je, fedha hizo za kuanzishia vyuo vikuu kila mkoa mtazitoa wapi? Jibu ni rahisi, pale zilikutoka shilingi bilioni 40 za kununulia *rader* au zitakapotoka shilingi bilioni 40 za kununulia ndege ya Rais na wala sisi hatusemi ndege isinunuliwe wala *Radar* isinunuliwe na hata pale ambapo shilingi bilioni 60 hazikulipwa na *TTCL*. Hela hizi zote tungekusanya kwa hekima na busara tungeweza kupata angalau shilingi bilioni kumi kumi kwa kila mkoa kwa Mikoa 14 za kuanzia ujenzi wa Chuo Kikuu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hapa tunachosisitiza ni kwamba ni pamoja na *Financial Discipline* pamoja na kipaumbele Mheshimiwa Spika. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa utaratibu wa kanuni za Bunge uliotoa nafasi kwa Kamati ya Kudumu za Bunge, umetekelezwa vizuri kwa wewe Mheshimiwa Spika, kuwapanga Wasemaji wa Kambi ya Upinzani Bungeni kwa kila Wizara, kuwa Wajumbe wa Kamati za Kudumu za Bunge zinazohusika na kila Wizara, Msemaji anayosemea. Basi Kambi ya Upinzani inayajua maoni ya Kamati mapema na haioni sababu ya kuyarudia rudia katika maoni yake. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani imezipokea taarifa za kusitishwa kwa shughuli za Chuo Kikuu cha Teknolojia ya Tiba, IMTU pamoja na ile ya Chuo Kikuu cha *Bukoba University*. Kambi ya Upinzani imesononeka na kuona aibu kwa niaba ya Watanzania wote si kwa sababu Baraza la Ithibati ya Elimu ya Juu haikuwa na sababu za kusitisha shughuli za Vyuo hivyo. Bali ni kwa sababu Kambi ya Upinzani haiamini kuwa kwa mfano, watu wapatao milioni mbili na nusu wa Mkoa wa Kagera tena *Nshomile*. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, Serikali yao inayodhamiria kugeuza jamii ya Watanzania kwa miaka 20 ijayo kuwa ya watu walioboea katika masuala ya sayansi na teknolojia katika maisha yao ya kila siku wanguhindwa kuziendeleza shughuli za Chuo Kikuu hicho na hii ikizingatiwa ni kwamba Mkuu wa Chuo Kikuu hicho cha Bukoba yuko humu Bungeni. (*Makofi*)

Aidha, Serikali ingekubali kuona chuo pekee chenye kushughulikia teknolojia ya Tiba kinatelekezwa. Sasa nigeukie upande wa Sayansi na Teknolojia, kabla sijaendelea napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa nilipotakiwa kuandaa hotuba hii nilitamani kuleta na kurudia kusoma hotuba yangu kuhusu Wizara hii niliyoitoa tarehe 18 Julai, 2001 kuhusu vipengele kadhaa vinavyohusu Sayansi na Teknolojia chini ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, dira ya Wizara pamoja na Taifa kufikia mwaka 2025 ni kujenga na kuboresha jamii iliyoelimika na ya kisasa katika matumizi ya Sayansi na Teknolojia ili kuleta maendeleo ya haraka ya kiuchumi na kijamii kwa nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika hotuba yangu ya tarehe 18 Julai, 2001 nilisema yafuatayo kuhusu dira ya Wizara na Taifa kuhusu Sayansi na Teknolojia. Napenda kunukuu, “Lakini Kambi ya Upinzani ina wasiwasi na udhati, dhamira na uwezo wa Serikali yetu wa kuweka matendoni yale yote yaliyoainishwa katika dira hii na hii ni kutokana na kwanza, ufinyu wa fedha zinazotolewa kwenye Bajeti ya Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu na pili, tafsiri nyembamba ya Wizara hii, kwa dhana ya kuiangalia katika muktadha wa elimu ya juu tu. Huku Idara za Sayansi na Teknolojia zikipewa uzito ndogo hasa katika kiasi cha fedha zinazotolewa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Tanzania ilipopata Uhuru miaka ya 1961 na katika miaka ya 1970, maana au *definition* ya maneno ujinga (*ignorance*), maradhi na umaskini pengine ilikuwa tofauti na ilivyo sasa. Ujinga ulielezwa kama kutojua kusoma, kuhesabu na kuandika, maradhi kama ugonjwa ambao ungeweza kutibika na umaskini ulielezwa kwa maana ya umaskini wa kutokuwa na fedha au kipato.

Lakini ni dhahiri kuwa kuna mabadiliko katika maana ya maneno au dhana hizo (ujinga, maradhi na umaskini) kufuatana na mahitaji ya dunia ya sasa. Katika maana ya sasa mtu kwa mfano anayejua kusoma na kuandika na kupiga chapa kwa *Typewriter* tu, sasa hivi ni mjinga kama hajui kutumia kompyuta katika masuala hayo ya kompyuta na hawezi kuajiriwa mara moja katika kazi ya kupiga chapa mpaka ajifunze kompyuta.

Katika maana ya sasa mtu mwenye ng’ombe mia moja ambaye hatumii umeme, hajui kutumia *internet*, hana na wala hajui kutumia simu anahesabiwa kama ni mtu maskini.

Kwa maana ya sasa, mtu yeyote ambaye hana malaria, hakurogwa kama kurogwa kupo, nakumbuka katika Biblia Mtume Paul kwa Wakoritho aliwauliza, ni nani amewaroga ninyi? Wala hakulazwa lakini ana virusi vya Ukimwi huyu ana maradhi. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, nchi yoyote ile duniani hata kama ina wakulima wengi na ardhi kubwa yenye rutuba, ina dhahabu, almasi na mafuta, kama nchi hiyo haikuendeleza Sayansi na Teknolojia, nchi hiyo ni maskini tu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wataalam waliopanga *alphabet* za lugha ya Kiingereza kuanzia A mpaka Z; na A ikiwa nafasi ya kwanza, B nafasi ya pili, C nafasi ya tatu na Z ikiwa nafasi ya ishirini na sita. Walifanya hivyo kwa kuhesabu idadi ya mara za kutokea (*frequency of occurrence*) kwa herufi hizo katika maandishi yoyote katika lugha hiyo ya Kiingereza. Kwa mfano huo, ili kujua dhamira na utashi wa kisiasa wa Serikali na jamii yoyote juu ya shughuli au jambo lolote, utahesabu idadi ya mara za kutamkwa kwa

shughuli au jambo hilo. Kwa mfano hapa Tanzania ni mara ngapi viongozi wanatamka Ubinafsishaji, Ukimwi, Sera za Chama cha Mapinduzi, Vyama vya Upinzani, Tanzania kusamehewa Madeni, wawekezaji kutoka nje ya nchi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa msisitizo huo ni semina, makongamano, warsha na safari nje ya nchi ngapi kwa ajili ya kueneza propaganda juu ya umuhimu wa hayo yaliyotajwa hapo juu? (Makofi)

Vile vile mtu angependa kujua ni mabilioni ya fedha kiasi gani yametumika katika kueneza propaganda za umuhimu wa mambo hayo.

Mheshimiwa Spika, aidha, mtu atapenda kujua kwa upande mwingine, ni mara ngapi viongozi na wananchi wametamka matumizi ya Sayansi na Teknolojia, Maendeleo ya Uchumi wa Taifa yatategemea, Uwekezaji katika Sayansi na Teknolojia. Tunawakaribisha wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kuwekeza katika Taasisi na Vituo vya Utafiti katika Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Spika, katika hayo hapo juu ni semina, makongamano, warsha na safari nje ya nchi ngapi kwa ajili ya kueneza propaganda juu ya umuhimu wa hayo yaliyotajwa hapo juu katika maendeleo ya uchumi wa Taifa? (Makofi)

Vile vile mtu angependa kujua ni mabilioni ya fedha kiasi gani yametumika katika kueneza propaganda za umuhimu wa kuwekeza katika maeneo yaliyotajwa hapo juu?

Mheshimiwa Spika, ujuzi unaotokana na Sayansi na Teknolojia ndiyo raslimali na engine ya kuendesha uchumi wa kisasa kwa ajili ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Hapa nitatoa mifano michache.

Kwa mfano, Teknolojia ya Kompyuta katika *Hardware* na *Software* ndiyo inayoshikilia nafasi ya pili katika kuchangia uchumi wa Marekani. Huko Israel mchango wa Teknolojia ya hali ya Juu (*High-Tech*) inatoa zaidi ya 50% ya Pato la Taifa. Huko Taiwan nchi yenye watu milioni 22 kwa mfano mchango wa kilimo katika pato la Taifa ni 3% na matumizi ya ujuzi wa Sayansi na Teknolojia unachangia 97%; na hapa Taiwan *export* yake inaipatia nchi hiyo dola bilioni 112 na ina *import* bidhaa ya dola bilioni 98 za Kimarekani. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kutokana na takwimu hizo hapo juu ni dhahiri kuwa, Kambi ya Upinzani inashauri Serikali kufanya yafuatayo:-

Kwanza, kuangalia upya Sera ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia ili kupanua upeo wake, kufanya utafiti na kuandaa mpango kamambe (*Master Plan*) wa miaka 10 wa jinsi ya kukuza Sayansi na Teknolojia hapa nchini. Lazima hapa tukiri kuwa uko mpango ambao umekwishaandaliwa kwa sababu ya mwaka 2003 mpaka 2018 lakini unaweza kuboreshwa zaidi na bahati mbaya hata sisi Wabunge hatujaupata na sijui kama kuna mtu anajua upo lakini nadhani baadaye tutajua na Serikali iunde chombo cha Kitaifa kitakachofanya utafiti na kutoa ushauri kwa Serikali kila mara wa jinsi ya kuunganisha nguvu za wadau wote katika matumizi na maendeleo ya Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Spika, chombo hicho kitakachounganisha Vyuo Vikuu na Taasisi za Utafiti, wagunduzi na wavumbuzi binafsi, wenye viwanda, mashirika na makampuni ya biashara na huduma, Serikali na sekta binafsi ili wote hawa waweze kufanya yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, awali kutafuta njia za kupashana taarifa, kutafuta vyanzo vya fedha za kuendeleza Sayansi na Teknolojia, kuhimiza kasi ya kuunda na kuzalisha ujuzi mpya (*new knowledge*) katika nchi yetu, kuweka mikakati ya kuanzisha na kuendeleza juhudi za kukuza *biotechnology* nchini, Serikali iunde Mfuko wa Maendeleo ya Sayansi na Teknolojia na kuanzishwe jarida litakalokuwa likitoa taarifa za matokeo ya utafiti uliofanywa na wagunduzi ama wavumbuzi wa Tanzania tangu uhuru hadi leo na kuendelea. (Makofi)

Pia kuwepo na mkutano wa kila mwaka wa wadau wote katika masuala ya Sayansi na Teknolojia ambao Mwenyekiti wake tungependekeza lazima awe Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili kuendeleza kwa kasi matumizi ya Sayansi na Teknolojia na Elimu ya Ufundi, tunapendekeza kila Wilaya ya Tanzania iwe na Chuo cha *VETA* na Mitaala ya Vyuo hivyo ipangwe kulingana na mahitaji halisi ya eneo hilo pamoja na mambo mengine ya ujumla.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaiomba Serikali ilete Muswada wa Sheria hapa Bungeni kwa minajili ya kutunga Sheria ya kuanzisha Mfuko wa Taifa wa Maendeleo ya Sayansi na Teknolojia na Serikali ikubali kutumia 2% ya pato la Taifa kwenye mfuko huo. *(Makofi)*

Pili, makampuni yote yanayofanya biashara hapa Tanzania katika sekta za viwanda, madini, utalii, simu, Mabenki na kadhalika wakubali na waelimishwe kutoa 2% ya faida ya makampuni yao kwenye mfuko huo kwani wao ndiyo wanaotumia sana sana wahitimu kutoka Vyuo vya Elimu ya Juu na ndiyo wanaotumia matokeo ya utafiti kutoka Taasisi hizo na Vyuo hivyo katika viwanda, makampuni na mashirika yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatu, Kambi ya Upinzani inaiomba Serikali ianzishe mjadala mara moja kuhusu hoja ya umuhimu wa kuendeleza Sayansi na Teknolojia kama ilivyo kwa mjadala katika masuala mengine niliyoyataja na vie vile jinsi ya kupata raslimali (*resources*) za kuendeleza kwa kasi ya haraka matumizi ya sayansi na teknolojia nchini.

Mheshimiwa Spika, ni matumaini yetu Kambi ya Upinzani, kuwa Serikali itayachukulia maoni yaliyotolewa kwa uzito unaostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MHE. REMIDIUS E. KISSASSI: Mheshimiwa Spika, naomba kukushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kwanza ya kuchangia katika Wizara hii muhimu sana kwa maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri pamoja na watendaji wake wote, kwa kutuletea hotuba hii ya ya Bajeti ya Wizara yao ambayo kwa kweli imefanyiwa kazi nzuri. Ni matumaini yetu kuwa utekelezaji wake na hasa ule mpango kamambe kwa kuboresha sayansi na teknolojia, basi utasaidia sana kuharakisha maendeleo katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, kwa kuwa leo ni mara yangu ya kwanza kusimama tangu Bunge hili la Bajeti lianze, napenda kuwapongeza Mheshimiwa Wabunge wote walioingia katika Bunge lako Tukufu kutokana na chaguzi ndogo zilizofanyika 18 Mei, 2003. Ninawatakia kila kheri na tunawakaribisha hapa ili tuungane pamoja katika kuchangia nguvu ili kuweza kuijenga nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla sijasahau basi na mimi napenda kusema kuwa naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, umuhimu wa sayansi na teknolojia na umuhimu wa kuwa na Vyuo Vikuu vingi katika nchi yoyote ile haina haja ya kurudia rudia. Isipokuwa napenda kusema kuwa, ni vizuri basi nchi ikatambua umuhimu wa kuvitumia vile vyuo kwa manufaa yake. Hivi Vyuo Vikuu vinatumika zaidi siyo kutoa tu wanafunzi lakini zaidi katika tafiti. Tafiti ambazo zinasaidia sana kuendeleza uchumi na maendeleo ya jamii.

Kwa hiyo, napenda kutoa wito kwa Wizara, Idara, mashirika na asasi za binafsi kutumia vyuo hivi katika kupanga mipango yao ili siyo tu kuwasaidia kuleta maendeleo yao na kuwa na mipango ambayo ni endelevu iliyofanyiwa utafiti mzuri lakini vile vile kusaidia kuongeza mapato ya hivi vyuo ili viweze kujiendesha.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi utaona *tendency* ni kutumia zaidi wataalam kutoka nje ya nchi. Hili kwa upande mmoja ni zuri kwa kuwa tunaongeza *technology transfer* lakini kwa kweli ni vizuri

tukawatumia wazalendo wetu kama *lead partners* katika kufanya tafiti ndani ya nchi yetu. Hawa ni watu ambao wana uchungu na nchi hii na wanajua mahitaji halisi ya nchi.

Kwa hiyo, kama tutawatumia kama *lead partners* katika miradi yoyote, wao ni wepesi kujua labda kama kunahitajika taaluma yoyote mpya ambayo haipo hapa nchini kuwa wataipata wapi. Wao wanakuwa *responsible* na wanakuwa *accountable*. Kwa hiyo, bado nasisitiza kuwa tuvitumie vyuo vyetu hivi na asasi zetu hizi katika kutuletea maendeleo yetu ndani ya nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pili, naomba kupendekeza pia kwamba Serikali kwa makusudi ivitumie hivyo vyuo vyetu kama *think tank* kwa ajili ya maeneo mbalimbali, sekta mbalimbali ili kupata *alternative opinion* katika kutekeleza miradi na programu muhimu za kuendesha miradi ya nchi hii.

Mheshimiwa Spika, suala lingine muhimu ninaloliona ni tatizo la wanataaluma hawa kuvunjika moyo, wengi wanavunjika moyo kwa sababu wanahisi hawapati maslahi stahiki, maprofesa na madaktari walioboea utakuta mishahara yao ni duni na marupurupu ni kidogo. Sasa wapo wale ambao wanapata *option* za kwenda nchi nyingine ili kwenda kufanya kazi lakini pia wale wengi ambao wanabakia hapa, napenda kuiomba Serikali kwa makusudi kabisa ifanye utaratibu ili mishahara yao iongezwe maradufu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mfano mzuri ni katika hili *book* la matumizi, *Volume II* katika ule ukurasa wa *XIV*. Ukiangalia *Vote* ya Wizara hii ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, *Vote* Na. 68, utaona mishahara yote ni shilingi milioni 642 na ushehe hivi na hii ni Wizara ambayo ina wataalam na Vyuo Vikuu vingi. Ukiangalia asasi kama Redio Tanzania, inapata mishahara yake karibu milioni 500 na kitu. Sasa sitarajii kuwa Vyuo Vikuu vyetu vyote hivi pamoja na asasi zake zote basi iwe na wataalam *almost* wanaolingana na redio Tanzania. Lakini ina maana wataalam hawa katika Vyuo Vikuu wanapata mishahara midogo na asasi nyingine ambazo ziko katika Mawizara zinapata mishahara mizuri na hiyo vile vile pengine ndiyo sababu ambayo inawafanya wakufunzi wengi wanakimbia katika vyuo hivi na kuweza kupenya katika Mawizara mengine. Sasa ili tuweze kuwa-retain kuna haja ya kuongeza mishahara yao na mafao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo ningependa kuchangia ni suala la Chuo Kikuu Huria. Mimi ni *Part time Lecturer* pale na ninaona tuna matatizo mengi. Chuo hiki kimeanzishwa kwa nia nzuri sana ya kuwapatia Watanzania elimu hasa wale ambao hawakuipata katika mikondo ya kawaida. Lakini tumekianzisha bila mtaji wowote na kimeendelea kutoa huduma, kimetumia Ofisi za kupanga na sasa hivi wamejaribu kununua Ofisi kwa mikopo. Tatizo ni kuwa bado na hata kwenye Bajeti hii nimeona fedha walizopewa kwa kazi za maendeleo ni kidogo sana, wamepewa shilingi milioni 50 tu. Kwa kweli kutokana na utaratibu na mambo ambayo wamejipanga ni kwamba shilingi milioni 50 ni kidogo sana. Ningependa kuiomba Wizara hii iangalie na Serikali kwa ujumla iangalie angalau kwa uchache basi wapate shilingi milioni 200 ili waweze kukiimarisha na kujiimarisha wenyewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa hivi nimeelezwa kuwa wanafunzi wanaochukua masomo ya sayansi nusura wafukuzwe kwa sababu wamekosa fedha za kuchangia katika *practical*. Walimu wengi wa *part-time* mimi nikiwa mmojawapo tunaendelea kukopeshwa au kukopwa na chuo hiki kwa huduma tunazozitoa. Sasa nafikiri kwa *spirit* ya kuimarisha hicho chuo na kuwapatia Watanzania wengi elimu, ni vizuri basi Serikali ikajitahidi angalau kwenye masuala haya ya mishahara na marupurupu, basi wapewe walimu ili waongeze bidii na wapatikane wasomi wengi zaidi.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo ningependa kuchangia ni suala la Chuo cha *Marine Science* ambacho kipo Zanzibar. Kwa kweli napenda kuipongeza Serikali ya Muungano pamoja na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kwa kufikia mahali kuwa sasa wameamua chuo hiki kitajengwa katika eneo la Buyu na ambalo kwa bahati limo ndani ya Jimbo langu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ujenzi unatarajiwa utaanza wakati wowote mwaka huu, naona pesa kidogo zimetengwa, shilingi milioni mia mbili na nusu, pengine kwa kuanzia kusafisha viwanja na kuweka misingi, si mbaya. Lakini tatizo nililoliona ni suala la *compensation*. Fedha ambazo zilitengwa kwa ajili ya

kuwalipa fidia wananchi wale ambao sasa hivi wameacha kuyatumia maeneo yao yale kwa kilimo, hawajalipwa na walikuwa walipwe tangu Januari, sasa karibu unaingia mwezi wa nane.

Sasa mimi wasiwasi wangu ni kuwa itabidi ile fidia iongezeke kama hawatolipwa kwa muda na wao kwa bahati mbaya kilio chao kikubwa ni kuwa sasa hivi hawajalima tena kwa kuwa walijua tayari walikuwa wahame ili wakaanze makazi yao mapya. Namwomba Mheshimiwa Waziri akisikilize hiki kilio cha wananchi wa Buyu walipwe haraka haki yao ili wakaanze shughuli zao za maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya la mwisho ni suala la mfuko wa kusaidia kukopesha, kuwakopesha vijana ili waweze kujielimisha. Mfuko huu ni mzuri na ninapenda kuipongeza sana Serikali kwa kuanzisha huu mfuko. Naomba kama walivyosema wenzangu, Kamati ile ya Huduma za Jamii, kuwa ni vizuri na wadau wengine wakachangia kwenye mfuko huu kwa sababu wengi wanafaidika na mfuko huu. Kutokana na wanafunzi ambao watatoka kule chuoni, basi ni vizuri vile vile wachangie angalau asilimia fulani ya faida katika biashara zao ili tuwapate wananchi wengi zaidi, vijana wetu wapate kuendelea na masomo katika ngazi za juu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo na mimi napenda kusema kuwa naiunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

MHE. BERNARD K. MEMBE: Mheshimiwa Spika, naomba awali ya yote na mimi niungane na wenzangu waliotangulia kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, Mheshimiwa Naibu Waziri wake pamoja na Kamati, kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kutuletea hotuba hii na nischeleweshe kusema naiunga mkono hotuba hii moja kwa moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimeyagawa mazungumzo yangu kwenye vifungu viwili tu, nayo ni elimu ya juu pamoja na sayansi na teknolojia. Kwa upande wa elimu ya juu ni ushauri tu.

Mheshimiwa Spika, ni kweli Taifa linahitaji kuwa na Vyuo Vikuu vingi vya kutosha. Katika nchi kama ya kwetu na pia kwa mfano Canada yenye watu milioni 30 kama Tanzania ina Vyuo Vikuu 200 na intake ya wanafunzi ni kubwa mno zaidi ya 560,000, linganisha na Vyuo Vikuu vya Kenya na Uganda ambavyo na vyenyewe vimetuzidi, sisi bado tuna Vyuo Vikuu vichache na wanafunzi wanaoingia kwenye Vyuo Vikuu hivyo ni wachache sana. Kwa vyovyote vile tutahitaji kupanua wigo wa kuwa na Vyuo Vikuu vingi.

Mheshimiwa Spika, lakini hatari ninayoiona ni kwamba tusipoangalia tutajikuta tunavunja Vyuo vya kati, *Professional Institutes* na kuvifufusha viwe Vyuo Vikuu. Sasa hii ni hatari na nitairudia tena. Kuongeza Vyuo Vikuu ni vizuri lakini msivunje *Professional Institutes* ambazo ndizo zinazotengeneza kada ya *professionals* ya mafundi, watu ambao kwa kweli wanafanya kazi nzuri zaidi katika uzalishaji na maeneo mengine yote.

Sasa isiwe mbadala yaani hatuui hizi *Institutes* kama *IDM, IFM, College of Business Education* au Mbeya *Institute of Technology* msembe kesho na kesho kutwa hivi tunakusudia viwe Vyuo Vikuu, *that is suicide*, huui vile. Hatuwezi kuwa na nchi ambayo tuna vijana wanaosoma vizuri halafu baadaye wanakwenda tu *University* kwa sababu kule ni *academics*.

Mheshimiwa Spika, lakini *VETA* au hizi *Colleges* ndizo kwa kweli zinazotakiwa ziende sambamba na *higher education* na ratio yenyewe ni hiyo ya *one, five, thirty five* kwamba unakuwa na mtaalam mmoja kutoka Chuo Kikuu halafu awe na mafundi watano kutoka *Colleges* yaani *Institutes of higher learning* halafu awe na *thirty five* mafundi mchundo, wale wengine wale.

Sasa tusipofuata hivyo tukisema kwamba *Institute* hii mbele ya safari iwe Chuo Kikuu tunaua kada ya katikati na nchi hii tutakuwa tumejiharibia uwezo wetu wa kupanua siyo elimu peke yake lakini pamoja na sayansi na teknolojia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nije kwenye sayansi na teknolojia, nilizungumza mwaka jana na somo hili napenda sana nilizungumze tena mwaka huu.

Mimi ni miongoni mwa watu wengi duniani tunaoamini kwamba sayansi na teknolojia ndiyo msingi kamambe wa maendeleo kwa nchi zote duniani, naomba tena nitamke kwamba sayansi na teknolojia ndiyo msingi mkubwa wa maendeleo ukiacha *infrastructure*, ukiacha raslimali na ukiacha *good leadership*.

Mheshimiwa Spika, siku zote hizi na sijui kwa nini haiingii hii, siku zote hizi tunapozungumza lazima tujue kwamba ili tuendeleo tunahitaji elimu ya sayansi itakayotueleza na kutupata picha halisi ya dunia tunayoishi, kwenye sakafu ya dunia yetu na ndani ya ardhi yetu kuna kitu gani, hiyo ni elimu ya sayansi. Tukigundua huko chini kuna madini, petroli au gesi kama sayansi inatupeleka hivyo lazima tu-*develop technology*. *Technology* ni *means* ya kufikia hiyo *scientific discovery* uliyoipata kule. Ni kitu kimoja kizuri kweli kwamba unakuwa na *science* halafu unakuwa na *technology*. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, hizi *Science and Technology* zimegawanyika katika makundi mawili. Kundi la kwanza ni *Foreign Technology* yaani teknolojia za nje kwamba wenzetu wame-*invest* yaani wenzetu wameishaifanya kazi hiyo sisi huku tuna *introduce*, tuna *absorb* na tuna *apply*, tunaichukua, tunaiweka kichwani mwetu na tunaitumia kama chombo hiki ninachokitumia sasa hivi, ni *product* ya *Foreign Technology*. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nchi zote zinazoendelea ndiyo *stage* yao ya kwanza ya kutumia *science and technology* ilivyofanyika kwamba mwenzako amekufanyia kazi wewe una *introduce*, una *absorb* na kisha unai-*apply*, ndicho tunachokifanya katika nchi zetu. Lakini nchi ambayo ipo *serious* katika maendeleo lazima tu-*shift* sasa, mkishafika hiyo *stage one* ya *science and technology* lazima sasa m-*shift* katika *ku-invest research and development*. Sasa ndiyo suala la *investment* kwenye RND linavyofika yaani lazima ku-*invest* sasa kwenye *research and development*.

Mheshimiwa Spika, tunaposema *research and development* ina maana ya *scientific research and technological development*, ni maneno yamejificha pale, ni vizuri tukayachambua hayo. *Scientific research and technological development* kwamba tunayo *challenge* katika jumuiya ya Watanzania na siyo kwa *higher education* peke yake.

Mheshimiwa Spika, suala la *science and technology* si *monopoly* ya *higher education* peke yake, kuna *basic sciences* hata kule kwenye shule za msingi, shule za sekondari, *high schools* na *colleges* na *Universities*, hizi bado zinaweza zikafundishwa *basic sciences*, wakajifunza utafiti wa *science* na hata kujifunza *technological development* katika *levels* zote ili kuipa uwezo nchi yetu ya kuendelea katika *fields* hizo.

Mheshimiwa Spika, sasa tunapofika kwenye *scientific research* na *technological development* lazima tu-*focus* dira, nia yetu tufanye nini, tuendeleze kitu gani?

Mheshimiwa Spika, kwa vyovyote vile tutakubaliana kwamba tunapofanya *science* zote hizi dunia nzima inakuwa na malengo makubwa manne, sisi nadhani ni matatu. Dunia inapofanya *research*, inapo-*invest* kwenye *research* na *science* wanataka kwanza kabisa kudumisha na kutanua *biotechnology*, kilimo kwa mfano, kitahitaji mbolea siyo ya ng'ombe tu, *sulphur* zinazotumika hizi, ni *product* ya *scientific research* na *technological development*.

Lakini pili ipo *environmental technology* kwamba, ili kutunza mzingira yetu vizuri, tunahitaji *technology* ya mazingira, inayoweza kutusaidia kutunza mazingira zaidi. Tatu, *information technology* kwamba ili kuifanya *globalization* iwe *realistic* na dunia nzima tujikute kama kijiji kimoja upande wa *information* lazima uende, hiyo ndiyo inaitwa *information technology*. Lakini ya nne ya hatari ambayo wakubwa hawataki tu-*develop* ni *nuclear science and technology*, sasa si ya kupigana tu lakini pia kwa *energy*. Siku moja dada yangu Mheshimiwa Anne Makinda, alisema ukifika kwenye *cancer centers* kama *Ocean Road*, pale chini pana madini ya *uranium* ambapo ukiya-*misuse* yanaweza kuwa hatari. *CT-Scan* na uchunguzi mwingi sana wa ile *cancer center* unategemea madini ya *uranium* ili kufanya kazi hiyo. Lakini pia katika ku-*generate hydroelectricity uranium/nuclear* inatumika lakini wakubwa hawataki tuitumie kwa

sababu ikituingia sana vichwani tunaweza tukaipeleka kwenye Majeshi wakafanya vitu vyao kule tukapata matatizo. Lakini hayo ndio maeneo manne ya sayansi na teknolojia.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa sayansi na teknolojia, napenda kutoa changamoto moja kwamba, ili nchi yetu iweze kufanikiwa katika sayansi na teknolojia, tunahitaji *energy*. Ukiwa na sayansi na teknolojia *in place* lakini huna umeme kwa mfano, nilipata msaada wa *computers* kwa ajili ya shule zangu lakini kwa sababu Jimbo langu la Mtama halina umeme, *computers* ni *irrelevant*, haziwezi kutumika. Kwa hiyo, kumbe ili sayansi na teknolojia ifanye kazi yake vizuri lazima ivae kiatu chake cha pili au soksi yake ambayo ni *energy*. Tunapozungumzia *energy* lazima tuwe na *alternative energy source* kwamba pale tunapona umeme haupo basi *solar energy* ipate *emphasis*.

Mheshimiwa Spika, tunapolia kilio cha umeme kwa sisi watu wa pembezoni ambao hatuna *energy* hiyo kwa sasa, hivi kuna ubaya gani wa ku-*invest* kwenye *research and development* ya kuona kama inawezekana kuvipatia *solar energy* Vijiji, Tarafa na Kata ambapo hawana umeme? Sio tu itatusaidia kupika na ku-*serve environment*, lakini teknolojia hii ambayo tunai-*introduce* ku-*absolve* na *apply* kama ya *computer* na vyombo vingine ambavyo vinahitaji sayansi na teknolojia kwa vyovyote vile vingetusaidia sana hadi pale tutakaposubiri sisi watu wa Lindi, Mradi wa Songosongo wa *gas electricity* utuletee umeme unaoaminika katika Mikoa ya Lindi, Mtwara na Ruvuma. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naomba *efforts* zitumike kuona wapi na namna gani tunaweza kutumia nguvu za jua kuleta umeme, nguvu za upepo kuleta umeme wa kusukuma maji yetu, kuleta maendeleo yetu katika sehemu tunazotoka. Hiyo ndio changamoto ya sayansi na teknolojia. Tuwe na wataalam, utukutu, jeuri ya kujaribu kufanya uvumbuzi wa kupata *energy*. Ukiwa na *energy, application* ya sayansi na teknolojia inakwenda vizuri zaidi. Kwenye Mikoa ile ambayo hatuna sayansi na teknolojia kwa sababu ya ukosefu wa nguvu hizo za umeme, naomba tufanye jitihada za makusudi za kutumia *solar energy*.

Mheshimiwa Spika, Wajerumani wako katika hali nzuri, *Canadians* wako katika hali nzuri na utaalam mzuri sana wa kuleta *solar energy*, sioni sababu kwa nini tusitenge fedha kujaribu kupanua wigo wa *alternative energy sources* katika nchi yetu kwa kutumia jua ambalo wenzetu huko nje hawalioni na kama wanaliona ni saa chache na sisi hapa tunalo *cash* saa kumi na mbili? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, napenda nimalizie kwa kurudia kusema kwamba, nchi za wenzetu wanakuwa na Wizara moja tu ya *Science and Technology*, hawachanganyi na *education* mbele ya safari, naamini hilo ndilo litakalokuwepo ili tu-*concentrate* katika msingi huu wa maendeleo. Halafu baadaye tunakuwa na *Tanzania Institute of Technology*, ambayo ita-*deal* na mambo ya *Institute* tu. Tatu mnakuwa na kitu kama *Presidential Advisory Council* ya Sayansi na Teknolojia, itakayokuwa na *overall coordination* sasa ya masuala yote ya sayansi na teknolojia katika nchi yetu. Tukifika hapo tutakuwa tumeipa sayansi na teknolojia kipaumbele kinachostahili na kwa kweli ndio itakuwa hasa msingi wa maendeleo ya nchi yetu itakayo-*support infrastructure* kama msingi mwingine wa pili.

Mheshimiwa Spika, kwa maneno hayo, napenda kuwapongeza Mawaziri kwa kazi nzuri na ni matumaini yangu kwamba, mambo haya yatafanikiwa na naunga mkono mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja kwa mia moja. (Makofi)

MHE. BERNADINE R. NDABOINE: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia Wizara hii ya Sayansi na Teknolojia. Kwanza kabisa, napenda kumpongeza Waziri kwa hotuba yake nzuri, yenye mwelekeo wa kuleta maendeleo katika nchi yetu. Vile vile napenda nimpongeze Naibu Waziri, pamoja na wataalam wake, ambao wamesaidiana kuleta hotuba hii Bungeni.

Mheshimiwa Spika, katika kuendeleza pongezi zangu, naomba nimpongeze Waziri na Wizara yake, hasa kwa kuongeza namba ya wanafunzi ambao wanajiunga na Vyuo Vikuu vya Sayansi hapa nchini. Katika Chuo Kikuu cha Sayansi ya Tiba, namba imeongezwa lakini naomba Chuo hiki kizidi kupokea wanafunzi wa kike kwa sababu asilimia 29.6 ambayo imetajwa ni ndogo mno tukizingatia kwamba, Waganga hasa wanawake wanakuwa karibu sana na wagonjwa na ndio wanaofaa kuwasikiliza na kuwahudumia wagonjwa. Kwa hiyo, nashauri sana namba ya wanawake ambao wanajiunga na Chuo Kikuu

cha Tiba, iweze kuongezwa angalau ifikie asilimia 50 kwa 50 kama alivyotaja kwa sababu mwaka 2006 ni mbali sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile napenda kuipongeza Wizara kwa kufikiria kuunda chombo cha kutoa mikopo na kurejesha mikopo kwa wanachuo. Hii itasaidia sana kwa wanafunzi wanaotokana na familia maskini, ambao wana uwezo lakini wanashindwa kujiunga na Vyuo Vikuu na hivyo tunakuwa tumepoteza utaalam wa watoto hao.

Mheshimiwa Spika, vile vile napongeza kwa kupunguza gharama za Chuo Kikuu kutoka shilingi milioni tano ambazo walikuwa wanalipa, kuanzia shilingi laki sita mpaka shilingi milioni moja, hili ni punguzo kubwa sana tunaishukuru Wizara. Vile vile tunaomba izidi kuangalia watoto maskini ambao hata hizo shilingi laki sita hawawezi kupata. Kwa hiyo, katika kutoa mikopo watoto hawa wafikiriwe kwanza kwa sababu kuna watoto ambao wana uwezo wa kulipa kiasi hicho lakini watoto wa maskini ni vigumu kupata hizo shilingi laki sita kujiendeleza kimasomo pia ni vigumu kupata wafadhili wa kuwadhimini kupata pesa hizo. Kwa hiyo, nashauri Wizara izidi kuangalia watoto wenye vipaji vya sayansi wafikiriwe kuondolewa gharama hizi hasa watoto wa kike kama nilivyosema.

Mheshimiwa Spika, tafiti ni muhimu sana na mtu anayetaka kufanya utafiti ni mtu ambaye anapaswa atulie na aridhike. Mara nyingi watu hawa wanaofanya tafiti wanapaswa wawe na sehemu nzuri ya kufanyia tafiti zao. Nashauri katika tafiti kuwe na maabara maalum ambapo tafiti hizi zinazohitaji utulivu, watafiti waweze kukaa, kutulia na ninaposema kutulia ni kwamba wasiwe na mawazo mengine ya kutafuta maslahi ya kuwawezesha kuendesha maisha yao, maabara hizi zivasaidie kupata huduma za kila siku ambazo wanahitaji, mtafiti asikae anafikiria nitakula nini, nitatoa wapi pesa za kuwasomesha watoto wangu, yeye akae akifikiria tafiti na namna gani anaweza kuendeleza tafiti zake. Nashauri maabara hiyo iwepo ambayo itawasaidia watafiti kutulia na wapewe vitendea kazi kusudi waweze kufanya kazi zao bila wasiwasi na kwa utulivu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika tafiti nashukuru kwamba tafiti nyingi zimefanywa na Wizara iko katika harakati za kufanya tafiti mbalimbali zikiwemo tafiti za kutumia mionzi, nishati lakini katika tafiti hizo basi nashauri hapa nchini tulipokwenda Iringa tumekuta kuna vumbi la mbao, ambalo linaweza kusaidia kutengeneza nishati ambayo ingeweza kuwasaidia akina mama katika kupunguza uharibifu wa misitu. Naomba vumbi hili lifanyiwe utafiti ni namna gani linaweza kutumika kama nishati rahisi. Hili likifanikiwa litasaidia katika kupunguza uharibifu wa mazingira na vile vile litasaidia akina mama ambao wanaharibu misitu kutulia nyumbani na kufanya kazi zao vizuri.

Mheshimiwa Spika, wataalam wetu kwa kukosa fedha za kutosha, mara nyingi wanakimbilia nchi nyingine na wakikimbilia nchi nyingine, katika taaluma zao tunaajiri wataalam kutoka nje ambao tunawalipa pesa nyingi sana. Nashauri Wizara iangalie ni namna gani tunaweza kuwasaidia wataalam wetu waweze kukaa hapa nchini. Nashauri kiwepo kitengo au benki ya wataalam ambapo hawa wataalam wetu watapatikana. Mara nyingi unakuta kuna wataalam wanamaliza Chuo lakini hawapati ajira wanapaswa wenyewe watoke ofisi moja hadi nyingine na ikishindikana ndio wakati mwingine ndio wanakwenda nje. Lakini kungekuwa na sehemu ambayo wanaripoti wanajulikana na wote wanaohitaji wataalam waende katika Ofisi hii kutafuta wataalam hao, ingekuwa ni rahisi kuwatafutia ajira. Vile vile tungekuwa na wataalam wa kutosha nchini kuliko kukimbilia nchi nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna watafiti ambao wametoa utafiti, wamepata vifaa ambavyo vinaweza kusaidia katika nchi yetu lakini kutokana na kuwa hawajulikani au hawapati tuzo, wanabaki na tafiti zao ambazo hazisaidii nchi. Ninao mfano, kuna kijana hapa nchini aligundua mashine ya kutengeneza maji ambayo yanatumika katika maabara na vile vile amegundua mashine ambapo anaweza kutengeneza vifaa vya maabara. Bahati mbaya kijana huyu hakupata tuzo yake na licha ya kwamba hakupata tuzo, hakusaidiwa kuendeleza taaluma yake angalau akaweza kujiajiri. Nashauri hawa watafiti wanapokuwa wamegundua vifaa wasaidiwe kuendeleza taaluma zao kusudi tusinunue vifaa kutoka nje wakati wataalam wetu wapo na wanaweza kuvitengeneza humu humu nchini. Kwa hiyo, nashauri wapewe mikopo na ijulikane wataipata wapi kuliko kurandaranda na mikopo hii iwe ya masharti nafuu. Unamwambia kijana aliyetoka Chuo Kikuu awe na dhamana ya nyumba ataitoa wapi? Hawezi kuipata nadhani dhamana yake

ingekuwa ni utalam wake, apewe mkopo atengeneze vifaa vinavyohitajika na akiuza ndio aweze kulipa mkopo wa namna hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika tafiti za magonjwa au madawa kuna tafiti za madawa ya kienyeji ambazo zinafanyika lakini tunao Waganga wengi wa kienyeji ambao wako vijijini, nashauri wataalam waweze kuwafikia kwa sababu wanazidi kuzeeka, watakufa na utalam wao tutakuwa tumeukosa. Nashauri tafiti ziende mpaka vijijini na huko ndio kuna Waganga wa kienyeji ambao wana dawa zinazotibu magonjwa mfano kansa, kuvunjika miguu, malaria na dawa zao hatujazitumia vizuri wanahitaji wasaidiwe. Malipo yao kwa kawaida ni kidogo lakini tukiwatumia wataweza kutusaidia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vile vile tukishawapata hao Waganga wa kienyeji ambao wana dawa ambazo ziko huko vijijini tunahitaji tuhifadhi madawa haya kwa sababu yanapotea, mazingira yanabadilika. Kwa hiyo, nashauri kuwepo na *botanical garden* ambayo itasaidia kuwa na madawa ya kienyeji ambayo yatakuwa yamefanyiwa tafiti kusudi yaweze kutusaidia huko tuendako.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kidogo niongelee watoto wetu ambao wako vyuoni. Mara nyingi katika Vyuoni kunatokea migomo, migomo hii mara nyingi inatokea kwa sababu ya pesa. Pesa wanazopewa kwa ajili ya matumizi pale Chuoni, kununulia vitabu, kwenda *field*, hazitoshi na ingawa hazitoshi wakati mwingine hazitolewi kwa wakati muafaka. Kwa hiyo, watoto wanahangaika na kwa kuwa bado akili zao hazijakomaa vizuri, wanaanzisha migomo. Kuanzisha migomo sio jambo la busara lakini tunapaswa kuangalia kwa nini migomo hii inatokea. Kuna Kamati na Bodi za Vyuoni kwa hiyo zifanye juhudi za makusudi za mara kwa mara kukutana na uongozi wa Vyuoni au na wanachuo wenyewe, kuona matatizo ambayo yanakuwepo kusudi tupunguze migomo hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja ya Wizara hii na nampongeza Mheshimiwa Waziri na wataalam wake kwa hotuba nzuri. (*Makofi*)

MHE. DR. HAJI MWITA HAJI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii ili nami nitoe mchango wangu kidogo katika hoja iliyo mbele yetu ya Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli nimefarijika sana kutokana na Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, pamoja na viongozi mbalimbali wa Wizara hii, kwa jinsi walivyoitayarisha hotuba hii kwa juhudi, maarifa, ufupi na kueleweka hadi kufikia leo ikaletwa mbele yetu kuijadili. Sio kuijadili *as such*, lakini kuijadili ni katika kuona tu vipengele fulani fulani ambavyo kwa fikra zangu, ningeomba kidogo kuvitilia mkazo ili kuiboresha hotuba hii hasa tukizingatia kwamba, nilikuwa mmoja wa Wajumbe ambao tulishirikiana katika kuipitia hotuba hii, pamoja na maelekezo ya Mheshimiwa Waziri katika Kamati ya Huduma za Jamii.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu wa leo nimeuelekeza katika sehemu mbili, tatu. Kwanza kama tunavyoelewa, taaluma ya sayansi na teknolojia ni taaluma ambayo inahitaji msingi mzuri wa elimu nzuri kuanzia chini mpaka kufikia kiwango cha kwamba sasa hivi tunakuwa *scientists*. Katika Wizara hii ambayo tunaita Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, imechanganya masuala ya teknolojia, sayansi na elimu ya juu. Lakini tunapozingatia taaluma ya elimu ya juu, hebu tufikirie elimu ya juu inanzia wapi, tukishajua elimu ya juu inanzia wapi, nafikiri tutakuwa mahali pazuri pa kuona kwamba, huko kunakoendelea kwa kuweza kuwa na *scientists* na *technologists*, waliokuwa na taaluma tunaweza kufikia pazuri.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii tumeona kidogo imekuwa tofauti lakini tegemeo langu ni kwamba, kuna ushirikiano mkubwa baina ya Wizara ya Elimu na Utamaduni Tanzania Bara, pamoja na Tanzania Zanzibar, ambapo tunasema hizi ni shughuli za Kimuungano. Sasa wakati tunapozingatia suala hili kimsingi ili kuweza kupata ile taaluma ambayo inaweza kutuongoza tukafikia kwenye lengo la sayansi na teknolojia, naona kidogo kuna tofauti ya *syllabus* ya elimu ya sekondari mpaka kufikia *high school*. Je, Wizara hii ina utaratibu gani wa makusudi ambao unaweza kutuongoza katika kuleta mafanikio ya sayansi na teknolojia wakati itakapofikia kiwango cha kufanya hivyo? Ntoa ushauri kwa Wizara hii kuwa na ushirikiano wa dhati kati ya Wizara za Elimu ya Sekondari na *high school* ili kuwa na utaratibu mzuri utakaoweza kutuongoza katika sayansi na teknolojia.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo napenda kuchangia ni kuhusu Vyuo Vikuu. Mheshimiwa Waziri, amekuwa na mipango mizuri ya taaluma ya kuwawezesha vijana wetu ambao wanamaliza *high schools* kuingia Vyuo Vikuu. Katika dira hii na malengo yao, vimetajwa Vyuo ambavyo vinahusika katika kuwaingiza wanafunzi hawa kushiriki katika masomo haya ya juu. Lakini hapa kidogo nataka ufafanuzi na kujua ingawa vimetajwa Vyuo viwili vya Zanzibar, lakini hatukuelewa je katika idadi ya wanafunzi ikiwa suala la elimu ya juu ni suala la Muungano, hivi Vyuo vya Zanzibar vinachangia kiasi gani katika kuboresha au kuongeza idadi ya wahitimu wa Vyuo Vikuu na kupata mwelekeo wa kupata wataalam kufuatana na ushirikiano uliokuwepo kati ya Wizara ya Elimu ya Zanzibar na Wizara ya Elimu ya Tanzania Bara?

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo napenda kuliongezea, kwanza nitumie fursa hii kuipongeza sana Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, kwa uamuzi wake wa makusudi wa kutoa taaluma kwa Viongozi wa Baraza la Wawakilishi wa Zanzibar kuhusiana na suala la mionzi. Natumaini sana kwamba uamuzi huu umetupa faraja na mwelekeo wa jinsi gani tunaweza kushirikiana ipasavyo katika kuona hali halisi ya maendeleo ya shughuli zinazohusiana na mionzi na *atomic* ili kuondoa wasiwasi ulio kati yetu na kuwa na taaluma na mwelekeo sambamba kati ya Tanzania nzima kwa jumla.

Mheshimiwa Spika, kama tunavyoelewa kuenea kwa shughuli za *atomic* ni jambo la muhimu sana katika dunia yetu ya leo na hasa tukizingatia kwamba, shughuli hizi zinapofikiwa, visiwa ambapo kuna mianya mingi ya kuingia vitu mbalimbali, ambavyo vinaweza kutuletea athari, kuwa na sheria ambayo itatumika na kuweza kueleweka vizuri katika sehemu zote za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ni suala la msingi na busara sana ambapo Wizara yetu hii imefikiria na kushirikiana kwa pamoja na kuleta ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na suala hili, sisi ambao tunatoka Zanzibar au katika visiwa vyenye matatizo ya umeme, niipongeze sana Wizara hii kwa kule Zanzibar ambapo kwa makusudi imeweza kutoa taaluma au kuleta wataalam kutoka nchi za nje wakatoa taaluma ya kutumia mionzi katika shule. Mfano mzuri ni shule moja iliyopo katika Jimbo langu inayoitwa Kizimkazi, nimefarijika sana kuona wataalam kutoka Ujerumani wanatoa taaluma hizi za mionzi pamoja na kuiuza *energy* ile kwa wananchi kwa bei nafuu ambapo wenye fursa wanaweza kununua na ikatumika katika sehemu hizi ambazo zinahitaji masuala kama haya. Kwa hiyo, naishauri sana Wizara hii, kujaribu kadri inavyowezekana, kutafuta nyenzo na utaratibu wa sehemu kama hizi za Visiwani kutumia nyenzo hii ili kuleta maendeleo ya sayansi na teknolojia na kuweza kuwaondolea usumbufu kwa kiasi fulani wale wananachi ambao wapo kabisa na suala la kutumia umeme. Kutokana na hali hiyo, nitafurahi sana kama kutakuwa na ushirikiano wa pamoja katika kuenea suala hili sehemu mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo napenda kulizungumzia ni suala la Chuo cha Sayansi za Baharini (Majini), sio majini ya mashetani lakini majini ya kwenye maji ya Zanzibar. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, nimefarijika sana kusikia kwamba, katika maelekezo yaliyopita, Wizara hii ikishirikiana na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, imeshalipa baadhi ya fedha kwa ajili ya kuwalipa fidia watu watakaaoathirika. Katika maelekezo yaliyotolewa na Kamati ya Huduma za Jamii, nimepata taarifa kwamba, wakati huu tunategemea sana kuanza shughuli za ujenzi wa Chuo hicho. Kwa hiyo, nasisitiza kwamba, Wizara isilichukulie suala hili kama ni rahisi, tunalitizama kwa moyo mzuri sana, tukilingojea kwa hamu sana ili kuongeza idadi ya vijana wetu watakaojiunga na taaluma hizi za sayansi za juu na kuleta mafanikio katika nchi yetu hii ya Tanzania.

Mwisho, ningezungumzia kuhusu wataalam ambao wapo Vijijini. Mbali na kuzingatia kwamba Wizara hii inategemea sana au inaangalia sana au imeweza jicho lake sana kuhusu vyuo, lakini kuna vijana ambao hawako vyuoni lakini wana ujuzi. Vijana hawa wameweza kuvumbua wao wenyewe kwa mfano, nimeshuhudia hapa Dodoma kijana ambaye amekuwa na taaluma, ametengeneza mashine ya matangazo, ile ambayo inazunguka kuweza kuleta matangazo mbalimbali kwa kutumia vyombo duni kabisa. Watu kama hawa ningeshauri sana kuwe na utaratibu wa kuweza kuinua vile vipaji vyao na kuwapa taaluma zaidi na mambo kama yale yakachukuliwa kwamba ni uvumbuzi maalum. Hii inaweza kutusaidia katika kuwapunguzia makali ya maisha na wakati ule ule kuweza kutangaza ule utalam wao

ambao tayari vijana hawa wamekuwa nao, ambao ni wa kuzaliwa nao. Ikiwa kama mfano wa kijana kama huyu ambaye yupo hapa hapa Dodoma, pengine wataalam kama wangependa kumwona ningeweza kwenda kuwaonyesha na mimi nilipita tu kienyeji nikamwona na nilivutiwa sana na suala hili. Kwa hiyo, ningeshauri sana Wizara hii mbali na kuweka mkazo wao katika vyuo tu, vile vile tuwe na fursa ya kuwapa nafasi vijana kama hawa ili kuweza kuendeleza utaalum wao.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo machache, ningependa tena niunge mkono hotuba hii kwa asilimia mia kwa mia na kuwatakia kila la kheri na mafanikio katika maisha yote. Ahsante sana. *(Makofi)*

MHE. SULEIMAN A. SADIQ: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipatia nafasi na mimi asubuhi ya leo. Naomba nianze na pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na timu yake yote, kwa hotuba nzuri, yenye mchambuo mzuri na wa kina kwa faida ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kuchangia kwa kukizungumzia Chuo Kikuu cha Mzumbe. Chuo Kikuu cha Mzumbe ni Chuo Kikuu kipya ambacho kilizinduliwa rasmi mwishoni mwa mwaka 2002 na Mheshimiwa Rais wetu, ni Chuo ambacho kipo katika Wilaya mpya ya Mvomero. Lakini naomba nianze na pongezi kwa Uongozi wa Chuo Kikuu cha Mzumbe. Chuo Kikuu cha Mzumbe baada ya kutangazwa rasmi kuwa kimekuwa Chuo Kikuu, Uongozi wa Mzumbe uli-*take off* vizuri sana, kwa umakini na timu nzima ya uongozi pale ilifanya kazi nzuri mpaka leo Waziri anasimama na kueleza mafanikio ya Chuo Kikuu, pamoja na upya wake. Nawapongeza sana Viongozi wote wa Chuo Kikuu cha Mzumbe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilifurahi sana niliposikia Profesa Warioba, amechaguliwa kuwa *VC* wa *Mzumbe University*. Warioba ni mzoefu, yupo Mzumbe muda mrefu, Mzumbe ina historia kubwa katika Taifa letu na chini ya uongozi wake sasa matunda mazuri yameanza kuonekana pale Mzumbe.

Mheshimiwa Spika, Chuo Kikuu hiki kina matatizo mengi. Lakini pamoja na yote hayo, niishukuru kwanza Wizara imeanza na maeneo machache, wameanza kutoa fedha kwa ajili ya Maktaba, *ITP*, kusomesha walimu na kadhalika. Lakini pamoja na juhudi hizi za Wizara, ningependa kumsihi na kumshauri Waziri aongeze juhudi, atupie jicho lake tena pale Mzumbe kwani kuna matatizo mengi. La kwanza, ni majengo. Majengo ya Mzumbe ni ya muda mrefu, kwa hiyo yamechakaa. Nyumba za watumishi nazo hazijapata bajeti muda mrefu, ningepomba Waziri katika bajeti zake ahakikishe kwamba majengo ya Chuo Kikuu cha Mzumbe yanafanana na hadhi ya Chuo Kikuu kipya katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na suala la majengo, katika ziara yangu ya mwezi wa Sita nilipokwenda pale, wanajumuiya wa Mzumbe walitoa matatizo yao mengi likiwemo la upungufu wa vitendea kazi hasa kompyuta, suala ambalo niliwasiliana na Naibu Waziri na aliahidi kwamba litafanyiwa kazi. Kwa hiyo, nikaona nitumie nafasi hii kulileta rasmi ombi hili ili lifanyiwe kazi sasa kwa kutumia bajeti yetu ya leo. Jina la Mzumbe lina historia ndefu katika Taifa letu lakini hali ya Mzumbe ya leo ni shwari, mambo yanakwenda vizuri, tunaomba msukumo kutoka Wizarani.

Mheshimiwa Spika, tatizo la muda mrefu ambalo tumewahi kulizungumza ni barabara. Barabara ya kutoka Sangasanga kwenda Chuo Kikuu Mzumbe ina urefu usiozidi kilomita mbili na nusu. Barabara hii ilishawekwa katika mpango wa kuwekwa lami miaka mitatu iliyopita lakini jambo la kushangaza yakatokea majibu ya ajabu ajabu kwamba wafadhili waliotoa fedha zile hawakuweza kuishughulikia barabara ile kwa sababu Serikali yetu haikutoa mchango wake. Ni jambo la kusikitisha, kwa hiyo ninaiomba Wizara ya Elimu ya Juu, ishirikiane na Wizara ya Ujenzi, huu mpango upo njiani, tuusimamie tukamilishe barabara ile ili iwekwe lami kama ilivyokusudiwa katika mipango ya huko nyuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na tatizo hilo la barabara lakini bado tuna matatizo mengine ambayo mimi nina hakika chini ya uongozi wa Profesa Warioba, yatatatuliwa hatua kwa hatua. Tatizo lingine ambalo wanajumuiya wameomba ni suala la ada. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kimepunguza ada, Chuo Kikuu cha Mzumbe bado ada zake zipo pale pale wanatozwa kuanzia shilingi laki tisa na nusu mpaka shilingi milioni moja na laki tatu, wenzetu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kuanzia shilingi laki sita na kuendelea. Suala hili nimeliwakilisha kwa Mheshimiwa Naibu Waziri na bahati nzuri leo yupo, ningepomba

atutolee ufafanuzi na tunaomba Chuo Kikuu cha Mzumbe nacho kiweze kupewa kiwango cha ada sawasawa na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, pamoja na matatizo hayo naomba tena kurudia kauli yangu kuipongeza Wizara kwa kuanza kupeleka fedha Chuo Kikuu cha Mzumbe, lakini ningepia pia waendeleo na mipango mingine mizuri zaidi ili kukijengea heshima. Tunashukuru kwamba hiki ni Chuo Kikuu kipyua, kimepata marafiki wengi na kinaendelea kupata misaada, lakini bado tunaomba msaada wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa niende Chuo Kikuu cha Kilimo *SUA*. Nianze na pongezi nyingi sana kwa Uongozi wa *SUA Morogoro*, kwa kazi nzuri wanayofanya hususan kuwaendeleza wakulima wadogo wadogo Vijijini. Chuo Kikuu cha *SUA* kama kingetumiwa vizuri na Wizara ya Kilimo leo kingekuwa mkombozi wa kilimo katika Taifa letu. Wananchi wa Vijiji zaidi ya vinne wa Tarafa ya Mgeta, Wilaya ya Mvomero wameondokana na umaskini kutokana na Chuo hiki kupeleka miradi, kuwaelimisha na hatimaye leo Mgeta ndiyo inalisha matunda katika Mikoa mingi kama vile Morogoro, Dar es Salaam na Mikoa jirani. (Makofi)

Chuo Kikuu hiki cha *SUA* nacho kinaendeleza ushauri wa kilimo kwa maana ya mazao mbalimbali lakini pia kimewanufaisha wananchi katika kuwaelimisha na kuwapa mafunzo ya ufugaji. Leo Mgeta kuna mbuzi wa maziwa, tena mbuzi wa kisasa, mbuzi mmoja anatoa zaidi ya lita tano. Mbuzi mmoja anauzwa kwa Sh.80,000/=, 90,000/= au 100,000/=. Ukiambiwa mbuzi anauzwa bei hiyo huwezi kuamini, lakini mbuzi hawa ni wa kisasa na ni utaalum unaotolewa na *SUA*. Nawapongeza sana *SUA* na nawaomba sana waendeleo na Vijiji vingine vya Ngerengere, Mvomero, Matombo, Turiani na maeneo mengine. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, *SUA* wana huduma ya *TV*. Huduma ile inaendelezwa na Taasisi ya Elimu ya Kujiendeleza, inatoa elimu kwa wakulima na inaelimisha zaidi matunzo ya wanyama, mifugo, pamoja na kilimo. Ningewaomba sana Viongozi wa *SUA* wahakikishe *TV* ile sasa inaonekana na wananchi wa Mkoa mzima wa Morogoro badala ya Manispaa peke yake. Sasa hivi *SUA TV* inaonekana Manispaa tu, wananchi wa Mgeta, Nyandila, Chenzema, Kikeu hawaoni ile *TV*, lakini ni wadau wa *SUA*. Kwa hiyo, nashauri Uongozi tushirikiane nao. Mimi kama Mbunge, niko tayari kwa hali na mali kushirikiana na Uongozi wa *SUA*. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naomba *SUA* wapokee taarifa rasmi kuwa Mradi wa Umeme Mgeta utakamilika mwishoni mwa mwaka huu na miradi yote ya *SUA*, pale Mgeta, Langali itapata huduma ya umeme.

Mheshimiwa Spika, kwa leo yangu yalikuwa ni hayo. Nawapongeza tena *SUA* na Mzumbe, nawatakiya kila la kheri na mwisho kabisa naunga mkono hoja mia kwa mia. (Makofi)

MHE. KIDAWA HAMID SALEH: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi na mimi ili nitoe mchango wangu mdogo tu katika hoja hii iliyokuwepo mbele yetu. Ninaanza na kutoa pongezi zangu za dhata kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu wake na Watendaji wake wote, kwa kutuletea hotuba hii ambayo ni ya kina, ni fupi lakini imechanganya maeneo yote ambayo yalikuwa ni muhimu kutolewa taarifa.

Mheshimiwa Spika, naungana na mwenzangu Mheshimiwa Membe hapa aliposema kuwa elimu ya juu, sayansi na teknolojia ni *factor* muhimu sana katika kuleta maendeleo ya nchi yoyote ile. Hakuna nchi ambayo inaweza kuendelea ikiwa wananchi wake hawana elimu ya juu hata kama wakiwa wengi kiasi gani. Tanzania tuna watu wengi mno lakini tuko nyuma sana kielimu hasa elimu ya juu. Kwa maana hiyo tuna safari ndefu ya kwenda ili kuweza kufikia maendeleo ya kisasa. Katika ulimwengu huu wa utandawazi na ufunguaji wa milango ya kukaribisha *FDIs* au *Foreign Direct Investment* na sera zetu hizi za ubinafsishaji ni lazima kabisa wananchi wetu tuwapatie elimu ya juu.

Kama si hivyo tutabakia sisi kuwa ni wasindikizaji tu katika soko huria la kazi kwa sababu tutashindwa kupambana na wale wenye taaluma. Kwa maana hiyo kazi hata ndani ya nchi yetu zilizokuwa za maana ambazo zinahitaji taaluma zitahodhiwa na wenye taaluma kutoka nchi za nje.

Mheshimiwa Spika, takwimu zinatueleza hapa kuwa Watanzania tunakamata mkia katika kutoa wahitimu hasa tukilinganisha na nchi za Afrika Mashariki yaani Kenya, Uganda na sisi wenyewe. Tunaongozwa na Kenya na Uganda na sisi tuko mkiani. Hali hii kwa kweli siyo nzuri na Serikali yetu itabidi iandae mipango kamambe na mkakati kamambe wa kulitafakari hili na kuona namna gani linaweza kuondolewa katika siku za karibuni. Kama si hivyo tutakuwa katika hali mbaya sana ya kimaendeleo.

Mheshimiwa Spika, vyuo vyetu tunavyo kama ilivyozungumzwa hapo lakini haviwezi kukidhi yale mahitaji ya wananchi wetu kielimu kwa kuwa hawawezi kuchukua wananchi wote ambao wana uwezo wa kujiunga na Vyuo hivyo Vikuu. Kwa maana hiyo ule mkakati niliozungumza ni lazima uandaliwe kwa sababu tutakuwa tunawakosesha haki ya elimu ya juu wale wote ambao wana uwezo wa kupata elimu hiyo.

Mheshimiwa Spika, baada ya dibaji hiyo, sasa nije katika kutoa mchango wangu katika Chuo Kikuu Huria. Naipongeza kwa dhati Serikali kwa kukianzisha Chuo hiki ambacho kimeanzishwa mwaka 1992. Chuo hiki kwa kweli kinafanya kazi nzuri sana kwa sababu kinajaribu kuwachukua wale wote ambao hawakupata nafasi ya kuingia katika vyuo vingine Vikuu na hawa wanafunzi wanaoijiunga hapa kuna wengine utashangaa wamemaliza darasa la saba lakini wameweza kujiendeleza mpaka waka-*qualify* kuingia katika Vyuo Vikuu na wanahitimu vizuri. Hii inathibitisha kuwa kwa kweli tuna matatizo, wanafunzi hawana matatizo lakini nchi yetu tuna matatizo ya kuwa na nafasi finyu, hatuwezi kuwachukua wanafunzi ambao wana uwezo kabisa wa kujiendeleza hadi kupata elimu ya juu.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii vile vile kuipongeza uongozi wa Chuo Kikuu Huria. Kwa kweli wanajitahidi sana kwa sababu wanafanya kazi katika mazingira magumu na mazingira ya kipekee. Lakini uongozi huu una zile sifa tatu za uongozi (*3 Cs*), ambazo Mheshimiwa Diallo, amekuwa akitukumbusha mara kwa mara. Ambazo ni *confidence, competence and commitment*. Wanajitahidi kweli. Chuo hiki katika mwaka 1994 kilikuwa na wanafunzi 766 tu lakini hadi kufikia mwaka 2003 kina wanafunzi 13,351. Hali hii ni ya kupongezwa kabisa na inaonyesha kuwa Watanzania wana moyo wa kujiendeleza na wamehamasika sana na kujua umuhimu wa kuwa na elimu ya juu. Kwa hiyo, naomba Serikali itoe msaada wa kila hali kuwasaidia hawa wananchi wanaotaka kujiendeleza kupitia Chuo hiki Kikuu Huria na ikiwezekana kuwapatia mikopo ya kutosha kuweza kupata elimu hii kwa sababu wanaoijiunga hapa ni watu wazima na wana majukumu makubwa ya kifamilia na ya kijamii. Kwa hiyo, ni ujasiri mkubwa mtu kuamua hasa katika mazingira kama hayo, kujiunga na chuo ili apate elimu, hii inaonyesha ujasiri na uelewa mkubwa wa umuhimu wa elimu.

Mheshimiwa Spika, takwimu tulizopewa zinaonyesha kuwa kati ya wanafunzi hao wanaoijiunga na Chuo asilimia 19 tu ndiyo wanawake na waliobakia asilimia 81 ni wanaume. Hii vile vile inathibitisha kuwa majukumu waliyo nayo wanawake ni makubwa sana hasa ya kifamilia ndiyo maana wanakuwa na kigugumizi kidogo kwenda kujiunga na chuo hiki hasa ikiwa kama msaada wanaoupata katika familia zao ni mdogo sana. Lakini hata hivyo, natoa wito kwa wanawake wajitahidi kujiunga na Chuo hiki kwa sababu elimu ni ya wote na inawanufaisha wote wanawake na wanaume. (*Makofi*)

Chuo Kikuu Huria kimeenea kote Tanzania. Kina vituo katika Mikoa 21 Tanzania Bara, ukiwemo na Mkoa mpya wa Manyara, kituo ambacho kimefunguliwa tu hivi karibuni na kina vituo viwili kule Zanzibar kimoja kipo Unguja na kingine kipo Pemba. Kwa maana hiyo, wananchi wanapata fursa ya hii elimu kupitia vituo hivi huko huko Mikoani mwao.

Mheshimiwa Spika, ingawa Chuo hiki kinafanya kazi nzuri lakini kina matatizo. Mengine tayari Mheshimiwa Kissassi, alishayazungumzia, lakini mimi nimeyaorodhesha machache tu yafuatayo:-

- (a) Kuna upungufu wa wafanyakazi wakiwemo hata wahadhiri.
- (b) Kuna uhaba wa machapisho ya kufundishia na ya kujifunzia ingawa wanajitahidi kwa kiasi chao kutayarisha haya lakini bado hayajatosha na wala hayajatosheleza mahitaji.
- (c) Kuna tatizo la kuchelewa kusahihishwa *assignments, tests* na hata mitihani yenyewe.
- (d) Wakati mwingine inashindikana hata kufanyika *face to face session* kama inavyotakiwa kufanywa kwa wakati maalum.

Mheshimiwa Spika, lakini haya yote yasingetokea kama ingekuwa chuo hiki kinapatiwa fedha za kutosha za kuendeshea kazi zake. Chuo hakipatiwi fedha za kutosha, Bajeti wanayoileta inakatwa vibaya sana na hata ile ambayo inapitishwa, hawapatiwi fedha kwa asilimia mia moja. Wanapatiwa fedha kidogo mno ambazo zinasababisha kuwa na matatizo haya. Chuo kikishakuwa na matatizo kama haya ambayo ni ya kitaaluma kwa kweli sijui tunataka kiendeleo namna gani.

Mheshimiwa Spika, ili kukifanya Chuo hiki kiweze kufanya kazi yake vizuri, nashauri Serikali ijaribu kufikiria ile Bajeti ambayo wanaileta wao wenyewe, kwa sababu wao ndiyo wanaojua mazingira ya kazi zao, wao wenyewe ndiyo wanajua wana matatizo gani na kiasi gani cha fedha kinaweza kuwatosha katika kufanya kazi zao. Lakini wao wakileta ikikatwa, wakipewa tu kinachofikiwa labda hiki kinatosha ndiyo matatizo kama haya yanatokea. Kwa hiyo, hili lifikiwi kutokana na mazingira yalivyo.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni la utafiti. Kwa kweli naungana na Kamati ya Huduma za Jamii, iliyoambua hoja hii kwa kusema kuwa Serikali iweke asilimia fulani kutoka mfuko wake mkuu kwenda katika utafiti, kwa sababu bila utafiti sidhani kama kuna maendeleo yoyote yanayoweza kupatikana. Kwa hiyo, hili na mimi naliunga mkono na nasisitiza Serikali ilifanyie kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia ningomba tu kupata ufafanuzi katika Kitabu hiki cha Bajeti, katika kiambatanisho namba 4, *column* ya 3, *bullet* ya mwisho, Chuo Kikuu cha Kimataifa cha Tiba na Teknolojia. Kuna nyota pale, halafu hii nyota inaeleza, haki zinazoendana na hati hii zimesitishwa hadi kutimizwa kwa masharti ya Baraza. Naomba ufafanuzi kuhusu hili, nini kimetokea na kwa nini iko hivi?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja ahsante sana. *(Makofi)*

MHE. MARGARETH A. MKANGA: Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii, kukushukuru kwa kuniruhusu tena kuchangia hoja iliyopo mbele yetu. Aidha, natoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, Mheshimiwa Dr. Pius Ng'wandu, Naibu wake, Katibu Mkuu, Wakurugenzi Wakuu, Wakuu wa Vyuo vyote, watendaji na wataalam wa Wizara, kwa kazi nzuri wanayoifanya katika jitihada za kujaribu kufikia kiwango cha juu cha matumizi ya sayansi na teknolojia nchini. Pia naipongeza Wizara kwa kuandaa hotuba nzuri, yenye kueleweka, ambayo imetoa ufafanuzi wa kina wa yale yote ambayo Wizara wametarajia kuyatekeleza katika mwaka huu wa fedha wa 2003/2004. Kwa msingi huo basi, mchango wangu utajielekeza katika kutoa ushauri tu na nyongeza za taarifa pale inapobidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza, nimefurahi sana kubaini kwamba, Serikali imedhamiria kupanua elimu ya juu kwa kuboresha miundombinu ya Vyuo Vikuu ili hatimaye iweze kuhimili uwezo wa wanafunzi. Hili kwa kweli ni dhamira na ni jukumu kubwa kwa sababu bila hivyo, kama ilivyo kwenye taarifa ya Kamati ambayo nimesoma asubuhi mambo yatatuwia magumu kwa vile wanafunzi wengi tunategemea kwamba wataweza kufaulu. Lakini nina ushauri kidogo tu kwamba, Wizara kwa sababu ndiyo msimamizi wa Vyuo vyote hivi, basi iendeleo kuvihimiza Vyuo hivyo viweze kubuni njia za kisasa za kufundishia na kujifunzia.

Mheshimiwa Spika, natoa pongezi kwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kwa sababu naona ilielezwa kabisa kwamba imeanza angalau mbinu mpya ya kisasa ya watu kupata *Lecture* kwa kupitia mtandao wa kompyuta. Hiyo inasaidia kumwezesha mwalimu kidogo kupumua, hiyo inasaidia mwanafunzi kuweza kujifunza kwa wakati wake na labda kuweza kupata taarifa nyingi zaidi kuliko *Lecturer* akisimama pale peke yake. Kwa hiyo, na Vyuo vingine basi vifuate mwelekeo huo katika mipango yao ya maendeleo kwa sababu ndiko tunakoelekea na hii itasaidia kutuletea wataalam wengi na kwa muda mfupi tu kwa sababu kwa kutumia kompyuta, unapata taarifa ya yale yote ambayo yanahitajika kuyapata kwa muda mfupi.

Mheshimiwa Spika, aidha, nakubaliana na ushauri wa Kamati ya Huduma za Jamii kuhusu mafunzo yanayotolewa na Kituo cha Kompyuta cha Dar es Salaam na ushauri wake wote, lakini ninashauri kuwa katika kituo hiki pawepo na kompyuta maalum ambazo zinaweza kutumika kufundishia watu au wanafunzi wasioona kama nchi za nje zinazofanya. Nasikia kuna kompyuta inatumika, inaimba halafu

inakuelekeza sasa bonyeza hapa au hapa, wenzetu wasioona huko wanatumia kompyuta hizo. Kwa hiyo, kituo hiki kwa sababu ndicho kina dhamana ya kuhakikisha taaluma hii inakwenda vizuri basi kiwe na kompyuta chache kusudi hata watu wasioona wasome pale na wanafunzi waliopo pale wasioona waweze kutumia teknolojia hii kama wengine wanavyofaidika.

Mheshimiwa Spika, naomba niunganishe hoja hii na ile ya Chuo Kikuu Huria kwamba, kwa mwaka huu wa fedha wamedhamiria kuanzisha karakana ya kompyuta ambayo itasaidia kuwafundisha wanafunzi kwa njia ya mtandao. Basi katika karakana hii pia pawepo na kompyuta hizo maalum ninazozingumzia na Chuo Kikuu Huria kimesema kwamba, mwaka huu kinaongeza idadi ya wanafunzi wasioona. Kwa hiyo, hapa hiki kiwe ni kifaa kimojawapo ambacho kitawasaidia kujifunza kwa urahisi.

Mheshimiwa Spika, naipongeze Wizara kwa kuongeza idadi ya wanafunzi wanawake katika vyuo vyetu na katika vyuo vya ufundi. Pongezi hizi zimetokana na kwamba tukumbuke ule usemi unaosema "ukimwelimisha mwanamke mmoja unaelimisha jamii nzima", hii inasaidia kwamba tutapata wataalam na nadhani ni kutokana na jitihada hizi hizi, mimi nimesoma gazetini kwamba kuna mama mmoja wa kwanza kupata nadhani *Ph.D.* ya *Physics* anaitwa Margareth kama mimi, lakini jina la pili nimelisahau, nikajisikia fahari, imeandikwa kwamba ni mwanamke wa kwanza Tanzania. Ni katika jitihada hizi za kusogeza wanawake kuelimika, kwa kweli watu wapo, wana uwezo, lakini wakati mwingine wanatingwa na majukumu ya kijamii. Hapo nishukuru kabisa kwamba, Chuo Kikuu Huria kinasaidia hata yule anayetingwa na majukumu ya kifamilia akipata muda anaweza kuendelea kujisomesha kama mwanamke. Wenzetu wanaume mna nafasi ili mradi tu mpate pesa, lakini ulezi wa watoto wachanga, tunabaki kunyonyesha sisi ninyi mnapokuwa shuleni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Waziri imeelezwa kuwa Tume ya Taifa ya Mionzi mwaka huu itakusanya mabaki ya vyanzo vya mionzi na kuyahifadhi huko Arusha. Kwa kweli nimefarijika na uamuzi huu kwa sababu hii mionzi inaweza ikawa ni hatari kama ikiachwa ikazagaa zagaa ovyo ila naomba kufahamu kulikuwa na habari kwenye gazeti moja kwamba, kuna mitungi imegundulika mtu ameingiza *uranium* hapa nchini bila idhini. Je, Tume ilifanikiwa kupata mitungi hiyo na ndiyo imeshahifadhiwa huko Arusha au ile mitungi iliishia wapi? Mimi niliona kwenye Televisheni nadhani lilikuwa jambo la kweli. Kuhusu suala hilo naomba ufafanuzi ili tujue kwamba mambo hayo yaliishia wapi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Muswada wa Elimu ya Juu, ambao unatarajiwa kufikishwa hapa Bungeni baadaye, natoa tu ushauri wa mapema kabisa katika maandalizi ya Muswada huo ili nisije nikawa na kelele nyingi baadaye kwamba, Muswada huo wa Elimu ya Juu uzingatie mahitaji maalum ya wanachuo na hasa wanachuo wenye ulemavu watakaoweza kufikia kiwango hicho cha Elimu ya Juu.

Mheshimiwa Spika, baada ya ushauri huo, mimi sikuwa na mengi ya kuzungumza, naomba tu niunge mkono hoja hii na niwatakie kheri watekelezaji. Kwa kweli Wizara hii nina mategemeo nayo mengi sana kwa sababu mambo yake yanafanyika kisayansi. Ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. BENSON M. MPESYA: Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nikushukuru wewe binafsi, kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia katika hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu.

Mheshimiwa Spika, pili naomba niungane na wenzangu walioiunga mkono hoja hii na mimi ningependa kuiunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Ninazo sababu za msingi hasa za kuiunga mkono hoja hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwaka 2002 mimi na Mheshimiwa Prof. David Mwakyusa, tulilizungumzia sana suala la *Mbeya Technical College* kubadilishwa kuwa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia, kama wosia aliotuachia Marehemu Baba wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, lakini nafarijika sana kwamba, Wizara hii imekuwa sikivu. Waziri wetu Mheshimiwa Dr. Pius Ng'wandu tarehe 9 Juni, 2003 wakati Bunge linaendelea alikuwa Mbeya kuzindua

Kozi ya *Advanced Diploma in Engineering* kama hatua za kukipeleka Chuo hicho katika kuwa Chuo Kikuu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika na siyo hilo tu, Mheshimiwa Naibu Waziri, naye alifika akatupa hamasa. Nilifarijika zaidi pale niliposikia kauli ya Katibu Mkuu alipoitoa kule Arusha kwamba, nia ya Serikali ya kukifanya Chuo cha *Mbeya Technical* kuwa Chuo Kikuu iko palepale. Kwa kweli sina budi kuipongeza Wizara hii, Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wataalam wake wote, kazi mliyoifanya kwa kweli ni nzuri sana. Naamini kabisa Mheshimiwa Waziri, utakuwa ni shahidi jinsi walivyokupokea Mbeya kwa matarumbeta na shamrashamra za wananchi zinatoshesha sana. Mimi nimepitia ripoti ya wataalam ni hatua zipi zifuatwe ili kiwe Chuo Kikuu na mimi nisingependa kutofautiana na ripoti ya wataalam. Mambo haya naona yanakwenda kisayansi zaidi badala ya blaa blaa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika na bahati nzuri Mheshimiwa Waziri ametuonyesha hata kwenye kitabu chake cha hotuba alichokiwasilisha hapa Bungeni, kwa kweli kimeandaliwa kisayansi. Hotuba yake ilikuwa na maneno machache na takwimu za *support* zimewekwa humo ndani. Kwa hiyo, tunakushukuru sana. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naomba niende kwenye eneo la pili, hasa kuhusu idadi ya wanachuo wanaojiunga Vyuo Vikuu mwaka huu. Mpaka leo asubuhi takwimu tulizonazo Kenya ina wanachuo 84,000, Uganda ina wanachuo 35,000 na Tanzania tuna wanachuo 18,000. Sasa ukilinganisha kwa nchi hizi tatu, utaona kwamba Tanzania bado tuko nyuma sana.

Mheshimiwa Spika, katika kitabu chake cha hotuba, Mheshimiwa Waziri, ameeleza waziwazi kwamba ipo tofauti kati ya kudahili halafu baadaye udhamini. Kwa hiyo, tatizo kubwa tulilonalo ni udhamini tutafanyaje na hili lazima tulichukulie kama tatizo na kilio cha nchi nzima. Chuo Kikuu cha Sokoine peke yake walidahili wanachuo 1,888 ambao wana sifa zote za kujiunga na Chuo Kikuu cha Sokoine, lakini wamechukulia vijana 700, hawa wengine 1,088 wanaenda wapi? Tukienda Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ni hivyo hivyo na tukienda Chuo Kikuu cha Mzumbe ni hivyo hivyo. Hili kundi linalobaki linaenda wapi? Wakati wenzetu wanapiga hatua za kusomesha zaidi. Kwa sababu *component* moja ya *globalization* ni Elimu ya Juu. Sasa tujiulize vijana wetu hawa wanaweza ku-*compete* na Wakenya, wanaweza waka-*compete* na Waganda katika soko la ajira. Sasa hiki lazima kiwe ni kilio cha Taifa. (Makofi)

Kwa hiyo, tunaona hata sasa hivi *trend* ya shule hizi zinazoanzishwa, wenzetu wa Kenya na Uganda ndiyo wanafundisha watoto wetu. Sasa hivi ukiangalia Mbeya iko mbali sana kutoka Kenya na Uganda, lakini wamefika mpaka kule ndiyo walimu wa *Kindergarten*, ndiyo walimu wa shule zetu tunazosema *English Medium*. Hawa vijana wetu watakwenda wapi. Lazima Watanzania tubadilike tuangalie namna ya kulitatua tatizo hili. Itafika mahali kitakuja kile kichekesho cha kusema nafasi ya kazi ilitangazwa mahali na walioomba walikuwa wengi wa Kenya, Tanzania na Uganda, sifa ziliwekwa pale ni Shahada gani unatakiwa uwe nayo. Lakini cha ajabu ni kwamba, Mtanzania alikwenda na *degree* ambayo waliokuwa wanaendesha usaili ule ilibidi watafute inapatikana wapi, alienda na *degree* inaitwa *ABF*.

Wataalam wakajaribu ku-*surf* kwenye *Internet* ni Chuo Kikuu kipi katika Vitivo vyote kinatoa *degree* ya *ABF*, ili tuweze kumsaidia huyu Mtanzania. Lakini alipokuwa amesimama alikuwa *so confident* kwamba na mimi ni mmoja kati wahitimu hapa, lazima nifikiriwe. Baadaye ilionekana kwamba hawakuiona, wali-*surf* kwenye *Internet* za Vyuo Vikuu vyote hata vile vya *E-learning* hawakuiona hiyo *degree* ya *ABF*. Lakini kwa sababu ya heshima ya Tanzania na huyo alikuwa anatoka Tanzania, *you never know* hawa wenzetu Watanzania wanajiamini, hebu tumwite yeye mwenyewe tumwulize. Akaitwa mbele ya jopo lile eeh bwana hii *degree* yako unayoiita *ABF* umesomea kitu gani? Akasema aah hiyo is *very simple*, ni *easy* kwa sababu hiyo maana yake *I attempted but failed*. (Kicheko)

Kwa hiyo, *attempted but failed*, lakini amekwenda pale. Hili ndiyo kundi ambalo tunalilea. Ukitangaza kazi ya kusema nataka watu wenye Shahada, kwanza hawa waliokosa kwenda kwenye Vyuo Vikuu watakwenda na *ABF (Attempted But Failed)* na yeye anataka awe *considered*, sijui sasa kama kutakuwa na *competition* hapo! Kwanza, naomba Wakala wa Mfuko wa Elimu ya Juu, atafutwe haraka sana ikiwezekana Mheshimiwa Waziri utaniona ni mkosefu wa adabu, kusema atafutwe haraka sana, kwa sababu mimi nilikuwa mwanafunzi wako, pamoja na Mheshimiwa Hamza Mwenegoha hapa. Lakini

naomba Mheshimiwa Waziri, huyu Wakala wa Mfuko wa Elimu ya Juu atafutwe haraka sana ili vijana wetu wengi waweze kupata Elimu ya Chuo Kikuu, ambayo inaendana na karne ya 21. (Makofi)

Lakini la pili, ningeliomba sana Mashirika ya Umma, pamoja na Mashirika yasiyokuwa ya Umma, tujenge tabia ya kuweza kuwa-*sponsor* hawa vijana ambao ni hazina kuu ya Taifa. (Makofi)

La tatu, rai yangu ni kwa Watanzania sisi wenyewe tujenge tabia ya kuwekeza kwenye Elimu ya Juu. Tusipojenga kuwekeza katika Elimu ya Juu, tutakuwa tunalegalega wakati wenzetu wanakimbia.

Mheshimiwa Spika, sasa niamie kwenye eneo lingine ambalo mimi pamoja na wenzangu watatu tunaliwakilisha Bunge hili, ni kuhusu Chuo Kikuu Huria. Katika ile idadi niliyoizungumza kwamba Tanzania mpaka leo asubuhi tulikuwa na wanachuo 18,000 na kati yao 13,000 ni wa Chuo Kikuu Huria, waliobakia ni hawa ambao wako kwenye hizi *Conventional Universities*, Mzumbe, *SUA* na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Sasa Chuo Kikuu Huria kinafanya katika mazingira magumu sana kuanzia walimu, uandaaji wa machapisho na mambo mengine. Tunashukuru kwamba, mmetupatia Profesa Mmari, kama kuna watu ambao ni *committed* katika nchi hii, basi Profesa Mmari na sikushangaa alipopewa ile *Award* ya *Martin Luther*, alikuwa anastahili nafikiri. Lakini Chuo Kikuu Huria kina matatizo sana na mengi mno kama hawa ndiyo wanaobeba jukumu la kusema ni 13,000 lazima zitafutwe mbinu za kutafuta namna ya kutanzia matatizo yaliyoko katika Chuo Kikuu Huria. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwanza nilikuwa naomba Wizara na wataalam wote hebu mfanye utafiti, *unit cost* ya kumsomesha mwanafunzi Chuo Kikuu Huria nafikiri siyo sahihi na ndiyo maana ruzuku yao inakuwa ni ndogo sana. Inatakiwa muangalie kabisa *unit cost* ya kumsomesha mtu Chuo Kikuu Huria ni kiasi gani, kama ipo iliyokuwa inatolewa mwanzo, mimi nafikiri ni *very unrealistic*, mambo yamebadilika sasa hivi. Mtu anasafiri kutoka Mbeya kwenda *University of Dar es Salaam* kwa ajili ya *practical*, lakini *unit cost* inaonyesha kwamba analipwa kiasi gani.

Mheshimiwa Spika, lakini la pili ni kwamba, hata katika mkopo tu. Huyu wa Chuo Kikuu Huria analipiwa theluthi moja ya ada kwa nini na hawa waliopo katika Chuo Kikuu Huria, *in-service* wengi ndiyo *true investment* ya nchi hii, una uhakika kwamba unapowasomesha hawa wanarudi kazini na wengine wanarudi kufundisha wanakuwa *more productive* kuliko yule ambaye tunam-*sponsor* hata kum-*trace* yuko wapi hatujui tufanye nini. Sasa ni kitu cha ajabu theluthi moja ya Sh. 120,000/= ndiyo anayopewa huyu Sh. 40,000/=, ana mke na watoto, atafanyaje mtu kama huyu na huyu kum-*trace* ni rahisi unajua utamkuta wapi, utamkuta katika shule ya sekondari, utamkuta mahali fulani na huyu ana *collateral* na ana pensheni yake, huyu ndiye alitakiwa afikiriwe zaidi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, tatizo la tatu, ambalo lipo ni madeni sugu katika Chuo Kikuu Huria. Mheshimiwa Waziri, nilikuwa naomba kuhusu deni hili mtafute namna ya kulitua kusudi mlimalize, halafu hawa ndiyo wafanye kazi katika taratibu zinazotakiwa, kuna deni ambalo wanadaiwa hata wanashindwa kufanya kazi. Mtamwuliza sana Mzee Mmari, yule bado ni *asset* katika Taifa hili, msaidieni katika kutatua tatizo hili. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, hili la kuhusu fedha za maendeleo siwezi kulizungumza kwa sababu tayari mwenzangu Mheshimiwa Remidius Kissasi, amelizungumzia. Lakini naomba nieleze tu kuhusu ruzuku kwa ujumla. Nimekuwa nikiangalia ruzuku inayopewa Chuo Kikuu Huria toka mwaka wa fedha 1998/1999, hakuna mahali ambapo Chuo Kikuu Huria kimewahi kupata ruzuku angalau asilimia 50 ya kile walichobajeti. Mwaka fedha 1998/1999, walibajeti shilingi bilioni mbili, ikawa *approved*, lakini walichokipata ni shilingi bilioni moja, chini ya asilimia 50.

Mwaka uliofuata wa 1999/2000, Bajeti yao ilikuwa ni shilingi bilioni 4/= ikawa *approved* walichokipata ni shilingi bilioni 1.900/=, chini ya asilimia 50 ya Bajeti waliyopangwa. Mwaka 2000/2001, Bajeti yao ilikuwa ni shilingi bilioni 4/=, *approved Budgeted* ikawa ile ile shilingi bilioni 4/=, lakini walichokipata ni shilingi 1,700,000,000/= chini ya asilimia 50, mwaka 2001/2002, Bajeti yako ilikuwa shilingi bilioni 3/= iliyokuwa *approved* ni shilingi bilioni 3/= walichokipata ni shilingi 1,100,000,000/=, inazidi kuteremka kulikoni? Sasa mnawategemea wafanye kazi gani kwa sababu *trend* inaonekana kwamba inateremka. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Benson Mpesya, ndiye aliyepangwa kuwa msemaji wa mwisho kwa mchana huu. Hata hivyo, nimebakia na msemaji mmoja tu kati ya waliojiandikisha kuchangia katika hoja hii kwa kuzungumza, naye ni Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, atapata nafasi ya kwanza katika kipindi cha jioni. Baada ya hapo watoa hoja watahitimisha hoja yao.

Sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni na tukumbuke tuliombwa tubakie hapa ili kupata maelezo fulani kutoka kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

(Saa 06.45 mchana Bunge lilifungwa mpaka Saa 11.00 jioni)

(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)

Hapa Mwenyekiti (Mhe. Eliachim J. Simpasa) Alikalia Kiti

MHE. DR. AISHA O. KIGODA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kwanza ili niweze kuchangia hoja iliyopo mbele yetu. Kabla ya kuchangia, naomba nitoe pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, Mheshimiwa Dr. Pius Ng'wandu, pamoja na Naibu Waziri wake, Mheshimiwa Zabein Mhita, kwa hotuba yao nzuri walioiwasilisha mbele yetu. *(Makofi)*

Vile vile napenda kuchukua nafasi hii niweze kuwapongeza watumishi wote wa Wizara hii pamoja na taasisi mbalimbali zilizo chini ya Katibu Mkuu, Bi. Lucy Mollel, kwa kazi nzuri sana ambayo wanawasaidia Mawaziri, hatimaye kuweza kupata hotuba iliyowasilishwa mbele yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa maelezo hayo naomba niseme pia naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuunga mkono hoja, naomba nichangie sehemu chache kwa nia ya kuboresha ili kuweza kuwa na utekelezaji mzuri. Kwanza, naipongeza Serikali kwa juhudi kubwa ya kutafuta uwezo kutoa ufadhili kwa wanafunzi ambao wanajiunga katika Vyuo Vikuu. Kwa sababu kweli kabisa ni kwamba, hali mbaya pamoja na kwamba uchumi wa nchi yetu ni mdogo lakini wanajitahidi sana na Wizara hii inajitahidi kuwafadhili. Lakini ninachoomba ni kwamba, naishauri Serikali pia ufadhili wao uweze kusaidia pia wale wanafunzi ambao wanatoka kule vijijini kwa sababu unakuta wengi wa vijana wetu wa vijijini siyo wengi wanaoweza kupata ufadhili au hata kama watapata ufadhili, mara nyingi taarifa za ufadhili huu haziwafikii. Kwa hiyo, naishauri Serikali kwa kweli pia ifanye *consideration* kwa hawa wanafunzi wanaotoka vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na ufadhili huu inaotoa Serikali, lakini vile vile kwa upande mwingine wa shilingi, kuna matatizo kwamba wakati mwingine kunakuwa nafasi zipo, lakini unakuta wanafunzi wenyewe huwa hawapatikani. Sasa mimi nadhani kama kuna ufadhili na nafasi zipo lakini wanafunzi wenyewe hawapatikani, nadhani kuna tatizo. Kwa hiyo, inabidi Serikali sasa kwa ujumla wake iangalie kwamba lazima iko sababu kwa nini hawa wanafunzi hawapatikani. Kwa hiyo, basi ningependa Waziri pamoja na Wizara yake au Serikali kwa ujumla, basi iangalie ni mikakati gani itakayoweza kufanyika ili kuona kwamba zile sehemu ambazo wakati mwingine nafasi hazijazwi kwa sababu moja au nyingine, basi zinatafutwa ufumbuzi na kuweka mikakati maalum na kuja kutueleza kwamba mikakati yao ni hivi na hivi. Kwa hiyo, huo ni ushauri wangu mmojawapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie kuhusu Chuo Kikuu Huria Tanzania. Kwa kweli na mimi niungane na wenzangu kuipongeza Serikali kwa kuanzishwa chuo hiki. Kwa kweli kimeweza kusaidia wale ambao wameikosa nafasi ya vyuo wameweza kuchukuliwa kama alivyozungumzia kwenye hotuba yake, idadi imeongezeka kutoka wanafunzi 10,000 mpaka 13,000 kwa kipindi cha mwaka uliopita na mwaka huu wanategemea kufikia mpaka 14,437. Kwa kweli hii inaonyesha kwamba, Serikali inajitahidi. Lakini vile vile ningependa kushauri kwamba, pamoja na kuongeza idadi ya wanafunzi na wigo

wa vitivo basi pia upanuliwe kwa sababu badala ya kuwa na Vitivo vya Sanaa, Sayansi ya Jamii, Sheria, basi na upande wa sayansi uongezwe ili watakapokuwa wanatoa hawa watalaam basi kuwepo na mchanganyiko mzuri kwa manufaa ya kuifanya nchi yetu iweze kuingia katika ushindani wa teknolojia na kitaaluma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie pia Taasisi ya Teknolojia ya Dar es Salaam, (*Dar es Salaam Institute of Technology*). Naipongeza Serikali kwa juhudi kubwa hii ambayo wameifanya kuweza kuona kwamba, hii taasisi inaweza kuwa na sura mpya ukilinganisha na wakati ule ilipokuwa *Dar es Salaam Technical*, nafikiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nikiwa kama mmoja wa Wajumbe wa Kamati, tuliweza kutembelea pale mahali. Naipongeza Serikali kwa sababu tumeona katika wale wanafunzi waliokuwepo, hakukuwa na ubaguzi wa kijinsia kwa sababu tulikuta wanafunzi wa jinsia zote hasa wanawake wako pale wanasoma vizuri sana mpaka na sisi wenyewe tukaona kweli hapa mambo ni mazuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tatizo tuliloona pale ile hali ya kile chuo kwa kweli inasikitisha sana. Kama tulivyozungumzia katika Wizara nyingine, kumwandaa mwanafunzi ni pamoja na kumwandalia mazingira mazuri ya kusoma ili kupata mtalaam mzuri. Lakini tulichokiona pale kwa kweli majengo kama walivyozungumza ni kwamba, yamejengwa tangu mwaka 1957. Si hicho tu ni kwamba, yale majengo yamechakaa, mpaka unashangaa hawa watoto hivi kweli wakitoka hapa watakuwa wanafunzi wa aina gani! (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, si hilo tu, tuliweza kutembelea sehemu kama karakana. Kusema kweli kwenye ile karakana unakuta sijui nisemeje kwa sababu vile vifaa vimechakaa, vimeisha kabisa, vingine havitengenezeki ingawa kweli wale viongozi wa chuo wanajitahidi kutafuta fedha huku na huku, lakini vitu vingine kweli vinahitaji Serikali ichukue juhudi maalum kuweza kuwasaidia, kwa sababu kama watakuwa wanapata masomo ya nadharia wakija kwenye *practicals* watakuwa wanashindwa. Majengo yanavuja na hii unakuta sasa siyo kuwakatisha tamaa wale wanafunzi, lakini unakuta pia hata walimu wenyewe ukiwakuta pale na wenyewe kweli kabisa wanakata tamaa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi nashauri hii Wizara kwa kweli Serikali iangalie hasa kile chuo kwa sababu ndiyo chenyewe kiko peke yake cha aina yake nadhani, tukifanye kionekane kina hadhi kwa sababu siyo tu kwamba kinachukua wanafunzi wa humu ndani, lakini kuna wengine wanaotoka nje ya nchi wanakuja pale. Kwa hiyo, tukipe hadhi yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba, nizungumzie suala dogo ambalo mimi binafsi huwa naliona. Ukichukua nchi yetu ya Tanzania *either* kihistoria au kumekuwa na baadhi ya mikoa au maeneo ambayo yanatoa wasomi ambao wanaongoza katika medani mbalimbali kama vile za kiuchumi, kisiasa, kiutawala (*economically, socially and administratively*). Serikali lazima sasa tuone kwamba, hii dhana tunayoiona kweli inapotea kwa sababu mara nyingi tunaona kwa sababu ambazo zimechanganyika kwamba kihistoria au kiutamaduni, unakuta wengine wanasema ukienda mahali fulani unakuta hawa watu wa hapa ndiyo jadi yao wakulima, labda wavuvi, wachungaji wengine wao ndiyo wenyewe wasomi katika nchi hii.

Lakini mimi nadhani hii ni dhana potofu kwa sababu kama hiyo dhana itakuwa inaendelezwa katika nchi yetu, basi utakuta kwamba hakutakuwa na *balance* ya viongozi katika Tanzania. Kwa sababu wengine tangu wamezaliwa wanajua kabisa kwa mfano, ukitaka kupata mchungaji unakwenda kwa Wasukuma au Wagogo, ukitaka kwenda labda kwa waganga wa kienyeji labda uende Tanga, Bagamoyo na Rufiji, huo ni mfano. Ukitaka kwa mfano kupata wasomi labda uende huko Mbeya, Kagera na Kilimanjaro, ukitaka ngoma uende kwa Wazaramo vitu kama hivyo. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi nafikiri hii dhana tujaribu kuipunguza kwa sababu vinginevyo utakuta sasa hata inapofikia kwamba tunatafuta viongozi tunakuwa na *imbalances* ya viongozi. Sasa hii inasababisha watu wanabaki wanalalamika. Sasa ukitaka kuweka viongozi katika ngazi za kisiasa, kiuchumi, kiutawala, kwa sababu wao ndiyo walivyokuzwa basi hafikii katika *quality* ya uongozi. Kwa

hiyo, mimi ningeomba Mheshimiwa Waziri na timu yake na sisi wote kwa pamoja, labda tujaribu kuona kwamba tufanye nini ili dhana hii iondoke. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile ningependa kuzungumzia vyuo binafsi. Mimi nitagusia labda upande mmoja tu kuhusu vyuo vya madhehebu ya kidini. Napenda kwa moyo mmoja, niwapongeze kwa sababu wanajitahidi sana kujenga sekondari, vyuo, ili kuweza kusaidia pale panatokea pengo. Lakini kama nilivyozungumza mwanzo, mimi ningeshauri kwamba vyuo hivyo kweli ni vichache na wakati mwingine unakuta hawa wenzetu kwenye madhehebu mbalimbali wanakuwa na uwezo totauti wa kupata hata wafadhili na kujenga hivi vyuo. Mimi napenda kuwashauri na kuwahamasisha ili waweze kupanua idadi ya vyuo. (*Makofi*)

Lakini vile vile ukiangalia upande huu wa watu madhehebu ya dini na wenyewe vile vile kunatokea *discrepancy*, unakuta vyuo vingi ni vya dhehebu fulani, lakini siyo kwamba nalaumu ila nasema madhehebu yote yajitahidi kwa wakati wao ili waweze kuwa na vyuo vya kila aina. Vile vile kuweza kutoa dhana potofu kwamba isije ikaonekana kwamba dhehebu fulani ndiyo linakuwa na vyuo vingi, halafu badala ya kujenga vyuo mtu anabaki analaumu ohoo kwa nini viongozi ni wa dini fulaniau kwa nini wanafunzi wanakuwa wa aina hii. Mimi nafikiri wote kwa pamoja washirikiane na pale wanapooona panahitaji kuelekezana basi wasisite kushirikiana ili dhehebu hili liweze kumsaidia huyu, huyu aweze kumsaidia huyu, ili kuweza kuongeza wanafunzi ambao watakuwa wanafundishwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile mengi wameshaongea wenzangu na nikiwa kama Mwanakamati, mengi yamezungumzwa kwenye Kamati yangu, mimi nilikuwa nataka niseme hayo.

Lingine la mwisho nilikuwa nataka kusema pesa ambayo inatengewa Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, mimi naona kwamba haitoshi kabisa. Kwa hiyo, hebu Serikali kupitia huko kwenye fedha, waone kwamba hii Wizara nayo ni moja kati ya Wizara muhimu.

Tunahitaji madaktari, tunahitaji *engineers*, lakini bila kuwa na pesa haiwezekani. Pesa zinazotolewa ni ndogo sana. Kwa hiyo, wafikirie kwamba waongezwe ili waweze kufanya kazi kwa uwezo na kwa ku-*relax* kidogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii, narudia tena kuunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia. Nakushukuru. (*Makofi*)

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. JACOB D. SHIBILITI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili nitoe mchango wangu katika Wizara hii ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa pongezi kwa Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu, kwa hotuba nzuri yenye nia ya kuokoa nchi yetu juu ya adui ujinga. Nawapongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri kwenye viambatanisho vyake hasa namba 4 ameanisha kama ifuatavyo: -

- (i) Vyuo vyenye barua ya mamlaka ya kuvianzisha;
- (ii) Vyuo vyenye hati ya usajili wa muda; na
- (iii) Vyuo vyenye hati ya usajili kamili na vyuo vyenye hati ya ithibati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru kwa hatua mbalimbali zilizoonyeshwa hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufafanuzi juu ya Chuo cha Ushirika Moshi kuwa Chuo Kishiriki cha Chuo Kikuu cha Sokoine kimefikia wapi na ni vitu gani vinahitajika ili kiweze kusajiliwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu bado inahitaji Vyuo Vikuu vingi kutokana na kasi ya Watanzania ya kutaka kufuta ujinga hivyo ni muhimu kuongeza vyo vikuu. Je, Wizara ina mpango gani wa kukipandisha Chuo cha Kilimo Ukiriguru kuwa Chuo Kikuu Kishiriki cha Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine ili kuziba pengo la upungufu wa Vyuo Vikuu lililopo sasa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na juhudi za Wizara hii kuwa ni nzuri, zinanifanya niunge mkono hoja hii kwa asilimia mia moja na naitakia mafanikio mema Wizara hii kwa mipango yake ya 2003/2004. Ahsante.

MHE. MICHAEL L. LAIZER: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu wake na Watendaji wao wote kwa kazi nzuri waliyofanya kwenye Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo mengi yameonekana, kwanza kasi ya wanafunzi kujiunga na Vyuo Vikuu imeongezeka, Vyuo Vikuu vimeongezeka, mitaala ya aina mbalimbali na vifaa vya kufundishia vimeongezeka, pia, wamekamilisha sera ya elimu ya juu kwa asilimia kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio hayo yameonekana wazi kutokana na kupungua kabisa kwa malalamiko ya wanafunzi wa Chuo Kikuu, jambo ambalo ni hatua kubwa ya mafanikio. Tofauti na Vyuo Vikuu vya nchi jirani ambao kila mwaka wanasababisha mgogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wananchi wameelewa kabisa umuhimu wa elimu na kila mwaka idadi ya wanafunzi wanaokwenda Chuo Kikuu inaongezeka. Inafaa juhudi kubwa ifanyike ili Vyuo Vikuu viongezoke na wanafunzi wengi waweze kujiunga na elimu ya juu. Tanzania ina watu wengi kuliko nchi za Uganda na Kenya, ingefaa na wanafunzi wa Vyuo Vikuu wawe wengi kuliko walivyo katika nchi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Wizara kwa kujitahidi kuwalipia wanafunzi wa Vyuo Vikuu ada kwa ajili ya kupata elimu ya juu. Hili ni jambo mojawapo lililopunguza malalamiko ya wanafunzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kueleza kwamba, elimu ya juu kwa jamii ya wafugaji hasa Wamasai ni kama haipo kabisa. Naomba Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, isaidie kuwapokea wanafunzi wanaomaliza Kidato cha VI ili nao wasiachwe nyuma kielimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu Mungu aumbe Tanzania, jamii ya Kimasai haijawahi kutoa wasichana zaidi ya watano kwenda Chuo Kikuu. Nachukua nafasi hii kuomba sana wasichana wa Kimasai wachukuliwe nao waingie Vyuo Vikuu. Bila elimu jamii hii haiwezi kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa tumejitahidi mimi na Mbunge mwenzangu wa Jimbo la Monduli, Mheshimiwa Edward Lowassa, kuwapeleka wasichana hao shuleni, wengi wao wamemaliza Kidato cha VI na wengine wapo Shule za Sekondari. Tunaomba wapewe kipaumbele ili nao waweze kuendelea kusaidia kuelimisha jamii na wazazi wao waone mfano mzuri wa mabinti zao watakapopata elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anatoa majumuisho anijibu ombi langu kuhusu wasichana hao wa Kimasai, ambao hawajawahi kupata elimu ya juu. Tusipowajali tutakuwa na tabaka kubwa tofauti katika jamii zetu za Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili nisisumbue kwenye vifungu naomba majibu.

MHE. SALOME J. MBATIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa shukrani kwa kupata fursa ya kuchangia hoja iliyo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, napenda kuipongeza Wizara hii kwa kazi na juhudi iliyofanya katika kipindi kilichopita cha mwaka 2002/2003.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ambayo ni *relatively new*, katika orodha ya Wizara, ni Wizara labda muhimu na nyeti sana kupita zote hasa ukizingatia wakati tuliomo wa maendeleo makubwa na kwa kweli Mapinduzi ya Sayansi na Teknolojia hasa ya mawasiliano ambayo yamekolezwa na utandawazi ambao umeifanya dunia kuwa Kijiji kimoja. Kwa namna hiyo, Wizara hii ina kazi kubwa ya kubuni, kuongoza na kudhibiti masuala ya sayansi, teknolojia hasa utafiti na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara nyingi kazi za wanasayansi huwa hazionekani mara moja kwa sababu ya *nature* yake kwa mfano, tafiti zilizofanyika, inabidi zifanyike kwanza katika maabara *tests* mbalimbali na kadhalika kabla ya kutoa hadharani matokeo ya tafiti hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafiti hizo ndizo zinazosaidia jamii kama ugunduzi wa dawa mbalimbali, ugunduzi wa mbegu, ugunduzi wa sumu mbalimbali zinazoathiri wanadamu, wanyama na kadhalika. Kwa namna hiyo mara nyingi watu wana-*play down* umuhimu wa Sayansi, ingawa matokeo yake huyafurahia. Hawathamini ule muda wa utafiti na hivyo kuto-*realize* kuwa utafiti unahitaji *funds*, *support*, *patience* na kadhalika. Hii ni kasoro kubwa ya wanajamii hasa wa dunia ya tatu. Tunafurahi kuona vinaelea, lakini kugharamia uundwaji ili vielee hatuelewi!

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishauri Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, iipigie debe dhana hii ili jamii ielewe na iwe nao bega kwa bega kuienzi Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo zuri jinsi Wizara ilivyotamka kuwa inaweka mikakati ya kupata uwiano wa jinsia (*Gender Balance*) katika masuala ya masomo ya elimu ya juu na kadhalika. Lakini hatujaambiwa dhahiri mikakati hii ni ipi hasa. Nitamwomba Mheshimiwa Waziri, atakapotoa majumuisho aelezee zaidi kuhusu suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ningependa vile vile Waziri atueleze namna Vyuo vya Ufundi chini ya Wizara hii vinavyohusiana na kushirikiana na Vyuo vya Ufundi vya *VETA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na ninaunga mkono hoja.

MHE. PROF. DAIMON M. MWAGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri, kwa hotuba nzuri sana na ninaiunga mkono kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie mambo mawili. Jambo la kwanza ni kwamba, utaratibu wa kuwa na Vyuo Vikuu Vishiriki ulikuwa ni mfumo uliofanya kazi wakati huo, lakini kwa sasa hakuna sababu za msingi kwa nini Chuo Kikuu Kishiriki cha Sayansi za Afya Muhimbili na Chuo Kikuu Kishiriki cha Ardhi na Usanifu Majengo viendeele kuwa Vishiriki. Utaratibu wa kuwa na Vyuo Vikuu Vishiriki ni utaratibu uliopitwa na wakati na umekuwa ukiongeza gharama na urasimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kilikuwa Chuo Kikuu Kishiriki cha Chuo Kikuu cha Afrika Mashariki, madhumuni ya kuwa na utaratibu huu ulieleweka katika kipindi kile cha historia ya uanzishaji wa Vyuo Vikuu katika Afrika Mashariki, lakini si sahihi sasa hivi kuendelea na utaratibu huo. Chuo Kikuu Kishiriki cha Muhimbili na kile cha Ardhi sasa vinakaribia miaka mitano havijaweza kuwa Vyuo Vikuu kamili. Hii ni dosari kubwa katika mfumo wa Elimu ya Juu. *Empire building* na *patronage* ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam iachwe mara moja na Vyuo vya Muhimbili na Ardhi viwe Vyuo Vikuu kamili kuiga mfano wa Chuo Kikuu cha Mzumbe na Chuo Kikuu cha Zanzibar. Kama Chuo Kikuu cha Dare es Salaam kinahitaji *University Teaching Hospital*, ule mpango wa kujenga umefikia wapi? Nashauri wajenge ya kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, katika mpango wa Wizara wa 2003/2004, Ibara ya 25 ya hotuba ya Mheshimiwa Waziri katika ukurasa wa 18, inakusudiwa kuanzisha Chombo cha Utoaji na Urejeshaji Mikopo kwa Wanafunzi. Ninashauri *seriously* kwamba, vipo vyombo vya kifedha ambavyo vinaweza

vikafanya kazi hiyo. Kwa mfano, *NMB* ni chombo cha fedha ambacho kina matawi nchi nzima na kwa sababu hiyo kipo karibu zaidi na wakopaji na kinaweza kikajenga mfumo mzuri wa utoaji na urejeshaji wa mikopo.

Kwa hiyo, sioni sababu ya kuleta Muswada wowote Bungeni bali Wizara/Serikali, iteue chombo cha fedha kilichopo hivi sasa badala ya kuunda Taasisi nyingine. Hii inafanyika vizuri, kwa mfano, kwa mikopo ya pembejeo za kilimo ambayo inapitia kwenye Benki iliyoteuliwa na Serikali.

MHE. SEMINDU K. PAWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu idadi ya wanafunzi wanaolipiwa na Serikali, naomba maelezo kwa nini idadi ya wanafunzi wanaolipiwa na Serikali katika Chuo Kikuu imepungua. Taarifa na kumbukumbu zangu zinaonyesha hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine, Morogoro, kinafanya kazi nzuri sana katika miradi yake shirikishi katika milima ya Uluguru.

- (i) Ukaushaji wa matunda kwa mionzi na jua.
- (ii) Kuezea kilimo cha mfano *Terrace System* maeneo ya Kinole.
- (iii) Uendeshaji wa kilimo cha uyoga na ujenzi wa Daraja la Kalundwa - Mgozo. Natoa shukrani nyingi sana kwa *UMADEP*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina habari kuwa Prof. Jiwa hivi sasa hayupo; je, Mradi huu wa *UMADEP* nani mbadala na nini mipango ya ujenzi wa Daraja la Gizigizi kutoka Mkuyuni - Lung'ala. Tunaomba *SUA - UMADEP* watusaidie kuhusu daraja hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kutoa mafunzo ya madreva ngazi ya Stashahada, taaluma ya udreva ni muhimu sana, je, Chuo Kikuu kinaweza kuandaa *system* hiyo?

MHE. BAKARI SHAMIS FAKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nachukua nafasi hii kumshukuru Mungu, kwa kunipa uwezo wa kufanya kazi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ndio chemchem ya kuleta maendeleo katika nchi yoyote ile na hasa ile ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi zote ambazo leo hii zimekuwa na maendeleo makubwa, pamoja na mambo mengine ni kutokana na wingi wa wataalam wa elimu za ufundi na teknolojia ya hali ya juu ya Wananchi wa nchi husika. Ni muhimu sana kwa Serikali kupitia Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, itoe kipaumbele mahsusi katika kuboresha taaluma hii nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima Serikali ifanye utafiti wa kina wa kila nyanja na hatimaye utafiti huo uwafikie walengwa na wadau mbalimbali ili hatimaye utafiti huo utuletee maendeleo. Katika hili, tunashauri kwamba, Serikali itoe fedha za kutosha ili utafiti upate kuendelezwa kwa umakini zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukuza na kuongeza wataalam, lazima Serikali ikazanie sana suala la kuimarisha Vyuo vya Ufundi nchini kote Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar na ikiwezekana hata kila Mkoa ukipata Chuo kimoja cha Ufundi litakuwa ni jambo la busara sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kuwatambua na kuwapongeza pia na kuwaendeleza wale wataalam wenye vipaji ni jambo muhimu sana. Kwani kama mtu mwenye kipaji cha sayansi na ufundi akijua kwamba Serikali imemtambua kwa kipaji chake, basi na yeye hujisikia vizuri na hapo huwa anaongeza jitihada yake katika fani hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali na kuwatambua na kuwaendeleza wataalam, suala la kuwapatia mishahara mizuri, huwapa moyo sana na hata kuwafanya wasihame kwenda nchi nyingine kwa kufuata maslahi zaidi, ambapo hasara zake ni kukosa wataalam wa fani mbalimbali na hata kuanguka kwa kiwango cha Elimu ya Juu na Ufundi nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado idadi ya wanafunzi wanaojiunga na Vyuo Vikuu nchini ni ndogo sana ukilinganisha na nchi jirani, hii itapelekea nchi yetu kuchukua muda mrefu kupata wataalam wa kutosha. Hivyo, tunashauri Serikali ifanye jitihada ili kadri miaka inavyoendelea basi na idadi ya wanafunzi iongezeke vile vile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dira ya Wizara ya kujenga na kuboresha jamii iliyoelimika itakamilika tu, iwapo Serikali kwa kupitia Wizara hii itatoa kipaumbele juu ya kuboresha Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Ufundi, pamoja na ufinyu wa Bajeti, pamoja na kuzingatia ushauri nilioutoa hapo mwanzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha ni kikwazo kikubwa sana cha kufanikisha Dira ya Wizara. Kwa hiyo basi, inashauriwa Wizara ibuni vyanzo ili kupata raslimali kwa ajili ya kufanikisha shughuli zake. Hii ni pamoja na kuunda mifuko tofauti ambayo itachangiwa na Serikali, Mashirika na wadau wengine nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja hii. Ahsante sana.

MHE. PROF. HENRY R. MGOMBELO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, kwa hotuba nzuri. Vile vile, naipongeza Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii, kwa maoni yao ambayo yamegusa sehemu zote za hotuba kwa uwazi na ukweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia katika sehemu chache tu. Kwanza kabisa, ni kuhusu kuchelewa kuanzishwa kwa Chuo cha Kampasi cha Uhandisi na Teknolojia. Ninavyoelewa, kwa upande wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, maandalizi yote yamekamilika kinachosubiriwa ni kwa Wizara kuleta Bungeni Sheria ya *Flexible University Act*. Naomba Mheshimiwa Waziri, atueleze ni lini zoezi hili litakamilika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kwa juhudi zao za kuendeleza matumizi ya teknolojia ya mawasiliano chuoni kwao. Pamoja na majukumu yangu ya Ubunge, teknolojia ya mawasiliano imeniwezesha kufundisha somo moja kwa ufanisi mkubwa. Nashauri Vyuo Vikuu vingine navyo vitumie teknolojia hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Usajili wa Vyuo vya Elimu ya Juu, nalipongeza Baraza la Ithibati la Elimu ya Juu, kwa kusitisha shughuli za Chuo cha Teknolojia na Tiba (*IMTU*) na Chuo Kikuu cha Bukoba. Nashauri Baraza hili lifanye kazi kwa ufanisi mkubwa ili Vyuo visivyofaa vifungwe mapema iwezekanavyo ili kupunguza usumbufu kwa wanafunzi wanaojiunga na Vyuo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa kukubali kimsingi kuongeza muda wa kustaaifu kwa lazima kwa wanataaluma (*Professors*) katika Vyuo vya Elimu. Nashauri kuwa zoezi la kuufanya uamuzi huo ukubalike kisheria, likamilike mapema iwezekanavyo ili tusiwapoteze wataalam hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii.

MHE. SALIM OMAR ALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, sina pingamizi na hatuba hii na nasema naunga mkono hotuba hii kwa zaidi ya asilimia mia moja (150%).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wa Elimu hii ni muhimu sana, Dira ya Taifa hili inategemea pia Elimu ya Sayansi na Teknolojia, elimu hii ndio hasa inayofuta yale mambo matatu ya ujinga, maradhi na umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu hii ndio kioo cha Watanzania wote cha kujitazama tunafanya nini, wapi na vipi. Kwa kuwa Wizara hii imejipangia mambo muhimu ya utekelezaji wake ndani ya 2003/2004 na fedha ambazo zimeombwa kwa jumla ya Sh.86,140,463,400/= bila ya kuwa na fedha za nje, basi nina mashaka kidogo kwa yaliyotajwa katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, kuwa yatatekelezeka kwa wakati uliotajwa. Naomba Mheshimiwa Waziri, anitoe wasiwasi nilionao kama itatekelezeka. Fedha alizoomba Bunge litapitisha kwa wingi wa kura za 'ndiyo' bila shaka yoyote, lakini fedha ni ndogo kuliko haja iliyopo katika Wizara yenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba nijue Chuo kina mikakati gani ya kuongeza wahitimu katika kila mwaka ili angalau tuwe sambamba na jirani zetu wa Afrika Mashariki (Kenya na Uganda).

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba nipate majibu, je, uhusiano uliopo kati ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Chuo Kikuu cha Zanzibar unatosha? Je, cheti ambacho kinatolewa kwa mhitimu wa Chuo Kikuu cha Zanzibar kinatambuliwa vizuri na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam?

Mheshimiwa Mwenyekiti, namtakia kila la kheri Waziri, pamoja na Naibu wake na watumishi wake katika Wizara yao. Ahsante.

MHE. ANNA M. ABDALLAH: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa maoni kuwa turejeshe suala la mpango wa *bounding* kwa baadhi ya wahitimu wa taaluma kwa mfano Madaktari. Hata kama watakopesha fedha za masomo yao, fedha hizo ni za umma. Ni upotevu wa *resources* za nchi kuwasomesha wataalam kisha kuwaachia katika soko huria, wakati nchi bado inawahitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. PROF. DAVID H. MWAKYUSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuipongeza Wizara hii chini ya uongozi mahiri wa Mheshimiwa Waziri Balozi Dr. Ng'wandu, kwa hotuba ambayo imeandaliwa na kutolewa kisayansi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *higher education (Umbrella Act)*, nimefurahi kuelezwa kuwa Muswada husika utaletwa hapa Bungeni katika kipindi cha mwaka huu wa fedha. Kama Mheshimiwa Waziri anavyoelewa, Sheria hii imengojewa kwa miaka mingi na matokeo yake ni kwamba, marekebisho mengi katika uendeshaji wa Vyuo yamekaa foleni yakingojea Sheria hii kupitishwa. Hivyo, tihakikishe kwamba ndoto hii inatimia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *IMTU*, matatizo yaliyojitokeza katika Chuo hiki yawe fundisho kwetu. *HEAC* inabidi kuwa macho na wawekezaji matapeli wenye ubaguzi na wababaishaji. Ningependa kupata ufafanuzi wa *footnote* ya jedwali Na.4 inayotamka kwamba hati yao imesitishwa. Najua kuliteuliwa *Probe Committee* na *the public is entitled to know the outcome of the probe*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa maendeleo ya *Mbeya Technical*. *Ultimate aim* ni ile ile ya kukifanya Chuo Kikuu? *Any time frame*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika majumuisho, naomba Mheshimiwa Waziri, akazie kwamba wakati umefika kwa Wananchi kugharamia Elimu ya Chuo Kikuu na kuacha Serikali ishughulikie mazingira na vifaa vya kufundishia ikiwa ni pamoja na mishahara ya wafanyakazi. Wenzetu nchi jirani wanafanya hivyo, harambee zinafanyika kwa ajili ya elimu. Hata hapa nchini Watanzania wengi wanagharamia elimu ya watoto wao katika Vyuo binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. FATMA SAID ALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kianzishwe Chuo cha *VETA* cha Zanzibar ili kuendeleza kwa kasi matumizi ya sayansi na teknolojia Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara kwa kuhamasisha wanafunzi wengi zaidi wa kike kujiunga na Elimu ya Juu ya Ufundi. Hivyo basi, *VETA* Zanzibar iwepo kwa kuwaandaa wasichana wa Zanzibar ili waweze kujiunga na Elimu ya Juu ya Ufundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara katika azma yake ya kushirikiana na sekta binafsi katika kuanzisha Mfuko wa Mafunzo ya ubingwa katika fani za Utawala, Biashara, Fedha na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu kwa Zanzibar tutilie mkazo fani ya uvuvi kwani Zanzibar imezungukwa na bahari na bado hatujatumia raslimali hiyo kubwa. Ingawa tunacho Kituo cha *Marine Science*, lakini bado hatujapata taaluma ya kutosha kwa ajili ya kuendeleza biashara ya uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado hatujatumia zana za kisasa za uvuvi na wala hatujaweza kuingia biashara ya kuuza samaki Ulaya na Marekani. Tukiweza kutumia sayansi na teknolojia kwenye biashara ya uvuvi, Zanzibar tutajikwama.

MHE. LEONARD N. DEREFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa ushauri na kuwatakia utekelezaji mwema wa malengo mliyojipangia kwa mwaka 2003/2004.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na upatikanaji mkubwa wa madini katika Mikoa ya Ziwa, ninashauri Wizara kuanzisha Chuo katika baadhi ya migodi hasa Mwadui kuwa na Chuo Kikuu kitakachofundisha Elimu ya *Geology* na Elimu ya Uhandisi wa Maji kutokana na tatizo la maji katika nchi yetu. Elimu hii itasaidia udhibiti wa raslimali zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na ulipuaji wa miamba katika sehemu za machimbo ambayo hutetemesha ardhi na wakati mwingine husababisha mipasuko na kusababisha baadhi ya visima na madimbwi sehemu husika kukauka, ni vyema ukafanywa utafiti na kuona kama hii ni kweli ili wachimba madini waweze kuwapa maji katika Vijiji husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kuanzisha Taasisi ya Sayansi za Bahari huko Zanzibar ni la kupongezwa sana. Ninaamini Taasisi hii itapewa vitendea kazi vya uhakika na kwa kushirikiana na Taasisi kama hizo nchi za Ulaya na Amerika katika kutafiti meli zilizozama mwambao wa (*East African Coast*) ili kuona uwezekano wa kuibua baadhi ya madini ya thamani yaliyozama. Kuna baadhi ya nchi walio na ujuzi huo wameweza kupata mapato makubwa katika kuboresha uchumi wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwambao wa *East Africa* ulianza kutembelewa na wafanyabiashara wa Asia kuanzia miaka mingi, utalam huu utasaidia sana elimu ya bahari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na ugumu wa ukusanyaji mikopo kwa wanafunzi kuwa mgumu, ni vyema fedha hizo zisiwe za kukopesha maana vijana wengi wanapomaliza masomo yao hawapati ajira kwa muda mrefu. Gharama ya kukusanya pesa hizi ni kubwa sana ni vyema katika elimu ya juu tusijisumbue kurudisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wasomi wetu wataliletea faida Taifa *indirectly* siyo *directly*. Elimu ni gharama na ni vyema suala hili likatazamwa upya. Kama vijana wetu wangukuwa wanamaliza masomo na kuajiriwa, utaratibu huu ungekuwa na maana. *Tracing cost* za wanaomaliza vyaoni na kukaa miaka mitano, hata kama anapata kazi si rahisi kujua yuko wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na nawatakia utekelezaji mwema wa malengo waliyojiwekea kwa mwaka 2003/2004.

MHE. AGGREY D. J. MWANRI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeisoma na kuisikiliza kwa hamu kubwa hotuba ya Mheshimiwa Dr. Pius Y. Ng'wandu, Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu na kwa kweli nakiri imenifurahisha na kukidhi matumaini na matarajio ya Watanzania. Naunga mkono hoja na pongezi sana.

Hata hivyo, naiomba Serikali izidi kuweka msukumo wa kibajeti kwa Chuo Kikuu Huria ambacho kinategemewa na wananchi walio wengi. Ni kweli kiasi kilichotengwa 2003/2004, kimepanda hadi Sh. 54,000,000,000/= lakini bado kiasi hiki ni kidogo hasa tukizingatia majukumu ya chuo hicho.

Naunga mkono hoja.

MHE. IRENEUS N. NGWATURA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa ya kuchangia hotuba hii muhimu. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, pamoja na Watendaji wote walioshiriki katika maandalizi ya hotuba hii. Awali ya yote naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Naomba nichangie kwa ufupi kama ifuatavyo kwa lengo la kuboresha.

Kwanza, Serikali inashauriwa kuangalia upya Muundo wa Wizara hii kwa kuondoa Elimu ya Juu na badala yake ibaki Wizara ya Sayansi na Teknolojia. Muundo huo unaopendekezwa utafanya Wizara kutumia muda wake katika masuala ya Sayansi na Teknolojia hususan utafiti na *Information Technology*. Ipo haja ya Wizara hii kuwa na chombo cha juu cha ushauri wa Sayansi na Teknolojia wa Kitaifa.

Pili, Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Wizara ielekeze nguvu zake vijijini mfano wananchi wa Mbinga huwa wanatumia mchanganyiko wa mimea kwa ajili ya kuuwa wadudu waharibifu wa mazao. Natoa ombi maalum kwa Wizara kuwasaidia wananchi hao.

Tatu, napenda Waziri anieleze jinsi anavyohusiana na Taasisi zilizopo chini ya Jeshi la Ulinzi hususan *Mzinga Corporation* na Shirika la Nyumbu. Kwa kawaida, Wanajeshi wana nidhamu ya hali ya juu na nidhamu ni msingi wa kuweza kufanya ugunduzi wa aina mbalimbali

Nne, Mheshimiwa Waziri, nimefuatilia hotuba hii lakini haisemi lolote kuhusu Kijiji cha Sayansi na Teknolojia ambacho kilikuwa kijengwe Arusha, kazi hii imefikia wapi.

Mwisho, tabia ya ukorofi wa wanavyuo na wananchi wanaowazunguka, kwa mfano ule wa Chuo Kikuu cha Mzumbe na Kijiji cha Changarawe ni aibu kwa sababu wasomi wanapaswa kuwa mfano wa uvumilivu, busara, uadilifu hasa machoni pa watu wa kawaida. Naomba hali hii isitokee tena.

MHE. SHAMIM P. KHAN: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kuwampongeza Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, Naibu Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, Katibu Mkuu wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu na wataalam wote katika suala zima la kuendeleza gurudumu la Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu. Naunga mkono hoja hii ipite bila ya kupingwa

Nashukuru kwamba suala hili limezingatiwa kikamilifu na takwimu zinatia moyo kwamba Wizara hii inafanya bidii kwa kuhakikisha kwamba idadi ya wanawake inaongezeka katika kila nyanja ingawaje *at a slow pace*. Kikubwa ni kwamba imejitahidi kuvaa *gender lens*.

Majengo, Vitendea kazi, Walimu na kadhalika kwa wanachuo wenye ulemavu tofauti. Nimevutiwa sana kwamba majengo mengi yatajengwa au yatarekebishwa. Nashauri basi michoro yenu iwa-*accommodate* hawa watu wenye ulemavu. Hii itatoa lawama kwamba, Serikali inabagua makundi hayo. Labda mngeliarifu Bunge letu Tukufu, hatua zilizochukuliwa kurekebisha tatizo/matatizo hayo.

Mwaka jana Bweni la Wasichana (Mazimbu) *SUA*, liliungua. Wasichana hao hawakuambulia kitu chochote maana walikuwa darasani. Kikubwa ni kwamba wote walinusurika. Napenda kufahamu juhudi zilizofanyika na chuo kurekebisha hali hiyo.

Ningependa kufahamu wenzetu wanawaambia/wanawashauri kitu gani juu ya matumizi ya marejea. Siku hizi dhana hii tena haisikiki kama vile ilivyokuwa mnamo miaka 10 iliyopita.

Huduma ya *TV*, hongereni, sisi wa Morogoro Mjini tunanufaika sana, lakini tukumbuke wakulima wengi wako vijijini, *it's high time* na wao wanufaika ili waongeze mavuno na tuweze kuandaa tatizo la njaa.

Tatizo la tauni - Lushoto, hili sasa limekuwa donda ndugu, wataalamu wetu wanasaidiaje ili kuondokana na tatizo hili? Kwa upande wa *SUA*, wana *Rodent Control*.

MHE. YETE S. MWALYEGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu wake, Katibu Mkuu na wataalam wote chini ya Wizara yake kwa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Ufundi Mbeya kinaandaliwa kuwa Taasisi ya Sayansi na Teknolojia. Napongeza hatua hii. Naomba kwanza nieleze kuwa Mbeya kuna Hospitali ya Rufaa. Hii ni hospitali nzuri na inahitaji kuboreshwa na kuimarishwa. Pili, Madaktari nchi hii ni wachache sana na hospitali hii ikiingizwa kwenye mpango wa kuwa sehemu ya Taasisi ya Sayansi, Teknolojia na Tiba (*Mbeya Institute of Science, Technology and Medicine*). Tatu, tunaweza kuanza na wanafunzi wachache wa Tiba, labda 20 na hapo baadaye kinaweza kupanuliwa na kuchukua wanafunzi wengi zaidi.

Walimu wa Tiba wanaweza kuwa Madaktari waliopo na Madaktari kutoka Muhimbili kwa kuanzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua ya kwanza ni kuunda sheria ambayo itazingatia yote niliyoeleza hapo juu. Tofauti hapa ni kuongeza Tiba kwenye Taasisi hiyo. Wataalam waangalie uwezekano huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante sana.

MHE. MOHAMED ALI SAIDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tukubali kwamba, Wizara hii ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, ni Wizara muhimu sana kwani Sayansi na Teknolojia ndio msingi mkubwa sana wa maendeleo katika nchi.

Kwa hiyo, ili twende sambamba na mkondo huu wa Sayansi na Teknolojia, nashauri Wizara ifanye mambo yafuatayo:-

- (a) Vyuo Vikuu viongezwe
- (b) Wanafunzi wanaoingia, katika Vyuo Vikuu waongezwe kwa mwaka, kutokana na idadi ya sasa
- (c) Wahitimu pia waongezeke angalau tuwe na idadi kama iliyoko Uganda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ningeishauri Serikali isaidiane na uongozi wa Vyuo vya Elimu ya Juu, kuhamasisha Mashirika na Makampuni makubwa yenye viwanda yachangie asilimia ndogo ya mapato yao kwa ajili ya kusaidia Serikali kugharamia masomo katika Vyuo vya Elimu ya Juu, kwa vile nao huhitaji wahitimu wazuri kwa ajira mbalimbali kwenye Makampuni yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ningeishauri Serikali iweke Kitengo maalum cha watafiti ambao kazi yao itakuwa ni kutafiti shughuli mbalimbali za Sayansi na Teknolojia. Watafiti hawa Serikali iwahudumie kwa huduma zote zinazomhusu mwanadamu.

MHE. KARIM SAID OTHMAN: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nikupongeze kwa jitihada zako za kuiendeleza Wizara hii. Pia naipongeza hotuba yako ambayo haikuacha kitu ila nina machache ya kuongezea.

Mheshimiwa Waziri, Elimu ya Sayansi ya Kompyuta ni muhimu sana katika karne hii ya leo, ningeshauri elimu hii ianze tokea madarasa ya kati na Sekondari, mshirikiane na Waziri wa Elimu na Utamaduni katika kukuza Sayansi hii. Katika nchi zilizoendelea ziko kompyuta ambazo zimetumika na bei yake ni karibu ya bure hizi zikipatikana zinaweza kuweka msingi mzuri wa taaluma hii ya Sayansi ya Kompyuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeshauri kuwe na vipindi vya *TV* ambavyo vinawaonyesha wanafunzi au watu wote ambao wana uwezo wa kuonyesha vipaji vyao vya kuvumbua mambo na vionyeshwe hadharani. Pia Wizara yako iwe tayari kuwasaidia wavumbuzi wa mambo madogo madogo fedha kwa ajili ya kupata yale ambayo yanahitaji gharama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hotuba ya Kamati ya Huduma za Jamii ukurasa wa tisa, ibara ya 4.4. kwamba, Serikali ijiandae kwa haraka kuanzisha mipango ya kunyanyua na kukuza Elimu ya Juu, kwa sababu wanafunzi wengi wanakosa kusoma elimu hiyo kwa kukosa nafasi kutokana na uhaba wa nafasi vyuoni na Serikali kukosa fedha kugharamia elimu hiyo. Kwa sababu Serikali imefanikiwa sana katika mpango wa MEM, sina wasi wsi tukianzisha mpango kama huu kwa Elimu ya Juu tutafanikiwa kukuza kiwango cha wahitimu wa Elimu ya Juu na kama hatutawapita Kenya na Uganda angalau tutawakaribia.

MHE. SHOKA KHAMIS JUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kama kawaida yangu, namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutuwezesha kuendelea na Bunge letu kwa salama na vile vile kukushukuru wewe Mheshimiwa Mwenyekiti.

Vile vile natoa shukrani za pekee kwa Waziri wa Wizara hii, kwani ni Waziri pekee ambaye alitupongeza sisi Wabunge wapya kwa maandishi sio kusema tu kama walivyokuwa wakifanya Waheshimiwa wengine. Ninampongeza kwa hotuba yake kwani amepanga vizuri sana na inaeleweka kila kifungu hakuna kitu kilichokuwa kimefichwa kwa hakika ni Waziri mzuri kabisa. Sasa nikianza kuchangia hoja yenyewe napenda kuchangia katika Elimu ya Juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Elimu ya Juu pamoja na Ufundi ni katika mambo ambayo yametajwa katika orodha ya mambo ya Muungano. Kwa hiyo, ninamwomba Mheshimiwa Waziri, anieleze kwa faida ya Wazanzibari, Serikali ya Jamhuri ya Muungano inavisaidia vipi Vyuo vya Zanzibar ambavyo vinaendesha Elimu ya Juu.

Vile vile kwa faida yangu binafsi na wadau wengine ninaomba nipatiwe maelezo kuhusu huu Mfuko wa Elimu ya Juu unavyosaidia katika Vyuo vya Zanzibar. Mheshimiwa Waziri, ninaomba majibu usinisahau wakati wa kujibu hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda vile vile kuchangia kuhusu Chuo Kikuu cha Zanzibar, nimeona katika hotuba ya Waziri katika kiambatisho Na. 4 kimetajwa Chuo Kikuu cha Zanzibar. Lakini Mheshimiwa Waziri, alipokuwa akieleza Vyuo Vikuu namna vinavyopanga kazi zao, chuo hiki hakukitaja na wakati tunasema kwamba Elimu ya Juu ni suala la Muungano, kwa nini chuo hiki nacho hakiingizwi kwenye Bajeti ya Muungano. Vile vile napenda Mheshimiwa Waziri anieleze chuo hiki cheti chake kinatambuliwa rasmi Kimataifa au hapa Tanzania tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuishukuru Serikali kwa Chuo cha Sayansi ya Baharini kilichoko Zanzibar na ninaiomba Serikali iongoze matawi ya Chuo Kikuu, si Unguja tu lakini mpaka Pemba kwani Pemba ni sehemu nzuri ya kusomea (au kujifunzia) kwa sababu ni Kisiwa kitulivu na hakuna mambo mengi ya anasa.

Mwisho nami leo naunga mkono hoja hii ya Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, lakini na majibu nipate. Ahsante.

MHE. CAPT. JOHN Z. CHILIGATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naipongeza Wizara hii kwa kazi nzuri mnayoifanya, na kwa hotuba ya Bajeti yenye mwelekeo na malengo ya kupanua na kuboresha Elimu ya Juu. Naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka ya 1987 na 1988 Baba wa Taifa alianzisha Maadhimisho ya kila mwaka ya kuenzi kazi za Wanasayansi na wavumbuzi wa hapa nchini. Katika matukio hayo, mikutano ya wanasayansi Watanzania ilifanyika, maonyesho ya vitu vilivyovumbuliwa na Watanzania, na wanasayansi wazalendo waliotoa mchango mkubwa Kitaiifa katika kuendeleza Sayansi na Teknolojia walipewa hati za kuwatambua (*Certificate of Appreciation*).

Maadhimisho haya yalifanyika kwa miaka 2 tu kisha yakafa. Ni vema dhana hii ifufuliwe ili kila mwaka Watanzania tupate muda wa kutafakari masuala ya Sayansi na Teknolojia, wavumbuzi watambuliwe, na Taifa kwa jumla lihamasishwe kutambua umuhimu wa Sayansi na Teknolojia katika kusukuma maendeleo yetu kwa haraka.

Teknolojia ya kutumia mionzi ya jua (*Solar Energy*), ipo ngumu sana hapa nchini. Tumelekeza nguvu katika nishati ya umeme unaotokana na nguvu ya maji ambazo gharama zake ni kubwa mno. Kwa kuwa mionzi ya jua tunayo ya kutosha kabisa, tena kwa mwaka mzima, itafaa Wizara hii ielekeze nguvu zake kutafuta Teknolojia rahisi ya umeme wa mionzi ya jua. Hivi sasa mitambo ya *solar* ina bei kubwa sana hivyo usambazaji wake ni mdogo.

Changamoto iliyopo ni kutafiti njia ya kupata zana za *solar energy* za bei rahisi ili umeme huu usambazwe hadi vijijini kwa haraka zaidi na kwa gharama ndogo zaidi.

Narudia kusema kuwa naunga mkono hoja hii.

MHE. MARIAM S. MFAKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziri, Naibu Waziri na watendaji wake, kwa kuandaa hotuba ambayo inaonyesha tutokako na tuendako. Hotuba hii imeonyesha ni jinsi gani viongozi na watendaji wanavyoipenda kazi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kuchangia mambo yafuatayo:-

Kwanza, washiriki wanawake katika Vyuo Vikuu inaonekana ni wachache. Pamoja na juhudi zitakazoendelezwa na Wizara, kuwahamasisha wanawake kujiunga na Elimu ya Juu, naomba idadi iongezwe.

Pili, naiomba Wizara iongeze juhudi za kufuatilia utekelezaji wa miradi ya Nishati mbadala ikiwa ni pamoja na mkaa wa mawe, mionzi ya jua, gesi ya samadi ambayo itasaidia kuwakomboa akinamama katika adha kubwa wanayopata ya kutafuta kuni na matokeo yake kuharibu mazingira kwa kukata miti.

Tatu, Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Wizara ivishawishi vyuo vingine kwa mfano Chuo cha Biashara, Chuo cha Ustawi wa Jamii na kadhalika, ili vijana waweze kupata nafasi zaidi za kupata Elimu ya Juu, hiyo itakuwa imeongeza idadi ya Vyuo Vikuu.

Naomba kuunga mkono hoja hii.

MHE. MASOUD ABDALLA SALIM: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Spika kwa namna anavyoliongoza Bunge hili Tukufu. Aidha, ninampongeza Waziri, Naibu Waziri na timu yake ya wataalam katika Wizara hii ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, kwa namna walivyoyagusa mambo yote muhimu katika Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hali ya kujitutumua ya kuelimisha jamii, ninaishauri Serikali kuwapatia nafasi za ongezeko kwa wanawake kuingia katika Vyuo Vikuu kwani inaonekana idadi ya wanawake wanaojiunga na vyuo hivyo ni ndogo sana kama inavyojionyesha katika Chuo Kikuu Kishirikishi cha Ardhi na Usanifu Majengo kama ilivyojitokeza katika hotuba hii katika ukurasa wa tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishauri Serikali kuongeza idadi ya kompyuta katika Vyuo Vikuu, ambapo Serikali iwatengee walemavu idadi maalum ya kompyuta ili na wao waweze kujifunza kwa wakati wowote wa ziada kwani walemavu wa aina zote ni sehemu ya jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika dunia hii ya karne ya 21 ya Sayansi na Teknolojia, idadi ya Vyuo Vikuu hapa petu Tanzania ni kidogo sana na kupelekea usumbufu mkubwa katika Mikoa mingi kufutika hadi kufanikiwa kujiunga na vyuo hivi, hivyo ninaishauri Serikali kuongeza idadi ya Vyuo Vikuu hapa Tanzania ikitilia maanani kwamba, kila Mkoa unahitaji huduma hiyo, hasa ukilinganisha wenzetu nchi jirani za Uganda na Kenya wameshatutangulia mbele zaidi maradufu katika mbio hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishauri Serikali kwa namna ya pekee, iwe karibu na uongozi wa Vyuo Vikuu kwa kutambua kero zao hasa ni pamoja na posho, marupurupu na mafao mengine mbalimbali, hii itaijengea sifa Serikali kwa wanavyuo kuondokana na taiba ya migomo ya kila wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishauri Serikali iandae mpango kamambe wa kupunguza ada ya gharama kwa wanafunzi hawa wanaojiunga na vyuo mbalimbali, aidha gharama ya ada hizi zilingane na zisitofautiane kwani tofauti ya gharama za ada zinaweza zikachochea bughudha na ghasia katika vyuo hivyo.

MHE. DR. ASHA-ROSE M. MIGIRO: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda awali ya yote kuunga mkono hoja hii ya Mheshimiwa Dr. Pius Ng'wandu, Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu. Nampongeza pia Mheshimiwa Zabein Mhita, Naibu Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, pamoja na Watendaji wote na Wizara hii kwa hotuba nzuri, ya kina na iliyojaa matumaini kwa maendeleo ya Taifa letu.

Baada ya kusema hayo ningependa pia kupongeza juhudi zote zinazofanywa na vyuo na Taasisi zetu zote za Elimu ya Juu kwa mchango wanaotoa kuelimisha jamii zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza kuwa Vyuo vyetu viendeleze kazi nzuri inayofanywa kufikisha taaluma na matokeo ya tafiti zao kwenye ngazi za chini kabisa za jamii. Hivi sasa baadhi ya taaluma na tafiti hizi zinafika kwenye ngazi ya Serikali Kuu na labda ngazi ya Mkoa na Wilaya. Hata hivyo, upo uwezekano wa kuwafikia wananchi kupitia Taasisi zilizopo karibu zaidi na wananchi. Ningeomba kutoa rai kwamba, tafiti hizo ziwekwe katika lugha nyepesi na mbinu rahisi na zifikishwe kwa wananchi kupitia kwa mfano, Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi, *Folk Development Colleges (FDCs)*. Vyuo hivi vipo katika kila Mkoa wa Tanzania Bara na Mikoa mingine ina vyuo hivi zaidi ya kimoja. Napendekeza vyuo vyetu na Taasisi za Elimu ya Juu viweke utaratibu wa mawasiliano na *FDCs* ili matunda ya matokeo hayo yawafikie wananchi.

Maeneo ambayo yanaweza kunufaika na ushirikiano kati ya Vyuo Vikuu/Taasisi za Elimu ya Juu na *FDCs* ni Teknolojia nyepesi/rahisi na iliyo sahihi katika, kukuza kilimo, ufugaji bora, kilimo cha umwagiliaji, ujenzi wa nyumba za bei nafuu, usindikaji wa vyakula na kadhalika. Kwa kuwa *FDCs* hasa zinawalenga wananchi waliopo jirani navyo, basi endapo uhusiano huo utajengwa, kutakuwa na nafasi nzuri ya wananchi hao kupata taaluma hizo moja kwa moja.

Napongeza uanzishaji wa Vyuo Vishiriki. Nina imani itasaidia sana utendaji na utoaji wa Elimu ya Vyuo vyetu Vikuu. Napendekeza Wizara ibuni utaratibu utakaovipa Vyuo Vishiriki, kwa kushirikiana na Baraza la Ithibati ya Elimu ya Juu (*Higher Education Accreditation Council*) ili waweze kudhibiti viwango vya vyuo mbalimbali vinavyozuka kila kukicha. Ni kweli Baraza lina dhamana hiyo ya Ithibati, lakini kwa maoni yangu, Vyuo Vishiriki katika maeneo yake mbalimbali vinaweza kuwa vyepesi zaidi kubaini upungufu/udhaifu katika vyuo hivi vingine vinavyozuka kama vile *IMTV*, vyuo vingine vya utabibu na kadhalika.

Baada ya kusema hayo napenda tena kuipongeza Serikali na hususan Wizara hii, kwa kazi zake nzuri za kukuza taaluma, Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. BENITO W. MALANGALILA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kuipongeza hotuba nzuri ya Mheshimiwa Waziri.

Mchango wangu napenda niuanze na pongezi kwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa kupunguza ada kwa wanafunzi wanaojilipia, hatua hii inatakiwa kupongezwa sana kwani inatoa nafasi kwa vijana wengi kuweza kusoma elimu ya Chuo Kikuu.

Jambo la pili ni migogoro isiyoisha ya Taasisi ya Ufundi ya Dar es Salaam (*DIT*), inaonyesha wazi kuwa Taasisi hiyo ina malalamiko mengi na ya muda mrefu kuanzia utungaji mitihati, vyeti vya kuhitimu,

huduma kwa wanachuo na walimu, mfumo wa uwajibikaji na mambo mengine mengi. Ni dhahiri na wazi kuwa cheti kinachotolewa *DIT* kiitwacho *Advanced Diploma in Engineering*, kina utata mkubwa na matatizo mengi. Hata usajili wao katika Bodi ya Uhandisi una utaratibu tofauti na wale wahitimu toka Kitivo cha Uhandisi Dar es Salaam na Vyuo Vikuu vingine. Ushauri wangu ni kuwa *DIT* iimarishwe kwa maana ya wanataaluma, vifaa na ziboreshwe sifa za wanafunzi Taasisi ile iwe sehemu ya Chuo Kikuu cha Teknolojia cha Dar es Salaam (*Former Faculty of Engineering of the University of Dar es Salaam*).

Pia nashauri Wizara iwe na utaratibu wa kutathmini *training ration* ya *Engineers Vs Technicians Vs Artisans*, ili tusiwe na *Engineers* wengi kuliko *Technicians* na *Artisans*.

Pia nipongeze sana kazi nzuri inayofanywa na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, ingawa wanafunzi katika Chuo Kikuu Huria wanalipa ada kidogo, lakini gharama za kuendesha chuo hiki ni kubwa kwa sababu mfumo wake wa uendeshaji ni tofauti na Vyuo Vikuu vingine hivyo, naishauri Serikali itoe fedha za kutosha kuwezesha shughuli zote za kitaaluma kuendeshwa ipasavyo. Pia nikipongeze chuo hiki kwa kuwa na wanafunzi wa kutosha na kutoa mchango mkubwa sana wa kutoa elimu nchini.

Pia nashauri liundwe Baraza au Tume ya Kutathmini Ubora wa Elimu inayotolewa katika Vyuo Vikuu nchini, tukio lililotolewa katika Chuo Kikuu kimoja cha Madaktari pale Dar es Salaam kinaiaibisha nchi, ningependa kupata maelezo hali ile imefikia pale kwa sababu gani?

Ziko athari nyingi, nchi yetu itapata kama utaingia utapeli katika elimu, nadhani ni vema kuwa na *Accredition Council* ya mara kwa mara kutathmini ubora wa elimu katika Vyuo Vikuu, kwa sababu hata Vyuo Vikuu vilivyo bora kabisa katika kipindi fulani na mazingira fulani vinaweza kuporomoka kitaaluma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. HERBERT J. MNTANGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe pongezi kwa Mheshimiwa Waziri wa Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, Mheshimiwa Naibu Waziri, Viongozi wote na Watendaji wa Wizara hii kwa hotuba yao nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii sasa lazima ifanye jitihada kubwa katika kuongeza idadi ya wanafunzi wanaoingia Chuo Kikuu. Hali ya Udahili mwaka 2002/2003, inaonyesha kuwepo kwa idadi kubwa ya wanafunzi walioiva kiuwezo kuendelea na Elimu ya Chuo Kikuu, lakini Serikali inakosa uwezo wa kuwalipia wakati walezi wa wanafunzi hao pia hawana uwezo wa kuwalipia na pia kwamba vyuo vyenyewe havina uwezo wa nafasi ya kuwapokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeze Wizara hii kwa mpango wake wa kuanza kuongeza madarasa na majengo muhimu katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Njia hii pamoja na kuongeza walimu na kuimarisha Mfuko wa Elimu ya Juu, ndio njia ya uhakika ya kuboresha mkakati wa kuongeza idadi wa wanafunzi kwenda Chuo Kikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tufikie lengo la kuwa na wanafunzi 13,000 watakaoweza kuingia Chuo Kikuu kwa mwaka 2008, ni lazima tuwe na mpango wa ongezeko endelevu kwa idadi ya wanafunzi kutoka idadi ya 3,500 mwaka 2003/2004 kwa ongezeko la 30%, 40%, na 50% mwaka 2007/2008.

Kama inavyoonyeshwa hapa chini Base: 3,500

Mwaka	2004/05	2005/06	2006/07	2007/08
Ongezeko	30%	40%	50%	50%
Idadi	1,050	1,820	3,185	4,777
Jumla	4,550	6,370	9,555	14,332

Idadi ya ongezeko la wanafunzi Chuo Kikuu 2004 - 2008

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tupange dira yetu Kisayansi na iendane kwa pamoja na kuongezeka kwa vyombo, huduma na mahitaji mengine muhimu ili kukamilisha lengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ongezeko la idadi ya wanafunzi litaweza kufanikiwa ikiwa pia tutaimarisha Mfuko wa Elimu ya Juu ili uweze kulingana na ongezeko la wanafunzi wanaodahiliwa na kutimiza kiwango cha kukubalika kuingia Chuo Kikuu, uwezo wa madarasa na uwezo wa mfuko kuwalipia wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa uwezo wa mfuko bado haukidhi mahitaji yote, lakini wapo wazazi wachache wenye uwezo wa kuwalipia watoto wao ada, basi tujenge mazingira mazuri ya kuwahamasisha wenye uwezo wa kukubali kuwalipia ada watoto wao ili Mfuko wa Elimu uweze kuwahudumia wasio na uwezo. Mfuko uwe na kipaumbele kwa makundi yafuatayo: Yatima, watoto waliofiwa na mzazi mmoja lakini mzazi aliyehai, hana uwezo, watoto wa wastaafu na wakulima ambao hawana uwezo na wazazi wasiojiweza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vigezo hivyo vitasaidia tu katika kuchambua wale watakaostahili kulipiwa moja kwa moja au kwa mkopo wa moja kwa moja kwa mwanafunzi kufuatana na malengo na uwezo wa mfuko wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nashauri sasa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kuwa na Idara maalum ya kutoa Elimu ya Madini. Aidha, ndani ya Kitengo cha Jiolojia au kuanzisha Kitengo maalum ili kuisaidia sekta ya madini hapa nchini.

Pamoja na kuwepo kwa Chuo cha Madini Kunduchi au Dodoma, sekta hii ni muhimu sana kwa uchumi wa Tanzania na hasa jinsi Tanzania inavyoaminika kuwa na idadi kubwa ya aina mbalimbali za madini na pia kuwa na kiwango kikubwa cha madini ardhini. Sekta hii bado haina wataalamu wazalendo na ni hatari kuendelea kutegemea wageni kusimamia sekta inayoweza kuboresha uchumi wa Taifa hili, bila kujua kinachoendelea katika ubora, uchimbaji, uchongaji na uuzaji wa madini ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo sasa nakiri kuunga mkono hoja.

NAIBU WAZIRI WA SAYANSI, TEKNOLOJIA NA ELIMU YA JUU: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nami naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge waliotangulia, kuwapa pongezi za dhiti Wabunge wote waliochaguliwa katika chaguzi ndogo za tarehe 18 Mei, 2003. *(Makofi)*

Aidha, kwa niaba ya Wanawake wa Mkoa wa Dodoma na Wilaya zake zote za Kondoa, Dodoma Mjini, Dodoma Vijijini, Kongwa na Mpwapwa na kwa niaba yangu binafsi, naomba nichukue nafasi hii kutoa pongezi kwa Mheshimiwa John Samwel Malecela na Mheshimiwa Anne Malecela, kwa kufunga pingu za maisha. Wanawake wa Mkoa wa Dodoma wanamkaribisha, nyinamtemi Mkoani Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho lakini si kwa umuhimu, napenda kumshukuru kwa dhiti Mheshimiwa Balozi Dr. Pius Yasebasi Ng'wandu, Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, kwa kuwa kiongozi na mwalimu wangu mahiri kazini na kwa imani yake anayoonyesha kwangu katika utendaji wa kazi zangu. *(Makofi)*

Baada ya utangulizi huu nami naomba nichangie hoja iliyo mbele yetu kwa kujibu baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge. Mheshimiwa Jacob Shibiliti, Mbunge wa Misungwi, alitoa hoja zifuatazo: Kwanza, alitaka kujua hatua iliyofikiwa ya kugeuza Chuo cha Ushirika Moshi kuwa Chuo Kikuu Kishiriki cha Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo na pia iwapo Serikali ina mpango wa kukipandisha hadhi Chuo cha Kilimo cha Ukiriguru kuwa Chuo Kikuu Kishiriki cha Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo. Napenda kujibu hoja za Mheshimiwa Jacob Shibiliti, Mbunge wa Misungwi, kama ifuatavyo:-

Mabaraza ya Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo na Chuo cha Ushirika Moshi, yamekwisha kamilisha hatua za maandalizi ya awali hususan muundo wa Chuo Kikuu Kishiriki kitarajiwa, taratibu na rasimu ya sheria ya kuanzisha Chuo Kikuu Kishiriki. Aidha, ombi la kukibadilisha Chuo cha Ushirika Moshi, kuwa Chuo Kikuu Kishiriki cha Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo, limewasilishwa Serikalini ambapo linachambuliwa kwa hatua zaidi za utekelezaji. *(Makofi)*

Ni matarajio yangu kuwa Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika kitaanzishwa mwaka wa masomo 2004/2005. Chuo cha Kilimo cha Ukiriguru kinazalisha wataalamu wa kilimo kwa ngazi ya cheti na stashahada. Wataalam hao ndiyo wanaofanya kazi vijijini kuendeleza kilimo. Hivi sasa idadi ya wataalam hao haikidhi mahitaji ya nchi. Kutokana na sababu hiyo, badala ya kugeuza chuo hicho kuwa Chuo Kikuu Kishiriki, ni muhimu kwa Serikali kukiimarisha ili kiweze kutimiza majukumu yake kwa ukamilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile Mheshimiwa Fatma Said Ali, alitoa ushauri kuhusu Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, kuhakikisha kwamba, inashirikiana na mamlaka husika kufanya mambo yafuatayo:-

(i) Kuanzisha Kituo cha *VETA* Zanzibar kitakachotoa mafunzo ya kuendeleza fani ya uvuvi; na

(ii) Kuanzisha mfuko wa kuendeleza fani za biashara, utawala na masoko kwa kushirikisha sekta binafsi kwa minajili ya kuwezesha wananchi kuchangia katika usindikaji na uuzaji wa samaki, Ulaya na Marekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Fatma Said Ali, kwa ushauri wake na tunamhakikishia kwamba, Wizara yangu imeuchukua ushauri huo na tutaufanyia kazi.

Vile vile Mheshimiwa Shamim Khan, Mbunge wa Viti Maalum, alishauri kwamba, miundombinu inayojengwa na kukarabatiwa itilie maanani mahitaji ya watu wenye ulemavu ili kuondoa dosari kwamba Serikali inabagua walemavu katika elimu ya juu na elimu ya ufundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Shamim Khan, kwa ushauri wake huo. Ni kweli miundombinu mingi iliyojengwa huko nyuma haikutoa nafasi nzuri kwa makundi ya walemavu kushiriki katika elimu ya juu na ya ufundi. Wizara yangu kwa kushirikiana na asasi zake, inahakikisha kuwa michoro na majengo yanayojengwa na kukarabatiwa yanapunguza tatizo hilo. *(Makofi)*

Aidha, Baraza la Ithibati na elimu ya juu linapokagua vyo vya elimu ya juu, hutoa maelekezo kwa vyo kujengwa *rafters* kwenye sehemu zenye ngazi kuwawezesha walemavu wanaotumia baiskeli kupita kwa urahisi. Labda nitoe mfano katika Hosteli za Mabibo, kuna kumbi mbili za mihadhara zilizoanza kutumika hivi karibuni katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, zinaweza kuhudumia walemavu bila matatizo. Wizara yangu pia kupitia Bajeti za asasi zake, hutenga fedha kwa ajili ya kuwasaidia walemavu kupata vifaa vitakavyowawezesha kusoma bila matatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu huduma ya *TV* inayotolewa na Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kwa wananchi wa Morogoro Mjini, nakubaliana na Mheshimiwa Shamim Khan kwamba, wakulima wengi wako vijijini. Hata hivyo, kwa hivi sasa *SUA* hawana uwezo wa kufikia wakulima wengi vijijini kwa kuwa vijiji vingi havina umeme. Ni matumaini yangu kuwa mara huduma za Televisheni ya Taifa itakapoimarika vijijini, *SUA* pia wataweza kuitumia kusambaza matokeo ya utafiti kwa wakulima. *(Makofi)*

Vile vile Mheshimiwa Profesa Henry Mgombelo, Mbunge wa Tabora Mjini, alitoa hoja zifuatazo, kuhusu kuchelewa kuanza kwa Chuo Kikuu cha Kampasi cha Uhandisi na Teknolojia katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Ushauri kwa Vyo vya Elimu ya Juu kuiga mfano wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa kutumia teknolojia ya mawasiliano kwa kufundishia. *(Makofi)*

Wizara imekamilisha maandalizi ya Muswada wa Sheria ya Elimu ya Juu, ambao utafikishwa Bungeni katika mwaka wa fedha 2003/2004. Kupitishwa kwa Sheria hiyo ya Bunge kutawezesha Chuo

Kikuu cha Dar es Salaam kurekebisha sheria yake na kuanzisha Chuo cha Kampasi cha Uhandisi na Teknolojia. (*Makofi*)

Ushauri wa Mheshimiwa Profesa Henry Mgombelo, kuhusu vyuo vingine kuiga mfano wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kutumia teknolojia ya mawasiliano kwa kufundishia, unapokelewa na Wizara yangu kupitia Baraza la Ithibati na Elimu ya Juu. Baraza litashauri vyuo kuwasiliana na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ili kubadilishana uzoefu walioupata katika suala hilo.

Vile vile Mheshimiwa Salome Joseph Mbatia, Mbunge viti Maalum, alikuwa na hoja mbili. Kwanza, suala la mkakati uliopo wa kutekeleza azma ya kuleta uwiano wa jinsia (*Gender Balance*) katika masomo ya elimu ya juu na pia uhusiano uliopo kati ya vyuo vya ufundi nchini, chini ya Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu na vyuo vya ufundi chini ya *VETA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Salome Joseph Mbatia, kwa mchango wake na pia kumjibu hoja zake kama ifuatavyo: Baadhi ya mikakati inayotumika kujenga uwiano wa jinsia katika elimu ya juu, ni kama ifuatavyo:-

Kwanza, kuanzisha Kamati Maalum ya Wizara ya kuratibu utekelezaji wa azma hii na vyuo kuongeza idadi ya wanafunzi wa kike katika vyuo vyote vya elimu ya juu na ufundi. Pili, kuanzisha *pre-entry programs* katika vyuo vyote ili kuongeza uwezo wa kitaaluma kwa wanafunzi wa kike. Tatu, kutoa kipaumbele cha nafasi za malazi chuoni yaani mabweni kwa wanafunzi wa kike. Nne, kuteremsha kiwango cha chini cha sifa za kujiunga na vyuo yaani *cut off points* kwa wanafunzi wa kike. (*Makofi*)

Vyuo vya Ufundi vilivyo chini ya Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, hutoa mafunzo ya ngazi ya ufundi sanifu (*Technician*) na uhandisi (*engineering*) ili hali vyuo vya *VETA* hutoa mafunzo ya ngazi ya ufundi stadi, wahitimu wa mafunzo ya ufundi stadi huweza kujiunga na mafunzo ya ufundi sanifu na hatimaye ya stashahada ya juu ya uhandisi. Aidha, Baraza la Elimu ya Ufundi (*NACTE*) inayoratibu masuala ya ubora wa elimu itolewayo na vyuo vya ufundi linashirikiana kwa karibu na *VETA* kutekeleza jukumu lake hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile Mheshimiwa Lekule Laizer, Mbunge wa Longido, yeye alikuwa na hoja ya elimu ya juu kwa wasichana wa Kimasai. Wanafunzi huchaguliwa kujiunga na Vyuo Vikuu kutokana na matokeo ya mitihani ya kidato cha sita na wengine hujiunga na vyuo vikuu wakitokea sehemu za kazi wakiwa na *equivalent qualifications*. Vyuo vina jukumu la kudahiri wanafunzi kulingana na taratibu zilizopitishwa na *Senate* na mabaraza ya vyuo. Hata hivyo, Baraza la Elimu ya Juu limetoa mwongozo kwa Vyuo Vikuu ya kujiweka mikakati ya kuongeza idadi ya wanafunzi wa kike wakiwemo wasichana wa Kimasai katika Vyuo Vikuu ili mradi mikakati hiyo haiathiri ubora (*quality*) ya elimu itolewayo na Vyuo Vikuu vyetu. Kwa maana hiyo wasichana wa Kimasai nao wamo katika kundi ambalo linapewa kipaumbele. (*Makofi*)

Vile vile Mheshimiwa Semindu Pawa, alikuwa na hoja ya Mradi ya *UMMADEP* na ujenzi wa Daraja la Gizigizi kutoka Mkuyuni hadi Lung'ara. Napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Semindu Pawa, kwa kufuatilia kwa ukaribu zaidi utekelezaji wa mipango ya Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo na napenda kujibu hoja zake kama ifuatavyo:- (*Makofi*)

Mradi wa *UMMADEP* ulikuwa mpango wa maendeleo wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo. Mradi huu ulikuwa ukifadhiliwa na Ufaransa, ukiwa na malengo ya kuwawezesha wananchi wa Morogoro kujiendeleza katika shughuli za kilimo cha mboga na matunda. Mradi huu ulikuwa na mafanikio makubwa na uliwanunulia wananchi gari la kusafirisha mazao yao kutoka mashambani hadi Morogoro Mjini na Dar es Salaam kwa mauzo. Mradi huo haupo tena tangu mwaka 2001 baada ya ufadhili wake kwisha. Hivyo basi, uwezo wa kifedha wa chuo ni mdogo kwa chuo kuweza kujenga Daraja la Gizigizi. Pamoja na ufadhili wa *UMMADEP* kutoka Ufaransa kwisha, chuo kinaendeleza mradi wa *UMMADEP* kwa kutumia wataalam wake katika kitivo cha kilimo, idara ya mimea vipando, hivyo basi, kufariki kwa Profesa Jiwa, hakuathiri utekelezaji wa malengo ya Mradi huo. (*Makofi*)

Vile vile Mheshimiwa Profesa Daimon Mwaga, alikuwa na hoja ya kuwa Vyuo Vikuu Vishiriki kuwa viwe Vyuo Vikuu kamili. Napenda kumjibu Mheshimiwa Daimon Mwaga kama ifuatavyo: Vyuo Vikuu duniani vimekuwa na utaratibu wa kuwa na Vyuo Vikuu Vishiriki. Madhumni ya kuwa na Vyuo Vikuu vishiriki ni kutoa nafasi kwa taaluma mbalimbali kukua katika Kampasi pamoja na kipindi cha mpito kwa Vyuo Vikuu Vishiriki kujenga uwezo kabla havijawa Vyuo Vikuu kamili. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kina Vyuo Vikuu Vishiriki viwili yaani Chuo Kikuu Kishiriki cha Sayansi za Afya Muhimbili na Chuo Kikuu cha Ardhi na Usanifu Majengo. Wizara yangu inakamilisha taratibu za kuvifanya vyuo vikuu katika kipindi kifupi kijacho baada ya vyuo hivyo kukidhi viwango kama vilivyowekwa na Baraza la Elimu ya Juu. Kuhusu chombo cha utoaji mikopo kwa wanafunzi, Serikali imekuwa ikitoa mikopo kwa wanafunzi wanaosoma katika Vyuo Vikuu vya Umma.

Lakini marejesho ya mikopo hiyo yamekuwa na matatizo kutokana na sababu nyingi zikiwa ni pamoja na kutokuwa na utaratibu mzuri wa kuwa na anwani za wahitimu baada ya masomo yao. Matatizo hayo ni kama vile ya ufuatiliaji, ukwepaji wa marejesho na kadhalika. Kama nilivyoeleza kwenye hotuba yangu, Wizara yangu inatayarisha mikakati ya kuhakikisha kuwa mikopo hiyo inayotolewa kwa wale wanaohitaji inarejeshwa kikamilifu. Mikakati hiyo italetwa Bungeni mara itakapokamilika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Benito Malangalila, Mbunge wa Mufindi Kusini naye alikuwa na hoja. Hoja ya kwanza ilihusu matatizo ya muda mrefu ya Taasisi ya Teknolojia ya Dar es Salaam yaani *DIT*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu inaupokea ushauri wa Mheshimiwa Mbunge wa kuimarisha Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam kwa kuipatia wanataaluma na vifaa vya kutosha. Ili kuboresha taaluma katika Taasisi, aidha, Wizara inatambua uwiano hafifu uliopo kati ya wataalam wa uhandisi, mafundi sanifu na mafundi stadi na inalifanyia kazi katika mpango wa kupanua mafunzo katika ngazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ilihusu uhakiki wa ubora wa elimu itolewayo katika Vyuo Vikuu. Baraza la Itifaki la Elimu ya Juu ndilo lenye dhamana ya kisheria ya kuhakiki ubora wa majengo, programu za masomo, sifa za walimu na wanafunzi pamoja na taratibu za uongozi katika Vyuo Vikuu. Kasoro zilizoonekana katika Chuo Kikuu cha Tiba na Teknolojia Dar es Salaam yaani IMTU, zilichunguzwa na Kamati maalum ya Baraza na kisha kuelekezwa kurekebisha kasoro hizo. Tayari Chuo hiki kimechukua hatua zilizoagizwa na Baraza na hatua inayofuata ni Baraza kuthibitisha marekebisho hayo ili Chuo kiweze kufikiriwa kwa hatua ya ithibati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kulikuwa na hoja ya maslahi ya wanafunzi watafiti. Serikali inatambua umuhimu wa kutoa maslahi mazuri kwa wanataaluma na watafiti na watumishi kwa ujumla kama motisha na kuhakikisha utendaji wa kuiletea nchi yetu maendeleo. Viwango vya mishahara na marupurupu mengine yatarekebishwa kadri ya hali ya uchumi itakavyoruhusu.

Kulikuwa kuna hoja ya migomo ya wanafunzi Vyuoni. Wizara imeteua Tume inayoongozwa na Mwanasheria Mwandamizi Dr. Hawa Sinare ili kuchunguza sababu ya kutokea migomo Vyuoni na kupendekeza njia za kuepusha isitokee.

Mwisho, kuhusu utafiti wa dawa za asili, Chuo Kikuu Kishiriki cha Sayansi za Afya Muhimbili kina Taasisi ya Madawa Asilia. Majukumu ya Taasisi hizi ni pamoja na kuwahusisha Waganga wa Jadi na kuwatafuta huko waliko Vijijini. Mpaka sasa Taasisi imekwishatembelea Mikoa 13 na taarifa wanazozipokea ikiwa ni pamoja na mimea na matumizi yake, inatunzwa katika *data base* za Taasisi husika. Aidha, Taasisi ina mikakati ya kutunza mimea yenye dawa kwa njia mbili. Ya kwanza, inayojulikana kama *insector conservation* ambayo wanawashauri Waganga wa Jadi kuitunza hapo ilipo ili isitoweke kwa mfano wanapochimba mizizi wasichimbe mizizi yote na kama ni kutoa magamba basi wasitoe gamba lote. Pia, Chuo kinamiliki mashamba ya hifadhi ya mimea ya dawa ambayo yapo Lushoto, Arusha, Kilema na Kibaha. Katika mashamba haya wataalam wa Taasisi ya Madawa Asilia huotesha na kutunza kwa nia ya kuhifadhi mimea ya dawa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kujibu baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge, naomba nimalize kwa kuunga mkono hoja hii ya Waziri kwa asilimia mia moja. Ahsante. (*Makofi*)

WAZIRI WA SAYANSI, TEKNOLOJIA NA ELIMU YA JUU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii kuja kuungana na wenzangu kuchangia kwenye hoja hii lakini hasa katika kutoa majumuisho ya hoja yetu. Napenda kumshukuru Naibu Waziri wangu, amejitahidi kutoa maelezo kwa baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge. Namshukuru sana. *(Makofi)*

Waliochangia katika hoja hii ni Waheshimiwa Wabunge 43 ukimjumuisha Naibu Waziri wangu aliyemaliza sasa hivi. Waliochangia kwa mazungumzo hapa Bungeni ni 12 na waliochangia kwa maandishi sasa wamefikia 32 maana Dr. Slaa naye ameleta maandishi yake sasa hivi tu nikiongea. Kwa hiyo, napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa mchango ambao wametoa kwa ajili ya Wizara yangu. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge wasiachie hapa, hii ni Wizara nyeti, ni Wizara ambayo kweli kweli tunahitaji. Mchango wao usiishie Bungeni hapa, Wizara hii haipo kwa muda wa siku moja inapojadiliwa Bungeni, ipo wakati wote. Tunaomba mchango wenu. Ni mambo mazito yanayozungumzwa, sio rahisi kufikia uamuzi kwa sababu mambo mengine ni ya kisiasa na mengi ni ya kiuchumi. Kwa hiyo, tunaomba msaada wenu. *(Makofi)*

Haitakuwa vizuri kufikiria kwamba tutaweza kujibu hoja zote za waliozungumza na walioandika sasa hivi. Nyingine zinahitaji muda mrefu wa kufikiria na kutafakari na kutoa majibu yaliyosahihi au yaliyokaribia usahihi. Kwa hiyo, tunaomba kwa unyenyekevu mkubwa na heshima kwamba tusiposema hapa sio kwamba majibu hayapo, kwanza muda wenyewe ninaopewa ni mdogo na vile vile unyeti na uzito wa hoja wakati mwingine zinahitaji utafiti. Kwa hiyo, naomba tu nizungumze kwa ujumla. Waheshimiwa wote ninawapatia ahadi ile ile ya umuhimu jinsi walivyotoa hoja zao, lakini nitaanza na wale ambao walikuja hapa kwa kuwakilisha Kamati au kuwakilisha Kambi ya Upinzani. Hao wanastahili angalau nijibu hoja zao.

Kwa upande wa Kamati ya Huduma za Umma, tumefanya nao kazi kwa ukaribu sana. Napenda kumshukuru Mheshimiwa Kwaangw' na wasaidizi wake ambao mmewaona hapa, Mheshimiwa Aisha Kigoda, Mheshimiwa Margaret Mkanga, wamewakilisha vizuri sana Kamati hiyo. Mawazo ya Kamati ambayo tumeyachambua kwa pamoja tumeyaafiki mia kwa mia. Nashukuru sana na siwezi kusema zaidi kwa sababu tumekubaliana na maoni ya Kamati. *(Makofi)*

Maoni ya upande wa Upinzani, sijui kama mliona tofauti, kuna tofauti kidogo katika namna Mheshimiwa Mutungirehi alivyoshiriki. Kwanza tuko pamoja kwenye Kamati; pili, nimemwonyesha hotuba yangu kabla haijachapwa; tatu, nimemwonyesha mipango kabambe ya Wizara yangu. Kwa hiyo, ikamsaidia kidogo kuweza kutayarisha hotuba yake. Natoa rai tu katika mpangilio wetu wa Bunge, Kambi ya Upinzani wapewe nafasi ya kutosha na vile vile vitendea kazi zaidi ili waweze kuboresha na kuandika hotuba kwa ukamilifu zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipokuwa tunazungumza, Mheshimiwa Mutungirehi bahati mbaya hayupo hapa, tulizungumza katika msingi wa kama ile tunasema a *loyal opposition*. Nilimwomba atoe mkakati mbadala, asirudie kusema tu ambayo nimesema. Aseme kingine na alijitahidi kufanya hivyo. Tunaweza kutokukubaliana naye, mimi sikubaliani naye na mkakati ule kwa sababu nina mkakati wangu. Lakini alijaribu kutoa mkakati mbadala na ndivyo ilivyotakiwa, napenda kumshukuru. *(Makofi)*

Kwa moyo huo, sitaki kusahihisha sahihisha aliyozungumza, kwa sababu takwimu zangu zinajulikana na mimi nina uwezo wa kupata takwimu kuliko yeye, kwa hiyo takwimu zangu ni sahihi. Sasa hakuna haja ya kuleta malumbano hapa, tutamsaidia tukipata takwimu sahihi ili tutofautiane tu katika tafsiri ya takwimu, lakini tusitofautiane kwenye takwimu. Ndio utaratibu wa Bunge lililokamilika. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo, napenda kuwatambua sasa wasemaji waliozungumza. Kwanza namtambua Mheshimiwa Zabein Mhita, Naibu Waziri wangu, amezungumza hapa, wa pili, Mheshimiwa Margaret Mkanga, aliyezungumza kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii, Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi, Mbunge wa Kyerwa na Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Remidius Kissassi, Mbunge wa Dimani, Mheshimiwa Bernard Membe, Mbunge wa Mtama, Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji, Mbunge wa Muyuni, Mheshimiwa Bernadine Ndaboine, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Suleiman A. Sadiq, Mbunge wa Morogoro Kaskazini, Mheshimiwa Kidawa

H. Saleh, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Margareth Mkanga kama Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Benson Mpesya, Mbunge wa Mbeya Mjini na Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, Mbunge wa Viti Maalum. *(Makofi)*

Waliotuandikia ni Mheshimiwa Prof. Henry Mgombelo, Mbunge wa Tabora Mjini, Mheshimiwa Semindu K. Pawa, Mbunge wa Morogoro Kusini, Mheshimiwa Anna Margareth Abdallah, Mbunge wa Lulindi, Mheshimiwa Jacob Shibiliti, Mbunge wa Misungwi, Mheshimiwa Prof. Simon Mwaga, Mbunge wa Kibakwe, Mheshimiwa Fatma Said Ali, Mbunge wa Mlandege, Mheshimiwa Shamim Khan, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Michael Laizer, Mbunge wa Longido, Mheshimiwa Salome Joseph Mbatia, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Dr. Asha-Rose Migiro, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Mwalyego, Mbunge wa Mbeya Vijijini, Mheshimiwa Leonard Derefa, Mbunge wa Shinyanga Mjini, Mheshimiwa Capt. Chiligati, Mbunge wa Manyoni Mashariki, Mheshimiwa Benito Malangalila, Mbunge wa Mufindi Kusini na Mheshimiwa Herbert James Mntangi, Mbunge wa Muheza. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mbunge wa Siha; Mheshimiwa Salim Omar Ali, Mbunge wa Tumbwe, Mheshimiwa Ireneus Ngwatura, Mbunge wa Mbinga Mashariki, Mheshimiwa Bakari Shamis Faki, Mbunge wa Ole, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mbunge wa Micheweni, Mheshimiwa Mohamed Ali Said, Mbunge wa Wingwi, Mheshimiwa Karim Said Othman, Mbunge wa Chambani, Mheshimiwa Mariam S. Mfaki, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Masoud Abdalla Salim, Mbunge wa Mtambile, Mheshimiwa Prof. David Mwakyusa, Mbunge wa Rungwe Magharibi, Mheshimiwa Hadija Kusaga, Mbunge wa Temeke, Mheshimiwa Aisha Magina, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Aziza Sleyum Ali, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Grace Kiwelu, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Anne Kilango, Mbunge wa Kuteuliwa, Mheshimiwa Major Jesse J. Makundi, Mbunge wa Vunjo na Mheshimiwa Dr. Willbrod Peter Slaa, Mbunge wa Karatu.

Nawashukuru sana kwa michango yenu ambayo ni madhubuti kabisa, itatusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba uniruhusu kwa sababu muda unakuwa mdogo sana niseme hivi, wote mmetuagiza na kutushauri, Serikali kwa ujumla wake na hususan Wizara yetu ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu kujielekeza na kuelewa kwamba Elimu ya Juu ni elimu muhimu ambayo inatusaidia katika maendeleo ya Taifa. Bila Elimu ya Juu na bila sayansi haiwezekani kabisa kujikwamua katika hali zetu duni na haiwezekani kabisa kujikwamua kwenye umasikini uliokithiri. Ndivyo mlivyosema kwa maneno yenu ya namna yake, ndivyo tulivyoelewa sisi mmetuambia hivyo. Pia fedha itolewe ya kutosha kuelekezwa katika utafiti, katika kuendeleza sayansi na kudahili wanafunzi wengi zaidi ili wapate Elimu ya Juu hii. Ndivyo tulivyosema au siyo? Nadhani tumesema hivyo kwa ujumla wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kabla sijasahau, alipokuwa anajibu hoja hapa Mheshimiwa Naibu Waziri, alimsahau kidogo ndugu yangu Mheshimiwa Sadiq ambaye alizungumzia sana Vyuo vyetu na wote tunakubaliana naye. Sitaki kujibu yote, lakini kuna la maana sana ambalo nilitaka kujibu. Ni lile la barabara ya kutoka pale kwenye njia kuu kwenda Mzumbe. Hilo halijasahauliwa, tunalifanyia kazi na kama barabara zinavyojengwa katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Vyuo Vikuu vingine na Chuo Kikuu kipya hiki, nacho tutakielekeza nguvu kiweze kuonekana na hadhi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda sasa ili kukubaliana katika hoja yetu sisi wote hapa na nyie, nionyeshe kwamba hata *President* wa Benki ya Dunia anakubaliana na sisi jinsi mlivyoshughulikia hoja yetu. Naomba sasa nimnukuu huyu *President* wa Benki ya Dunia, Bwana James D. Wolfensohn Rais wa Benki ya Dunia alipokuwa akizindua Kamati ya Kazi ya Benki ya Dunia kuhusu Elimu ya Juu na Jumuiya tarehe mosi Machi, 2000, alikuwa na haya ya kusema juu ya umuhimu wa Elimu ya Juu katika maendeleo ya Taifa na naomba kumnukuu kwa Kiingereza, wakati wa kutafsiri kwa Kiswahili sina. *"It is impossible to have a complete education system without an appropriate and strong Higher Education System. I am not for a moment suggesting a spring that Primary Education and Secondary Education are not at the very essence of Development but that is not enough. You have to have Centers of Excellence and learning and training. If you are going to advance the issue of Poverty and Development in Developing Countries. The key issue here is Higher Education not just only the technological side but to create people with enough wisdom to be able to use it."* *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo ningependa nijielekeze katika udahili. Naomba niazime kabisa masikio yenu hapa, imesemwa na wasemaji wengi kwamba sisi tuko nyuma katika kudahili wanafunzi katika Vyuo Vikuu. Nakubali tuko nyuma. Lakini nadhani ni nusu ukweli unaotamkwa hapa. Hebu sikilizeni ukweli wenyewe ulivyo. Imesemwa kwamba Makerere wana watu 30,000 na Nairobi wana wanafunzi 80,000, lakini hatukuelezwa *breakdown* wanafunzi hawa ni wa namna gani. Nataka kusema, Makerere pamoja na Vyuo Vikuu vya Chambongo, pamoja na Mbarara wote kwa pamoja kuna wanafunzi 29,000 tu. Kati ya hao ni 4,000 tu wanaodhaminiwa na Serikali. Hapa Tanzania ninao wanafunzi 23,000 ambao wapo Vyuo Vikuu. Asilimia 87 ya hao wanalipiwa na Serikali. Sitaki kutetea sera hiyo! Sera hiyo ndio imetudidimiza kutopata wanafunzi wengi. Tunahitaji kutoka kwenye sera hii kwamba asilimia igeuzwe. 87, walipiwe na watu binafsi, tutakwenda mbele zaidi kuliko Uganda na Kenya. (*Makofi*)

Taratibu tunazo na tumezifanyia kazi. Katika *Master Plan* zetu za Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia ambazo zinatusukuma kuelekea huko, mpango wetu ni kwamba sasa hivi tunapokuwa na wanafunzi niliowataja katika Vyuo Vikuu, Vyuo Vikuu vya Kitaifa, tuondokane na wanafunzi 10,400 katika mipango yetu na kufikia wanafunzi 30,000 ifikapo mwaka 2010 na ndivyo mpango wetu kabambe unavyosema. Kwa hiyo napenda kuwahakikishieni Waheshimiwa Wabunge kwamba mikakati huo tutautekeleza na tutaandamana nao kabisa na mtatusaidia katika kuboresha hoja yetu ili tuweze kupata hizo fedha. Fedha hizo tumeainisha katika mkakati wetu na mpango wetu kabambe. Imeonyeshwa kabisa *The Financial Plan*.

Kwanza Serikali yenyewe itaelekeza fedha na nguvu zake kwenye Taasisi na Asasi hizo za Elimu ya Juu kuweza kuwapatia nguvu na uwezo wa kujenga *capacity* ya kuchukua wanafunzi. Tatizo hapa sio kwamba wanafunzi wachache tu kwamba Serikali haidhamini wanafunzi au inadhamini wachache, ni kwamba katika Vyuo vyenyewe, kuna nafasi chache.

Waheshimiwa Wabunge watakubaliana na mimi kwamba hatutaki kupeleka wanafunzi Chuoni ambapo watakuwa wanagawana nafasi za ukaa, tuseme kwenye chumba cha mhadhara kinachotosha watu 50 tuingize watu 300 au watoke wakasomee nje. Mimi naamini kabisa hilo litakuwa ni kushusha hadhi ya Chuo Kikuu.

Kwenye *Laboratory* badala ya kuwa na watoto 16 unakuwa sasa na vijana 30, utafanana na yule mwanamke niliyewaambieni wakati fulani, aliyekuwa anajua kupika akafika sehemu hizo, hizo za usukumani kule, akakuta watu wengi sana akahubiri na wakashindwa kujua kupika mboga za majani. Hali kadhalika ndivyo itakavyokuwa.

Kwa hiyo, la kwanza ni kuvipatia Vyuo vyetu hivi uwezo. Kuviboresha kama mlivyosema kwa haki kabisa *DIT* iboreshwe. Lakini ningependa kuwaalika Wabunge waende tena *DIT* waliokuwa wameiona *DIT* kabla hatujaichukua. Kumekuwa na mabadiliko makubwa sana. Mimi nakifahamu Chuo changu cha *Dar es Salaam Technical College* tangu miaka ya 57 inayotajwa.

Leo ni Chuo tofauti sana na ndio sababu kimeteuliwa kuwa ndio Kituo pekee katika *SADC* cha *Culture of Maintenance*. Huwezi kuwa na *Culture* na *Maintenance* kama huna kitu kibaya. Wale walijua namna ya kutengeneza vitu ndio sababu wakateuliwa, wakapewa *The Culture of Maintenance*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, nataka niende kwa haraka kidogo nikimjibu Mheshimiwa Mutungirehi. Amesema sera ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia ya mwaka 1985 inahitaji kurekebishwa. Napenda kujiarifu Bunge lako Tukufu hapa kwamba sera hii ilikwishahuishwa tayari miaka kumi iliyopita baada ya kuwepo na hivi sasa Wizara yangu kama nilivyotaja katika hotuba yangu inatarajia kuihusisha tena sera hiyo.

Kuhusu mpango kabambe wa *Master Plan* ambao Mheshimiwa Mutungirehi alitushauri, pamoja na kwamba alikuwa tayari ameshaandika hotuba yake kabla hajasoma, kwa sababu mpango wa *Master Plan* upo ambao nimeueleza hapa. Kwa hiyo, tunashukuru kwamba anasisitiza tuutekeleze huo mpango

ambao tumekwishausindika tayari na kuuzindua. Ulizinduliwa tarehe 22 Machi, 2003 katika sherehe iliyohudhuriwa na waalikwa wengi ikiwa ni pamoja na Waandishi wa Habari na Mabalazi kadhaa. Uzinduzi huu ulitangazwa kwa Vyombo vya Habari nchini kote. Mpango huo umefafanua utaratibu wa utafiti utakaokuza sayansi na teknolojia nchini.

Kuhusu kuunda chombo cha Taifa kitakachofanya utafiti wa kutoa ushauri, napenda kutoa ufafanuzi ufuatao:-

Chombo kinachosimamia na kutoa mwega kwa Asasi na utafiti nchini, kimeshaundwa na Sheria Na.7 ya mwaka 1986 iliyounda Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia. Asasi, utafiti na ushauri katika Sekta kadhaa za uchumi zilianishiwa kwa sheria zilizotungwa na Bunge hili hususan katika mwaka 1979 na 1980. Asasi hizo ni kama *TIRDO*, *NIMR*, *STAFOR* na nyinginezo baada ya kuvunjika kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki ziliundwa hizo Asasi.

Asasi na Mashirika haya ni vyombo vingine moja kwa moja chini ya Wizara na Sekta husika lakini vimeshirikishwa kikamilifu na Tume ya Sayansi. Labda kwa ujulisho wa Bunge lako Tukufu, chombo hiki cha *COSTEC* Mwenyekiti wake kwa muda mrefu sasa amekuwa ni Waziri wa Sayansi na Teknolojia.

Aidha, Tume yangu imeunda Kamati ya Taifa ya Bioteknolojia ambayo hushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais, Wizara ya Kilimo na Chakula na Asasi na wadau wengine, tunaandaa sera ya Taifa ya Bioteknolojia na mwongozo kuhusu matumizi ya Bioteknolojia ambayo inaitwa *National Biotechnology Policy and National Biosafety Guideline*. Wizara yangu inatarajia kukamilisha rasimu na sera hii na miongozo hiyo ifikapo Desemba mwaka huu.

Mheshimiwa Mutungirehi alituasa na kutushauri tuunde Mfuko wa Sayansi na Teknolojia. Napenda kutoa maelezo kwa furaha kwamba sura ya tano ya sheria Na.7 ya mwaka 1986 iliunda Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia imeunda tayari Mfuko wa Taifa wa Uendelezaji Sayansi na Teknolojia yaani MTUSATE kwa Kiswahili na kwa Kiingereza *The National Fund for the Advancement of Science and Technology (NFAST)*. Kwa hiyo, mfuko huu tunao. Mfuko huu ulizinduliwa rasmi tarehe 1 Julai, 1995 na aliyekuwa Rais wa Zanzibar, Mheshimiwa Dr. Salmin Amour, ambaye alichangia Shilingi milioni tano. Mfuko huo hupata mchango rasmi kutokana na Bajeti ya Wizara yangu. (*Makofi*)

Kuhusu jarida litakalotoa matokeo ya utafiti uliofanywa tangu uhuru hadi leo, napenda kueleza yafuatayo:-

Tume ya Sayansi na Teknojia na Vyuo Vikuu vya Dar es Saalam na Sokoine vimeshaandaa mtandao wa mawasiliano katikati ya wanasayansi ili waweze kutumia *Data Bank* za utafiti. Hadi sasa mradi wa ukusanyaji wa taarifa kuhusu utafiti wa afya umekamilishwa na Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu yaani *The National Institute for Medical Research (NIMR)* na kuchapisha tafiti za miaka 50 iliyopita. Vyuo Vikuu pia vinaandaa *Data Bank* hiyo ambayo itawezesha wanasayansi na wadau wengine kwa ujumla kunufaika na mtandao wa mawasiliano utakapokamilika. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Mutungirehi kwa ushauri wake, napenda kumhakikishia kwamba mkakati wake mbadala tutauangalia na kama tutaona unafaa tutauingiza katika mpango wetu kabambe wa Wizara. (*Makofi*)

Kuna jambo lingine ambalo nataka niliweke wazi na napenda kuwapongeza na kuwashukuru Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ambacho kilichukua jukumu la kueleza wazi kabisa huu mkanganyiko kuhusu udahili na ufadhili wa wanafunzi. Walieleza vizuri kabisa na nashukuru magazeti yaliandika vizuri. Wamesema kwamba wao pale *University of Dar es Salaam* hawana nafasi 6,000.

Wanafunzi wanaomaliza Elimu ya Sekondari Kidato cha Sita ambao wana sifa ni 5,222 tu. Sasa 6,000 wanaokwenda University of Dar es Salaam wanatoka wapi? Kwa hiyo, wale wa *University of Dar es Salaam* bahati nzuri wakatoa kabisa maelezo na ninawashukuru sana na magazeti yakaandika vizuri. Nawashukuru sana. Wananchi wanapaswa kufahamishwa vizuri ukweli. (*Makofi*)

Sasa ukweli uko kwamba, waliomaliza *Form Six* ule Mwaka 2002 katika *Division* ya kwanza na ya pili ni 5,222. Ni asilimia kama 34 hivi. Sasa waliodahiliwa nimeona kwamba ni elfu mbili na kitu.

Kwa ujumla waliodahiliwa katika Vyuvo vyote wamebakia vijana 1,800 tu. Hawa wanahitaji kujigharamia wenyewe.

Elimu ni gharama! Kwa sasa hivi ambapo hatuna utaratibu wa kuwa-*target* watu sawasawa, kigezo ni kuanza ku-*merit* ushindi uko namna gani. Wale ambao wameshinda vizuri zaidi, Serikali hakuna vigezo vingine ndio tunawalipia kufuatana na fedha tuliyoanayo.

Sasa tutaleta hapa Bungeni utaratibu ambao pengine utaondoa utaratibu huu ambao watu watakopa. Ukiangalia Uganda asilimia 87 wanajitegemea wao wenyewe. Asilimia iliyobaki ambayo ni vijana 4,000 tu ndio wanasomeshwa na Serikali.

Kenya hakuna anayesomeshwa na Serikali, wote wanajigharamia wenyewe kwa kuchukua mkopo. Sasa labda tumejikwaza sisi wenyewe. Haiwezekani! Hakuna nchi Serikali iliyogharamia wanafunzi wenyewe ikaweza kupanua elimu, *no way!*

Korea ni mfano wa nchi ambayo naweza kufananisha Korea na Ghana. Huu ni utafiti uliofanywa na *World Bank*. Ghana waliendelea na mtindo wetu huu wa Serikali kugharamia wanafunzi wote, lakini pato la Taifa lilikuwa linafanana kati ya Korea na Ghana mwaka 1957. Leo Korea ina wanafunzi wengi zaidi kuliko Ghana.

Idadi ya wanafunzi wa Ghana wame-*stagnate* pale pale kwa sababu Serikali inawalipia. Lakini 85 percent ya wanafunzi kule Korea wanajisomesha wenyewe. Hili sio kwamba Hatuwezi kufanya, watu ukiweka kisomo cha bure, Mheshimiwa Mbunge mmoja amesema utafiti umesema kwamba watakoafaidi ni wale ambao wana uwezo ndio watafaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata kwenye dawa, ukifanya mambo ni bure, wale watu ambao wana uwezo zaidi ndio watazichukua nafasi za bure hizo na wale maskini kabisa hawatapata nafasi. Tusijidanganye! Huu ndio ukweli wa uhakika.

Sasa tutaweka utaratibu ambao utakuwa una-*target* makundi kama yalivyotajwa na Mheshimiwa Laizer kwamba kuna makundi ya wanawake, makundi ambayo ni watu ambao hawajapata hii, unataja tu makusudi, wazee, vijana, unawataja makusudi. Unaweza hata kusema kwamba Mikoa fulani ambayo ina nafasi ndogo inawekewa quarter kabisa kwao ili iwe inawekeza *scholarship* kule. Haya yanawezekana na ndivyo Wizara yangu inapanga sasa hivi tuweze kufanya hivyo. (*Makofi*)

Kwa hiyo, suala hili kweli tuko wasikivu sana katika mipango yetu tumeangalia miundo na mitindo mbalimbali ya jinsi ya kuweka utaratibu wa kugharamia elimu ya juu ambayo inaweza ikanyanyua elimu ya msingi, ikanyanyua elimu ya sekondari. Eliu ya juu isipokuwa na uwezo huo hutapata walimu wa kutosha kwenda kwenye vyuo vya walimu, kufundisha walimu wako wa *primary*. Hutapata walimu wa kutosha kwenda kwenye sekondari. Kwa hiyo, hivi vinabebana pamoja, siku hizi zitachukua ramani, unajenga, unajenga msingi, wakati ule ule ukijenga kuta na wakati huo huo unajengea chini pia unajengea paa lako. Unalinyanyua unaliweka juu yake, ndivyo watakavyofanya. Naomba nimalizie kwa kusema kwamba ni kweli kabisa tunahitaji kuboresha maslahi na maduhuli na marupurupu ya wataalam wetu. Tunahitaji kuwatumia wataalam wetu na ndivyo tunavyofanya katika vyuo vyetu, tunawaandaa wataalam wetu kuweza kuhudumia jumuiya yetu kwa ushauri sanifu ambao anaufanya pamoja na kwamba kwa muda uliopita kuna watu wanatoka, wanaenda katika nchi nyingine, unaweza kuita hii kwamba *brain drain*.

Lakini si wengi sana na hata waliotoka wanarudi na ni jambo zuri hili, wanapokwenda nchi za nje kwa madhumuni ya kupata *cross fertilization*. Wanapata uzoefu mwingine wanarudi hapa wana uzuri zaidi kuliko ambao wamebaki hapa. Lakini hatupendi wataalam watakoondoka moja kwa moja kwa sababu vivutio havipo. Kwa hiyo, uwende kwa kuvutiwa kupata maarifa zaidi. Kwa hiyo, tunachukua ushauri wa Waheshimiwa Wabunge tutaufanyia kazi. Kuna ushauri mwingi uliotolewa hapa. Kuna mchango mwingi uliotolewa hapa ambao tumetoa majibu ya maandishi hapa ambayo tutayasambaza kwa Waheshimiwa Wabunge muweze kuwa nayo. Kwa haya sipendi kuwachosha Waheshimiwa Wabunge na kuiba muda wa Bunge lako Tukufu. Kwa heshima naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

KAMATI YA MATUMIZI

MATUMIZI YA KAWAIDA

Fungu 68 - Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu

Kif. 1001 *Administration and General* ... Sh. 1,674,886,151/=

MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuniruhusu kuzungumza. Nianze kwa kusema kwamba sikusudii kuondoa shilingi katika mshahara wa Waziri na wenzake. Na vile vile katika masuala ya Sayansi hayana itikadi, wala dini. Kwa sababu kama ndege inaruka kwa kanuni hiyo, ni kanuni hiyo. Katika hotuba ya Waziri na ninavyokumbuka nadhani na wewe Mheshimiwa Mwenyekiti unakumbuka tulipitisha hapa Bungeni Mfuko kwa ajili ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu.

Lakini katika hotuba ya Waziri kuna mahali ambapo inaelekea mfuko ule umetoa bilioni moja karibu na milioni 400 kwa ajili ya kuwalipia watoto yatima. Tukielewana vizuri, mimi naelewa kwamba watoto yatima katika shule za sekondari ni kitu cha msingi kabisa ambacho Taifa haliwezi kupuuza. Lakini kuna watoto yatima wanaopashwa kwenda Chuo Kikuu.

Hoja yangu ni kwamba sitaki kumweka Waziri kiti moto bali tunataka Serikali tuelewane katika madhumuni ya kuanzisha mfuko ule. Kwa sababu mfuko ule aliyeleta Sheria ya kuanzisha mfuko huu alikuwa ni Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, hakuwa Waziri wa Elimu na Utamaduni, na madhumuni yale yalilenga pale. Lakini sasa inavyoelekea matumizi ya hawa wanaodahiliwa na wengine inavyokwenda umepelekwa katika Wizara Elimu na Utamaduni. Si kitu kibaya. Lakini tunataka ufafanuzi, yale malengo tuliyoyataka kwa elimu ya juu kwamba kwa kweli gharama kwanza ya elimu ya juu ni kubwa zaidi wakati mwingine kuliko kule. Kwa sababu mtoto yule yule yatima atataka kwenda Chuo Kikuu na atataka kuwa na *uniform* na shati na vitu vingine ambavyo Serikali haiwezi kutoa. Kwa hiyo, ndiyo tunataka ufafanuzi kama hela hizi zimekwenda kwenye mfuko ule au walichanganya sasa kwamba mfuko wa elimu utahudumia hata chekechekea, elimu ya msingi, sekondari na *High School*, pamoja na Chuo Kikuu. Nilitaka ufafanuzi hapa tuelewane kwa heshima hiyo, Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka tu ufafanuzi huo.

WAZIRI WA SAYANSI, TEKNOLOJIA NA ELIMU YA JUU: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa maelezo yafuatayo. Hapa ni kosa lililofanyika kwenye hotuba. Kwenye hotuba yangu hii hamna mahali nilipoandika hivyo na hivyo ni kosa. Zile bilioni moja na nadhani ndizo hizo anazozizungumzia, hazikwenda kwa hawa kutoa ruzuku ya Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, ili zitumike kugharamia wanafunzi walemavu. Hapa imeandikwa ni wanafunzi 603 waliokosa udhamini katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI: Ninachosema katika mfuko ule ambao....

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri amemaliza kueleza.

MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI: Katika hotuba ile, Mheshimiwa Waziri ameeleza kwamba mfuko ule ambao tuliuanzisha hapa wote mfuko wa elimu kwamba umepewa bilioni 1 na milioni 400. Sijui kama anaingalia hapa kwenye hotuba yake ama haioni? Kama haioni.. Mwenye mali hajasema, wewe ulichokonoa ukasema mtajie wewe, utakuwa unampeleka...

MWENYEKITI: Ongea na Kiti Mheshimiwa Mutungirehi.

MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI: Aaa! Naongea na Kiti Mheshimiwa Mwenyekiti. Inaelekea katika ile hotuba alionyesha kwamba mfuko huo wa elimu ulikuwa umetoa bilioni 1 na milioni 400 kwenda kusaidia elimu ya msingi katika eneo hilo analolitaja.

MWENYEKITI: Ukurasa gani?

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1002 - <i>Finance and Accounts</i>	Sh. 97,228,245/=
Kif. 1003 - <i>Policy and Planning</i>	Sh. 376,401,653/=
Kif. 2001 - <i>UNESCO Commission</i>	Sh. 259,543,198/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 3001 - <i>Higher Education</i>	Sh. 59,340,985,700/=
--	----------------------

MHE. MARIA D. WATONDOHA: Nakushukuru sana Mheshimiwa Mwenyekiti. Kwa kuwa Mheshimiwa Rais alishasema kwamba wanafunzi ambao wako katika vyeo vya *private* ambao wanachukua mafunzo ya uganga, digrii ya udaktari, sio *doctorate* hapana, *degree on medicine* wataweza kulipiwa na Mheshimiwa Waziri alitoa maelezo hayo katika Bunge hili. Naomba ufafanuzi ameweka utaratibu upi na mpango huo unaanza lini ili uwe wazi na wengine waweze kuhudumiwa.

WAZIRI WA SAYANSI, TEKNOLOJIA NA ELIMU YA JUU: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa maelezo yafuatayo. Maelekezo hayo yalitolewa kweli na hatukuweka kwenye Kasma mbalimbali hapa. Lakini kama mnavyofahamu Waheshimiwa Wabunge kuna mfuko, mifuko mingi katika Serikali. Tumekubaliana mimi na Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwamba utaratibu huo uanze mara moja. Tatizo siyo fedha kwa kweli. Tatizo ni kwamba nafasi katika vyuo hivyo vya *private*. Nimezungumza nao, nimezungumza na Bugando, nimezungumza na *KCMC*, ile *capacity* bado, itabidi sasa tufanye utaratibu wa kuwasaidia hata kujenga *capacity* ili tuweze kuongeza wanafunzi wetu. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 3002 - <i>Technical Education</i>	Sh. 6,041,707,956/=
Kif. 3003 - <i>Science and Technology</i>	Sh. 1,745,492,397/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

MIPANGO YA MAENDELEO

Fungu 68 - Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu

Kif. 1003 - <i>Policy and Planning</i>	Sh. 5,921,236,300/=
---	---------------------

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 3001 - <i>Higher Education</i>	Sh. 10,212,981,800/=
--	----------------------

MHE. REMIDIUS E. KISSASSI: Mheshimiwa Mwenyekiti, *Project 4398* - Chuo Kikuu Huria (*Open University*). Nilikuwa nimetoa maelezo hapa kuwa kutokana na uhaba wa fedha hizi za maendeleo Chuo Kikuu Huria, ilikuwa kinalazimika kutumia *OC* kugharamia miradi yake. Na hii ilisababisha walimu na kazi nyingine nyingi kusimama. Imefika mahali walimu wa *part time* wametishia kugoma kusaidia kazi za *Open University*. Naomba maelezo.

WAZIRI WA SAYANSI, TEKNOLOJIA NA ELIMU YA JUU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeelewa. Ni mgao wa fedha ulivyogawanywa sasa. Ni kweli mimi mwenyewe na Wizara yangu

tusingependa mgao kwa namna hiyo. Tungependa mgao mzuri zaidi. Na katika mipango yetu kabambe wa elimu ya juu tutatilia mkazo sana utaratibu huu wa elimu inayotolewa kwa njia hii ya *distance learning* na *open learning*. Lakini kwa sasa hivi kwa hali ya bajeti yetu ilivyo ni vigumu kubadilisha. Lakini tunavyoenda tutaweza kuona ni namna gani sasa tunaweza kuwasaidia *Open University*. Lakini napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba lengo letu kwa kweli ni kuelekea huku kwenye mafunzo ya aina ya *Open University* ili iweze kuwa na wanafunzi wengi zaidi na mahitaji ya fedha kupelekwa katika eneo hili. Tumemsikiliza na ombi lake na rai yake tutaifanyia kazi. Na hii hoja iko wazi kabisa siyo ya kubishia hata kidogo, Kwa sababu ndiyo mkakati wetu huu wa kuweza kuboresha na kuongeza wanafunzi zaidi.

MHE. REMIDIUS E. KISSASSI: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninachosema ni kweli *fifty million* kwa Chuo Kikuu kikubwa kama hiki *Open University of Tanzania* ambayo sasa hivi ina wanafunzi 13,000 katika wanafunzi karibu 18,000 wanachukua masomo ya juu Tanzania nafikiri ni kidogo sana. Kwa hiyo, rai yangu ni kuwa ziongezwe.

WAZIRI WA SAYANSI, TEKNOLOJIA NA ELIMU YA JUU: Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tumekubali kwamba inafaa kuongezwa. Lakini Mheshimiwa Mbunge atakubaliana nami wakati huu utaratibu wetu wa Bunge hili hatuwezi kubadilisha. Ndiyo utaratibu tuliojiwekea katika Bunge hili. Tutafanyia kazi na hivyo tumekubali kwamba katika mipango yetu ya baadaye ni kitu muhimu sana hiki na wala siyo kwamba tukomee kwenye wanafunzi 13,000 katika mipango yetu Chuo hiki kinahitajiwa kuwa na watu 100,000 ndiyo tuweze kukidhi mahitaji ya nchi yetu. Kwa hiyo ni lazima kabisa katika Serikali nzima tutakapokaa, tutabadilisha. Lakini siyo sasa.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Kif. 3003 - *Science and Technology* Sh. 470,000,000/=

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

(Bunge lilirudia)

T A A R I F A

WAZIRI WA SAYANSI, TEKNOLOJIA NA ELIMU YA JUU: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi ya Bunge Zima imeyapitia Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu kwa Mwaka 2003/2004 kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko yoyote. Hivyo kwa heshima naomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako Tukufu iyakubali na kuyapitisha makisio haya. Naomba kutoa hoja.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge kabla sijawahoji juu ya hoja hiyo, napenda kumtambua rasmi kwenye *Gallery* ya *Diplomatic Gallery* kuna Mzee wetu, Makamu wa Kwanza wa Rais na Waziri Mkuu, Mheshimiwa Rashid Mfaume Kawawa. Baada ya makofi hayo ya heshima kubwa sana kwa Viongozi wetu, Waasisi wetu, Karibu sana Mzee wetu, Mzee Rashid Mfaume Kawawa. *(Makofi)*

WAZIRI WA AFYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

(Makadirio ya Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu yalipitishwa na Bunge)

(Saa 12.18 Jioni Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Alhamisi Tarehe 17 Julai, 2003 Saa Tatu Asubuhi)

